Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Thelathini na Moja – Tarehe 17 July, 2009**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH (K.n.y MHE. WILSON M. MASILINGI - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA):**

Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika kwa Mwaka wa 2008/2009 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010

**MHE. SALIM YUSSUF MOHAMED (k.n.y MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI (k.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA):**

Randama za Makadirio ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Mwaka wa fedha 2009/2010.

**MHE. GAUDENSIA M. KABAKA –NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Chuo Kikuu cha Ardhi kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2008 *[The Annual Report and Audited Accounts of Ardhi University for the year ended 30th June, 2008]*.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 230

### Makao Makuu ya Nchi Kuhamia Dodoma

**MHE. FELISTER A. BURA** aliuliza:-

Kwa kuwa, uamuzi wa Serikali kuhamia Dodoma kama Makao Makuu ya Nchi ulifanywa zaidi ya miaka ishirini iliyopita na kwa kuwa, hata katika ramani ya Tanzania, Dodoma huoneshwa kama Makao Makuu ya Nchi:-

Je, ni sababu gani zinazofanya Serikali kuitisha mjadala wa Kitaifa kuhusu suala hili?

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, URATIBU NA BUNGE** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felister Aloyce Bura (Viti Maalum) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi wa Serikali kuufanya Mji wa Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi ulifanyika yapata miaka 35 iliyopita. Wakati huo Serikali iliweka programu ya kuuendeleza Mji wa Dodoma na kuhamia katika kipindi cha miaka 10 kwa gharama ya shilingi milioni 370 kwa mwaka kwa kipindi chote cha programu na hiyo siyo hela ndogo kwa sababu dola moja wakati huo ilikuwa ni shilingi saba. Hata hivyo hadi sasa azma hii ya Serikali haijafanikiwa kama ilivyotarajiwa kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

(i) Ukame wa miaka ya 1974/75 uliosababisha janga la njaa kwa nchi nzima na hivyo rasilimali kuelekezwa katika kukwamua tatizo hilo.

(ii) Tatizo la kiuchumi lililotokana na vita dhidi ya Idd Amin wa Uganda.

(iii) Kupanda kwa bei ya mafuta ya petroli na dizeli katika soko la dunia kwenye miaka ya 1970 kulikosababisha bei za bidhaa mbalimbali kupanda kutokana na kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania.

(iv) Mabadiliko ya mwelekeo wa sera za uchumi wa dunia katika miaka ya 1980 yaliyochangia kuparaganyika kwa chumi za nchi zinazoendelea, Tanzania ikiwa mojawapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na changamoto hizi, uamuzi wa Serikali kuhusu azma ya kuhamisha Makao Makuu ya Nchi kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma haijabadilishwa. Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 imeainisha wazi kuhusu kutungwa Sheria itakayotambua Dodoma kuwa Mji Mkuu wa nchi yetu na kuweka utaratibu bayana utakaotambulisha shughuli za Ustawishaji Makao Makuu. Kwa hiyo sababu za kuitisha mjadala wa Kitaifa juu ya azma hii siyo kupata maoni ya kubadilisha uamuzi wa awali. Lengo la mjadala wa Kitaifa ni kupanua wigo wa majadiliano na kukusanya maoni yatakayosaidia katika mkakati na namna ya kuongeza kasi ya mchakato wa Serikali kuhamia Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, uendeshaji wa mjadala huo utalenga katika kutekeleza masuala yafuatayo:-

(i) Kuibua na kubaini matatizo yanayozorotesha kasi ya uhamiaji Makao Makuu Dodoma.

(ii) Kudurusu na kupitia upya taratibu za kisheria zilizopo zinazohusu ustawishaji wa Makao Makuu, ikiwa ni pamoja na kupata michango ya wadau mbalimbali katika mchakato wa kutunga sheria mpya ya Ustawishaji Makao Makuu.

(iii) Kubainisha wadau watakaoweza kuchangia katika kuongeza kasi ya mchakato wa Serikali kuhamia Dodoma.

(iv) Kuweka mfumo wa kitaasisi na uendeshaji utakaoratibu kwa ufanisi programu hii.

(v) Kutoa mapendekezo Serikalini kuhusu njia bora za kuwezesha au kutekeleza shughuli zinazohusu ustawishaji Makao Makuu.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, kwa kuwa uamuzi wa Serikali kuhamia Dodoma kama Makao Makuu ya Serikali na kwa kuwa uamuzi huo umeshakuwa wa muda mrefu sana kama miaka 35 iliyopita, je mjadala huo utafanyika kabla ya uchaguzi mkuu ujao?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa kuwa Ilani ya CCM ya mwaka 2005 inasema kwamba Serikali itaongeza juhudi za Wizara kuhamia Dodoma kama Makao Makuu. Je, tangu Serikali ya Awamu ya Nne kuingia madarakani, ni Wizara ngapi zimeshahamia Dodoma rasmi kama eneo la kazi?

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza mjadala huu utafanyika kabla ya uchaguzi ujao na pia napenda kuongeza hapo kwamba sheria iliyotajwa hapo awali ya kuongoza Ustawishaji wa Makao Makuu itatungwa kabla ya uchaguzi mkuu ujao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili Wizara zilizokwishahamia rasmi Dodoma ni Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, sababu alizozitoa Mheshimiwa Waziri za kuchelewa kuhamia Makao Makuu, je sababu hizo hazikutokea Dar es Salaam ambako zimejengwa ofisi mbalimbali ikiwemo ya Makamu wa Rais, Wizara ya Fedha, Magereza, Polisi na kadhalika, hizo sababu nyingine zote ulizozitoa hazikuwepo Dar er Salaam zilikuwepo hapa Dodoma tu? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika muda huo kati ya uamuzi wa kuhamia Dodoma na sasa, majengo kadhaa yamejengwa Dar es Salaam, tumeshataja mara nyingi kwamba uamuzi wa kuhamia Dodoma haujakataza kuimarisha majengo mbalimbali ya Serikali yaliyopo Dar es Salaam kwa vile hatimaye hata tukihamia Dodoma majengo hayo bado yatakuwa na shughuli zingine za Serikali.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, fedha inayotengwa kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya Mji wetu wa Dodoma ni kidogo sana na ndiyo maana kila siku watu wapo barabarani wanatengeneza barabara ambazo hazikamiliki. Je, Waziri atakubaliana nami kwamba iko haja sasa ya kutenga fedha za kutosha ili tuweze kuboresha miundombinu ya Mji wetu wa Dodoma na hasa Ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami?

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara nyingi kuu tunazoziona hapa Dodoma hazijengwi na Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu, barabara hizi zinajengwa na mamlaka ya barabara *TANROADS* na hapa Dodoma kama ilivyo miaka mingine kuna uendeshaji wa *TANROADS,* Waheshimiwa Wabunge wote wa Mkoa wa Dodoma ni Wajumbe wa Bodi ile, naomba Mheshimiwa Mbunge pamoja na wenzake kuhakikisha kwamba barabara zote ambazo ziko chini ya *TANROADS* zinatengenezwa kwa kiwango kinachohitajika na kinakidhi haja ya Makao Makuu.

Na. 231

**Sekretarieti ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi**

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika utekelezaji wa shughuli zake inasaidiwa na Sekretarieti na kwa kuwa, Sekretarieti hiyo ina watumishi Makao Makuu tu na haina watumishi Mikoani na Majimboni:-

Je, Serikali ina maelezo gani kuhusu jambo hili

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, URATIBU NA BUNGE** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mbunge wa Micheweni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 74(15) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, imeainisha wadau muhimu wanaohusika katika kuratibu na kusimamia Uchaguzi chini ya Tume kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Makamu wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Wajumbe wote wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Mkurugenzi wa Uchaguzi, Watumishi wote wa Tume ya Uchaguzi na Wasimamizi wote wa Tume ya Uchaguzi katika Miji na Wilaya zote nchini. Hivyo basi, kwa mujibu wa Katiba Tume inatekeleza majukumu yake ikisaidiwa na Sekretariati iliyo na watumishi Makao Makuu na pia katika ngazi ya Halmashauri za Majiji, Miji na Wilaya kama ilivyotajwa kwenye Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Taifa ya Uchaguzi haina Watumishi wake Mikoani na Majimboni; kwanza ni kutokana na muundo wa Tume uliopo ambao unaishia Makao Makuu ya Tume na pili, Sheria kuwataja Wakurugenzi wa Halmashauri kuwa ndiyo wasimamizi wa Uchaguzi. Suala la Tume kuajiri watumishi wa kudumu katika ngazi ya Halmashauri lina changamoto nyingi ikiwa ni pamoja na uwezo wa kukidhi gharama mbalimbali. Kwa mfano, hivi sasa kwa kipindi cha miezi mitano ya maandalizi hadi uchaguzi, Tume hutumia jumla ya watumishi 6,273 kutoka katika Wilaya na Halmashauri zote Tanzania. Idadi hii ya watumishi huigharimu Serikali karibu Tshs. 11bn/= kwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo Serikali ingeamua kuajiri watumishi wa kudumu Majimboni kwa kipindi cha mwaka mmoja, gharama yake ingekuwa shilingi zipatazo bilioni 35.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo nia ya Tume ya Uchaguzi ni kuwa na Maafisa Uchaguzi wa kudumu angalau Afisa mmoja katika kila Halmashauri ambao watakuwa wanashughulikia masuala ya kiutawala katika uchaguzi kwenye Halmashauri katika utaratibu endelevu kuliko ilivyo sasa ambapo baada ya shughuli za uchaguzi kukamilika ilivyo sasa ambapo baada ya shughuli za uchaguzi kukamilika kunakuwa hakuna Afisa kwa ajili hiyo.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Moja, kwa kuwa, Waziri amewataja Wakurugenzi wa Miji pamoja na Halmashauri za Wilaya kuwa wanatambuliwa na sheria kama wasimamizi wa uchaguzi, je, haoni kwamba hawa Wakurugenzi hawawajibiki moja kwa moja kwa Tume ya Uchaguzi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, je, Waziri huoni kwamba hawa Wakurugenzi wanalalamikiwa na wadau wa uchaguzi kwamba hawatendi haki?

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nisikubaliane naye kwamba Wakurugenzi hawawajibiki moja kwa moja kwenye Tume, Wakurugenzi hawa wametajwa kwenye Katiba. Kwa hiyo, wasipowajibika kwenye Tume basi wanakiuka Katiba na sidhani kwamba kuna Mkurugenzi mwenye kuthamini kazi yake na mwenye maadili mema atakiuka Katiba ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana kuna malalamiko ya mara kwa mara dhidi ya Wakurugenzi hawa, lakini kuna taratibu ambazo zimewekwa kisheria za namna ya kutatua matatizo yanapotokea wakati wa kuendesha shughuli za uchaguzi. Walalamikaji wakubwa ni Chama kinachotawala hasa wakati wa Uchaguzi, kwa sababu inaonekana mara nyingi huwa wanaegemea upande wa vyama vingi sana katika Wilaya wakati Chama kimoja ndicho huwa kikishambuliwa. *(Makofi/Kicheko*)

**MHE. DOKTA. WILLIBROAD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa, Waziri amekiri kwamba Chama Tawala ni mlalamikaji mkubwa na hivyo kuthibitisha kwamba kuna tatizo na kwa kuwa kuna msemo kwamba demokrasia daima ni ghali na suala la bilioni kumi na moja katika suala la demokrasia siyo suala la msingi. Je, Waziri atakubalina kwamba ili kufuta malalamiko hayo ambayo hata Chama Tawala inayo sasa ni wakati muafaka wa kuanzisha ofisi hizo katika kila Wilaya?

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, narejea kusema kwamba ni kweli Chama cha Mapinduzi ni Chama kimojawapo kinachowalalamikia sana Wakurugenzi hawa na mfano mmoja ni Jimbo la Karatu. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa vile tu shauri lenyewe lipo Mahakamani, Chama cha Mapinduzi kilikuwa na mengi ya kusema kuhusu yaliyotendwa na Mkurugenzi wa Wilaya ya Karatu wakati ule wa Uchaguzi wa mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli demokrasia ni ghali ndiyo maana Tume ya Uchaguzi inatarajia kuwa na Afisa mmoja katika kila Wilaya hapo baadaye. Lakini tukumbuke kwamba katika muda wa miaka mitano baada ya uchaguzi kwa kweli hakuna shughuli nyingi sana ambazo zitafanywa na Maafisa hawa katika ngazi za Wilaya.

Na. 232

**Mpango Mkakati wa Kuondokana na Kilimo cha Jembe la Mkono**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika kujadili mwongozo wa mpango wa bajeti ya mwaka 2009/2010, Serikali ilionesha nia ya dhati ya kuhakikisha kuwepo kwa mpango mkakati wa kibajeti wa kuwaondoa wakulima kutokana na jembe la mkono kwenda katika matumizi ya matrekta madogo na makubwa sambamba na majembe ya kukokotwa na ng'ombe:-

(a) Je, ni fedha kiasi gani zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji huo katika Jimbo la Peramiho, Wilaya ya Songea na Mkoa wa Ruvuma kwa ujumla?

(b) Je, ni utaratibu gani utatumika ili kuhakikisha zana hizo zinawafikia wakulima wadogo wadogo walioko vijijini ambao ni wazalishaji wazuri wa mazao mbalimbali?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama Mbunge wa Peramiho lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa jinsi anavyojitahidi katika kuendeleza Jimbo lake hususan katika maeneo ya kilimo, miundombinu, maji pamoja na umeme.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Katika mwaka wa fedha wa 2009/2010, wakulima wa Mkoa wa Ruvuma wameibua miradi ya kuendeleza matumizi ya zana bora za kilimo nchini chini ya Mpango wa Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *DADPs*. Katika mpango huo jumla ya sh. 1,644,070,837/= zitatumika na Halmashauri za Wilaya mbalimbali za Mkoa wa Ruvuma kwa ajili ya kununua zana za kilimo na shilingi 21,599,000/= kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa wakulima juu ya matumizi bora ya zana hizo. Mchanganuo kwa Wilaya hizo ni kama ifuatavyo:-

Halmashauri ya Wilaya ya Songea ambako ndipo lilipo Jimbo la Peramiho, itanunua matrekta madogo ya mkono yatakayogharimu sh. 300,000,000/= pamoja na sh. 11,000,000/= za mafunzo juu ya matumizi ya matrekta hayo. Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga itanunua matrekta madogo ya mkono 50 yatakayogharimu sh. 350,000,000/= na imetenga sh. 130,004,610/= kwa ajili ya kununua mitambo mitatu ya kumenyea kahawa *(central coffee pulperies*). Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru itanunua matrekta madogo ya mkono 48 yatakayogharimu sh. 458,066,323/=. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo itanunua matrekta madogo 50 yenye thamani ya sh. 325,000,000/= na mashine nane za kusindika muhogo, zenye thamani ya sh. 10,999,904/= na imetenga sh. 9,099,904/= kwa ajili ya mafunzo kwa wakulima juu ya zana hizo. Manispaa ya Songea itanunua

matrekta madogo ya mkono 10 yenye thamani ya sh. 70,000,000 na itatumia sh. 1,500,000/= kwa ajili ya mafunzo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, matrekta haya yatakabidhiwa kwa vikundi vya wakulima vilivyoibua miradi ya kuendeleza matumizi ya zana bora kwa utaratibu shirikishi wa uchangiaji wa gharama ambapo wakulima wanapaswa kuchangia kati ya asilimia 20 hadi 50 ya gharama ili kuwa wamiliki wa zana za kilimo ili waweze kunufaika na utaratibu huu chini ya Mpango wa Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya(*DADPs*).

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika kwanza nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, pia naishukuru sana Serikali kwa kuzingatia mpango wa kuboresha kilimo na hivyo kuweka *allocation* ya matrekta kununuliwa kwa ajili ya wakulima. Maswali yangu ni kwanza, kwa kuwa matrekta haya yote ambayo yamepangwa kununuliwa ili kuwasaidia wakulima yatakwenda moja kwa moja kwenye vikundi vya wakulima wadogowadogo na matrekta haya ni yale matrekta madogo, je, Waziri kwa nia njema hiyo hiyo yuko tayari kutumia Ushirika wa Vyama vya Akiba na Mikopo (*SCULT)* ili kuweza kusaidia uwezekano wa kununua sasa matrekta makubwa kwa ajili ya wakulima ambao hawako kwenye vikundi, ambao wako nje ya mpango huu wa matrekta madogo madogo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa, ajenda hii ya kilimo kwanza imepokelewa vizuri sana na Serikali na wananchi wa Tanzania kwa ujumla wakiwemo wananchi wa Jimbo la Peramiho na kwa kuwa mpango huu wa matrekta utakuwa ni mpango wa kwanza wa kuhakikisha wakulima wanaondokana na jembe la mkono, je, Waziri ama Waziri Mkuu yupo tayari kuja kuzindua mpango huu rasmi Mkoa wa Ruvuma ili waweze kupokea shukrani za wakulima hao katika kuboresha suala hili la kilimo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza suala la *SCULT* hiki ni chombo cha ushirika na ni chombo cha hiari, kwa hiyo, hilo wazo ni zuri nadhani tutawapelekea wenyewe kama watakuwa na nia hiyo basi watafanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili la kuzindua mpango wa Kilimo Kwanza, mpango huu bado uko kwenye mchakato utakapokamilika utazinduliwa rasmi Kitaifa na viongozi wakuu wa Nchi, kwa hiyo suala hili tusubiri kidogo.

Na 233

**Uhitaji wa Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Songwe**

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Jimbo la Songwe lenye Kata (10) lina Hakimu mmoja tu wa Mahakama ya Mwanzo:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kupeleka Mahakimu watatu kwenye Jimbo hilo?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dk. Guido Gorogolio Sigonda, Mbunge wa Songwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, kutokana na ukubwa wa Jimbo la Songwe linahitaji kuwa na Hakimu wa Mahakama za Mwanzo zaidi ya mmoja. Hata hivyo, kutokana na upungufu wa Mahakama za Mwanzo tatizo ambalo linazikabili karibu Wilaya zote hapa nchini, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi kwamba Serikali inahitaji kuendelea kutafuta ufumbuzi wa tatizo hili. Aidha, kwa sasa Serikali imeajiri na kuwasambaza Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ili kukabiliana na tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2009 Serikali imeajiri Mahakimu 100, kati ya hao Mahakimu wawili wamepangiwa Wilaya ya Chunya kuanzia tarehe 30 April, 2009 na Hakimu wa tatu amehamishwa Sumbawanga mnamo Januari 2009 na kupelekwa Wilaya hiyo. Hakimu mmoja kati ya hawa amepangiwa Jimbo la Songwe katika Mahakama ya Mwanzo iliyopo Mwambani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, mwenye mamlaka ya kupanga Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ni Hakimu Mfawidhi wa Wilaya kulingana na mahitaji ya kila Kata na kipaumbele kikubwa katika kupanga Mahakimu hao huwa ni wingi wa kesi katika Kata husika.

Aidha, kwa sasa Serikali imeajiri na kuwasambaza Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ili kukabiliana na tatizo hilo.

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Songwe kumshukuru Waziri kwa ahadi yake kuanza kutekelezwa. Sasa hivi tumempata Hakimu mmoja, tunakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa yule Hakimu ambaye ameletwa kwenye Jimbo la Songwe katika Mahakamani ya Mwambani anafanyakazi kwa zamu na yule mwenzake aliyekuwepo pale kwanza yaani wanafanya sehemu moja, Mahakama moja wanapangiana kama asubuhi mpaka saa nne hakimu mmoja mmoja, halafu saa saba mpaka kumaliza hakimu mwingine. Je, kwa sababu ya tatizo hilo kwamba kuna sehemu ambayo kuna majengo ya Mahakama kama Udinde haiwezekani huyu Hakimu akaagizwa kwenda kufanyia kazi kwenye Mahakama hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa sababu ahadi ya Waziri tayari imeshaanza kutekelezwa, je, ni lini hiyo ahadi itakamilika kwa kumalizia wale Mahakimu watatu ambao ulikuwa umeahidi? Ahsante sana? (*Makofi*)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kupangiana zamu kutumia chumba kimoja katika Mahakama zetu ni utaratibu wa kawaida, lakini nimelichukua hilo na kama kuna uwezekano wa kuvigeuza hivyo vyumba vilivyoko huko Udinde kuwa Mahakama basi tuangalie kama vitakuwa vimekidhi mahitaji hasa viwango, kama vitakidhi tutafanya hivyo.

Kuhusu lini tutampatia Mahakimu zaidi nataka nimwahidi kwamba kila mara tunajitahidi kupeleka Mahakimu katika Mahakama za Mwanzo. Lakini niseme katika mpango huu tunakusudia kuzigeuza Mahakama za Mwanzo kuwa ndiyo ngazi ya kwanza ya kazi ya Uhakimu na wanaoingia pale wenye digrii ya kwanza nadhani tutalitatua tatizo hili mapema kuliko tunavyofikiria. (*Makofi*)

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wilaya ya Mbozi yenye Kata 26 ina Mahakama za Mwanzo zisizozidi tano na Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo wasiozidi watatu ambao wote hukaa Mjini Vwawa ambapo ni Makao Makuu ya Wilaya. Je, ni lini Serikali itatoa kipaumbele kwa yale maeneo ya zile Kata za Wilaya hizo ambazo ziko umbali wa zaidi ya kilomita 150 kupata Mahakimu?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna upungufu wa Mahakimu katika Wilaya ya Mbozi. Lakini kama nilivyosema katika jibu langu la awali ni kwamba anayepanga Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo wakae wapi ni yule Hakimu Mfawidhi wa Wilaya. Sasa kama Hakimu Mfawidhi wa Wilaya ameona wote wakae sehemu moja atakuwa na sababu labda sehemu hiyo ndiyo yenye kesi nyingi. Lakini nitalichukua jambo hili niliangalie na wenzangu wa Mahakama tuone kwamba tunaweza tukawasambaza kulingana na viwango vya Mahakama zilizoko huko Mbozi.

Na. 234

**Malimbikizo ya Madeni ya Mishahara ya Wafanyakazi**

**MHE. JUMA SAID OMAR** aliuliza:

Kwa kuwa kuna migomo inayofanywa na wafanyakazi mbalimbali nchini kutokana na kudai malimbikizo ya mishahara yao kwa muda mrefu:-

Je, ni kwa nini kunakuwa na malimbikizo ya madeni ya mishahara ya wafanyakazi kiasi cha kuwafanya wagome?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH J. SUMARI) alijibu**:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Said Omar, Mbunge wa Jimbo la Mtambwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, malimbikizo ya madeni ya mishahara ya wafanyakazi yanasababishwa na mambo makuu yafuatayo:-

(i) Kutokukamilishwa kwa wakati taratibu za awali za uajiri.

(ii) Kuchelewa kuwasilisha taarifa za mwajiriwa katika daftari la mishahara

(iii) Kuhamisha mtumishi na kumpeleka katika kituo ambacho bajeti yake haina mshahara wa kumlipa.

(iv) Kusubiri waajiriwa katika kituo kukamilisha taratibu za awali na baadaye kuziwasilisha taarifa zao kwa pamoja?

(v) Kuchelewa kwa mawasiliano baina ya Hazina na sekta husika.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali inafahamu kiini cha tatizo, kwanza, je, ina mpango wa kukabiliana na tatizo hili ili lisiendelee tena kutokea? Pili, kwa kuwa Tanzania ni nchi inayoongozwa kwa kufuata misingi ya sheria, haki za binadamu na utawala bora, je, Serikali haioni kwamba kuendelea kufanyika kwa migomo hii kunamaanisha kwamba dhana ya sheria, haki za binadamu na utawala bora haijatekelezwa ipasavyo na kwamba inatekelezwa zaidi kinadharia kuliko kivitendo, Serikali inasema nini? Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH J. SUMARI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kuhusu mikakati gani, mikakati ambayo tunayo ni ile ambayo itajihusisha hasa na utatuzi wa haya matatizo niliyoyataja ambayo ndiyo yanapelekea kuchelewa ulipaji wa mishahara.

Lakini pili, ni kujitahidi kuongeza utendaji katika ngazi ya utendaji, kuongeza ufanisi zaidi. Lakini tatu na hili ndiyo tatizo kubwa ni kuangalia upya mifumo ya ulipaji wa mishahara na marupurupu mengine ya wafanyakazi wetu.

Lakini kuhusu haki za binadamu nchi hii, sijawahi kuona nchi nzuri kama hii ambayo inazingatia sana haki za binadamu na Serikali yake ndiyo inayosimamia jambo hilo. Kwa hiyo, sikubaliani na Mheshimiwa Mbunge hata kidogo. Hapo tutakosana. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Hamruhusiwi kukosana mbele ya Spika. (*Kicheko*)

**MHE. KHALIFA S. KHALIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba na mimi tusikosekane, anijibu swali langu. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri napenda kumuuliza kama ifuatavyo. Ni muda mrefu sasa nchi yetu imekuwa ikitumia

utaratibu wa *cash* bajeti. Kimsingi *cash budget* maana yake unatumia kile ulichonacho, kile unakikusanya, sasa inakuwaje kitu unacho halafu unawakopa watu?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH J. SUMARI):** Mheshimiwa Naibu Spika, dhana ya *cash budget* maana yake ni kwamba unatumia kile ambacho unakuwa nacho wakati ule. Tukumbuke kwamba mara nyingi Mfuko Mkuu wa Serikali hauna fedha isipokuwa unawekewa fedha kwanza kutoka kwenye makusanyo ya kodi chini ya Mamlaka ya Kodi ya Tanzania lakini vile vile na vyanzo vingine vya mapato ya Serikali.

Lakini kama nilivyosema wala tatizo la ucheleweshaji wa mishahara na malimbikizo ya stahiki za wafanyakazi hayatokani na Serikali kutokuwa na fedha, yanatokana na mapungufu haya ambayo nimeyataja hapa na mikakati ambayo nimeitaja ndiyo ambayo itapelekea kusahihisha tatizo hilo ambalo tumekuwa nalo. Lakini kuhusu fedha, fedha Serikali wakati wote inayo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Unaona swali lililoulizwa kifupi na kujibiwa kwa kifupi tumetumia dakika tano tu na maswali mawili ya nyongeza yameulizwa.

Na. 235

**Kiasi cha Dhahabu Wilaya ya Kahama**

**MHE. JAMES D. LEMBELI** aliuliza:-

Kwa kuwa maeneo mengi ya Wilaya ya Kahama yanasemekana kuwa na madini mengi hasa ya dhahabu na almasi na kwa kuwa Kahama ni Wilaya pekee hapa nchini yenye migodi miwili ya dhahabu inayomilikiwa na kampuni ya Barrick (Buzwagi na Bulyanhulu):-

(a) Je, tangu Barrick waanze kazi ya kuchimba dhahabu katika migodi hiyo miwili ni kiasi gani cha dhahabu kimechimbuliwa na thamani yake ni kiasi gani?

(b) Je, kutokana na dhahabu iliyochimbwa katika migodi hiyo, Serikali imepata shilingi ngapi katika kodi na ada nyingine na ni kiasi gani cha fedha kimetolewa na Barrick kwa ajili ya huduma za jamii kwa Wilaya ya Kahama na maeneo yanayozunguka migodi hiyo?

(c) Je, kuna maeneo mangapi katika Wilaya ya Kahama yanayoendelea kufanyiwa utafiti na makampuni yanayofanya utafiti huo ni yapi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa James D. Lembeli, Mbunge wa Kahama lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli maeneo mengi ya Wilaya ya Kahama yana madini ya dhahabu na almasi na pia kuna migodi miwili ya dhahabu inayomilikiwa na kampuni ya Barrick (Buzwagi na Bulyanhulu).

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, mgodi wa dhahabu wa Bulyanhulu ulianza uzalishaji mwaka 2001 na unatarajiwa kuwa na uhai wa miaka 20 na mgodi wa dhahabu wa Buzwagi umeanza uzalishaji mwezi Mei, 2009 na unatarajiwa kuwa na uhai wa miaka 10. Kuanzia mwaka 2001 hadi 2008 mgodi wa dhahabu wa Bulyanhulu umezalisha madini ya dhahabu wakia 2,311,984 (kilo 71,910) yenye thamani ya dola za Kimarekani 1,091,155,963. Mgodi wa Buzwagi umeanza uzalishaji mwezi Mei, 2009.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilipata mrabaha wa Dola za Marekani 31,599,260 kutokana na mgodi wa Bulyanhulu na kodi ya *skills and development levy* ya Dola za Marekani 90,119,173.

Mheshimiwa Naibu Spika,kwa upande wa huduma za jamii, mgodi wa Bulyanhulu kuanzia mwaka 2000 hadi 2008 umechangia kiasi cha Dola za Marekani zisizopungua 9,500,000 katika Wilaya ya Kahama. Aidha, mgodi wa Bulyanhulu kuanzia mwaka 2005 umekuwa ukitoa Dola za Marekani 200,000 kila mwaka kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kahama. Kuanzia mwaka 2006 hadi 2008 Mgodi wa Buzwagi umetoa Dola za Marekani zisizopungua 1,000,000 kwa ajili ya huduma za jamii kwenye Wilaya ya Kahama.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yanayoendelea kufanyiwa utafiti katika Wilaya ya Kahama ni pamoja na Nyangalata, Mwambomba, Mwazimba, Busulwangili, Ushetu, Bumbiti, Isaka, Lunguya na Segesekuna. Makampuni yanayofanya utafutaji huo katika Wilaya ya Kahama ni pamoja na *Sub – Sahara Mineral Resources (T), State Mining Corporation (STAMICO), Barrick Exploration Africa Ltd, Pangea Minerals Ltd, Tuncan Mining company Sejo Company, Savannah Mining Company Ltd, Resolute Tanzania Ltd, Mabangu Mining Ltd, Rhodolite Mines Ltd na Twigg Resources Ltd.*

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Naibu Waziri ambayo yanaonyesha dhahiri kabisa jinsi gani nchi yetu inapata fedha kidogo kutokana na madini ukilinganisha na uharibifu unaofanyika wa mazingira na madini yanayochukuliwa kwenda nchi ya nje nina maswali mawili ya nyongeza. Kwaza, kwa nini Serikali inaendelea kuridhika na mapato hayo duni kutokana na madini yetu wakati nchi yetu bado ni maskini na wananchi wanaoishi katika maeneo kama yale ya Kahama wanaogelea katika dimbwi la umaskini?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa kuwa Serikali kupitia Naibu Waziri Mheshimiwa Adam Malima alipotembelea Buzwagi mwezi Agosti mwaka jana aliwaahidi wananchi wa Kata ya Mwendakulima kwamba atashughulikia matatizo yao dhidi ya Barrick katika kipindi cha miezi mitatu, leo ni miezi 11. Je, ni lini kwa uhakika Serikali kupitia ahadi hiyo matatizo ya wananchi wale yatatatuliwa ufumbuzi? Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeingia mkataba na Barrick kupitia *mining development agreement* iliyosainiwa miaka hiyo. Serikali katika mkataba huo imeingia makubaliano ya kwamba kuna ulipaji wa mapato fulani yatakayotokana na uchimbaji huo utakaoingia Serikalini lakini utategemea pia kipindi ambacho migodi hii itaweza kurudisha fedha zake zilizotumika kwenye uwekezaji wa migodi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipindi hicho tulichojiwekea bado kwa mgodi huu wa Bulyanhulu hakijafika. Lakini pamoja na hayo napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa kitengo cha ukaguzi cha dhahabu kinachosimamiwa chini ya Wizara ya Nishati na Madini kinafanyakazi nzuri sana, nakifuatilia sana kwa karibu mapato yote, pamoja yale mapato yanatokana na kupanda kwa bei ya dhahabu na nini ili tuangalie kama tunaweza tukafanya mabadiliko yoyote ambayo tunatarajia kuyafanya katika marekebisho ya mikataba na pia kulingana na sheria mpya hii ambayo tumeileta Bungeni mwezi wa 11.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la pili la Mwendakulima, ni kweli nilikwenda kwa kutumwa na Waziri wa Nishati na Madini, tuliongea na wananchi, tumeongea na Barrick, tumeongea na watu wa Halmashauri ya pale na kuna makubaliano tuliyofikia sote kwa pamoja ya utekelezaji huo. Tatizo la pale ni tatizo la fidia ambalo utekelezaji wake ulivurugwa na pande zote. Kwa hiyo, sisi kama Serikali tunalifuatilia kwa karibu. Lakini napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, yeye mwenyewe ni sehemu ya mchakato wa kutafuta ufumbuzi wa tatizo hilo na tunafanya naye kazi kwa karibu na hivyo tunaendelea kulifuatia kwa karibu na tunatarajia kuendelea kufanya naye kazi na tutapata ufumbuzi. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Majibu yamekuwa marefu. Mawaziri majibu yenu ni marefu sana.

Na. 236

**Serikali Kujiweka Kitalaam ili Kugundua Maeneo yenye Mafuta**

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna kila dalili kuwa nchi yetu itagundua mafuta na kwa kuwa tumeona mifano kwenye nchi jirani iligundua mafuta na kuanza kuchimba mafuta:-

(a) Je, Serikali ina mipango gani ya kujiweka tayari kitaaluma pindi jambo hili likitokea?

(b) Je, Serikali imejifunza nini kwenye nchi jirani iliyopata mafuta?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna dalili za kutia matumaini sana kuwa nchi yetu itagundua mafuta na hivyo kuhitaji maandalizi ya awali ya kutosha. Kama nilivyolieleza Bunge lako Tukufu tarehe 27 Januari, 2009 kuwa uwepo wa miamba ya *Sedimentary Rocks* Tanzania Bara na Visiwani ambayo kitalaam duniani inafahamika kuwa na uwezekano wa kuandamana na mafuta inaashiria uwezekano wa kuwepo kwa mafuta na gesi asili nchini.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, mipango ya kitaaluma inayoendeshwa kwa lengo la kujiweka tayari kwa matarajio ya ugunduzi wa mafuta na gesi asili hapa nchini ni pamoja na Wizara na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (*TPDC*) kuajiri watalaam katika fani mbalimbali zinazohitajika kwa ajili ya shughuli za usimamizi wa utafutaji na uendelezaji wa mafuta na gesi asili hapa nchini katika mazingira ya sasa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejifunza mambo mbalimbali ya msingi kutokana na ziara za mafunzo pamoja na kubadilishana uzoefu kutoka katika nchi zinazozalisha mafuta na gesi ikiwa ni pamoja na umuhimu wa kuwa na sera nzuri ya kiuchumi inayotoa dira na mwongozo wa namna ya kusimamia na kuendeleza rasilimali asili za nchi zikiwemo pia zisizojadidika za mafuta na gesi asili. Vile vile Shirika la Maendeleo ya *Petroli Tanzania (TPDC)* lina mpango na linatarajia kufanyiwa ukarabati wa muundo (*restructuring*) ili kujiendesha kiuchumi na kuweza kushiriki kikamilifu katika kusimamia na kuendeleza rasilimali hii.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ipo mbioni kukamilisha mchakato wa kuboresha sera, sheria na kuandaa kanuni zitakazosimamia shughuli za utafutaji na uzalishaji mafuta na gesi asili nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria ya utafutaji, uendelezaji mafuta ya mwaka 1980 ndiyo inayosimamia shughuli hii hapa nchini. Sheria hii kama tulivyosema inapaswa kufanyiwa marekebisho ili iendane na mabadiliko yaliyotokea nchini na duniani katika utafutaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asili.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nashukuru kwamba kweli Mwenyezi Mungu kuna dalili kwamba ametujalia, tunaweza tukapata mafuta kama tulivyopata gesi katika nchi yetu. Gazeti la *The African* la wiki hii, katika gazeti hilo Jumuiya ya Afrika Mashariki inatangaza tenda ya upembuzi yakinifu wa kujenga *pipeline* ya gesi ya kutoka Dar es Salaam kwenda Tanga mpaka Mombasa. Je, Sera ya Serikali ni nini ni kupeleka nje *products* za gesi kama ilivyo?

**NAIBU SPIKA:** Hili swali mbona halifanani kabisa na swali lako la msingi? Kwa sababu wewe *exploration* sasa mitambo tena haiji hapa.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mara ya mwisho tulivyotembelea katika kituo cha jiolojia tumegundua kwamba nchi yetu

ina *geologists* wachache sana yaani idadi yao ni 40 ukilinganisha na China ambayo ina watalaam kama hao zaidi ya milioni nne na kwa kuwa sasa hivi nchi yetu inajipanga hasa katika kuhakikisha kwamba rasilimali nyeti zinapatikana na zitapatikana kwa kuwa na watalaam kama hao. Je, Wizara itakubaliana nami kwamba ni vema sasa ikatenga sehemu ya fedha inayopatikana kutokana na migodi yetu kwa ajili ya kuwasomesha watalaam kama hao? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, swali lako nalo liko nje ya lile la msingi lakini Naibu Waziri jibu kwa sababu *exploration* na watalaam wetu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kusema tu kwamba kwa mfano wa China, China ina watu bilioni na zaidi, Tanzania ina watu milioni 40 kwa hiyo, kusema kweli kwa uwiano huo China ina watu wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza kwamba *TPDC* ina mkakati wa makusudi kabisa ambao unasimamiwa na Wizara wa kuongeza watalaam na kwa sasa hivi tumeridhia na katika bajeti tukayoleta wiki ijayo *TPDC* iongezewe watalaam. Katika miaka iliyopita walioajiriwa tumewaongezea *TPDC* wa jiolojia 18 na wahandisi 14. Yote haya ni kupelekea kuwa na *base* kubwa zaidi ya utalaam ndani ya *TPDC* lakini pia ndani ya Wizara yenyewe. Kwa hiyo, hili suala linafanyiwa kazi.

Na. 237

**Tofauti ya Ada kwa Vyuo Vilivyoko katika Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki**

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR (k.n.y. MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE)** aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka 2004 Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki lilipitisha uamuzi unaovilazimu Vyuo Vikuu vya Umma ndani ya Jumuiya kutoza ada zinazofanana kwa wanafunzi wote wanaotoka nchi wanachama wa Jumuiya:-

Je, ni vyuo vingapi vinavyotekeleza uamuzi huo tangu ulipotolewa na vyuo vipi vimekaidi uamuzi huo na vinaendelea kuwabagua wanafunzi toka nchi wanachama kwa ada.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Harrison George Mwakyembe, Mbunge wa Kyela kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo Vikuu vya Umma Tanzania vilianza kutekeleza haya maamuzi ya kuwatoza wanafunzi wa Uganda na Kenya kama raia wa Tanzania na wala si kama wageni katika mwaka wa 2005/2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Tanzania kuanza kutekeleza maamuzi haya kwa miaka miwili yaani 2005/2006 na 2006/2007 Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilibaini kwamba wanafunzi wa Tanzania wanaosoma katika nchi hizo kwa udhamini binafsi wanatozwa ada kama wanafunzi wanaotoka nje ya eneo la Afrika Mashariki na kuarifu uongozi wa *IUCEA*. Kwa kuwa uongozi wa *IUCEA* na vyuo wanachama vya *IUCEA* hawakuchukua hatua yoyote. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na vyuo vingine viliamua kusitisha utaratibu huo katika mwaka 2007/2008 na kuanza kuwatoza ada wanafunzi wanaotoka katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa mtindo unaotumika katika nchi wanachama wa Jumuiya hiyo.

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ushirikiano wowote ukikosa makubaliano kuna teteresha kuaminiana. Je, Serikali yetu imechukua hatua gani kuirekebisha kasoro hii? Pili, je, tukio hili halitutanabaishi sasa kuwa makini zaidi kwa makubaliano mengine ndani ya ushirikiano wetu? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwamba nchi zote za Jumuiya zilikubaliana kwamba wanafunzi hawa wanapokwenda katika nchi ambayo ni mwanachama wa Jumuiya basi ada ile ipunguzwe na iwe kama ada anayotozwa mwanafunzi wa nchi ile ile. Sasa kwa kuwa majirani zetu hawakukubaliana na hilo, basi sisi hatua tuliyochukua ni kuwa kama wao na sisi kuwatoza wanafunzi wao kama wanavyowatoza wa kwetu.

Lakini nakubaliana na wewe kwamba makubaliano yakishafanyika ni vizuri yaheshimiwe na nchi zote za jumuiya. (*Makofi*)

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa maamuzi haya yalifikiwa na Baraza la Mawaziri na ni dhahiri Baraza la Mawaziri lilitakiwa liendelee kuyasimamia kwamba yanakubalika na yanaendelea kuheshimika na vyuo vyote. Sasa baada ya Vyuo Vikuu vya Kenya vimepuuza na sisi tumepuuza hivyo ndivyo tunavyotakiwa kwenda au Mawaziri walitakiwa wakae kupitia upya uamuzi wao? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli maamuzi haya yalipitishwa na Vikao vya Baraza la Mawaziri lakini yalipovunjwa na vyuo husika basi hakukuwa na sababu tena ya Mawaziri kukaa kwa sababu uamuzi ule ulishapita.

Na. 238

**Ujenzi wa Chuo cha *VETA* Wilaya ya Bukombe**

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika Ilani ya CCM 2005, Ibara ya 64 (b), kuna maneno ya angalau kuanzisha *VETA* kila Wilaya na kwa kuwa Wilaya ya Bukombe tumetenga eneo zaidi ya ekari 70:-

(a) Je, ni lini Serikali itaanzisha ujenzi huo ili kukidhi utashi wa Ilani yetu ya CCM 2005?

(b) Je, kama Serikali itashindwa ujenzi huu, wananchi na vijana wa Bukombe wapewe maelezo gani?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel J. Luhahula, Mbunge wa Bukombe lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Mbunge, Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe na wananchi wote kwa kutenga eneo kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha *VETA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, azma ya Serikali ya kujenga Vyuo vya *VETA* vya Wilaya katika Wilaya 28 zisizo na Chuo cha Ufundi bado inaendelea. Hadi sasa maandalizi ya awali yamekwishafanywa kwa vyuo vyote 28. Kama tulivyosema katika jibu la swali namba 185 la tarehe 09/07/2009, lililoulizwa na Mheshimiwa Bujiku Philip Sakila, Mbunge wa Kwimba. Hivyo natoa wito kwa wananchi wote na vijana wa Bukombe kuwa na subira wakati Serikali ikiendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa chuo hicho.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa maandalizi yameshafanywa Wilaya 28 ikiwemo na Wilaya ya Bukombe. Je, maandalizi hayo ni yapi na Waziri anaweza akanipa kwa maandishi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa nikimaliza Bunge nitakwenda kufanya ziara na moja ya hoja nitakazozisema ni uanzishaji wa vyuo vya *VETA* na katika jibu wamesema wananchi wa Bukombe na vijana wavute subira. Je, Serikali inaniambia nini wavute subira mpaka awamu ipi ya uongozi ya nne au ya tano?

**NAIBU WAZIRI ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Luhahula kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, maandalizi yaliyokwishafanywa, kwanza ni kuhakikisha kwamba kila Halmashauri imetenga viwanja. Kama nilivyowahi kusema siku moja hapa nitapitia kuona kwamba Halmashauri hizi zimetenga viwanja kama tulivyokubaliana na kuviona *physically*. Lakini pili, Wizara imekwisha- *establish study* zinazotakiwa kufundishwa katika kila eneo kulingana na mazingira yaliyopo, kwa hiyo hii ni sehemu ya pili ya maandalizi. Lakini pia, ramani inayohusika na hivi vyuo imekwishaandaliwa pamoja na maandalizi mengine ni pamoja na kuandika *proposal* ambayo tumepeleka kwa wafadhili ili kuombea pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali la pili mtasubiri mpaka lini. Nafikiri hili watasubiri mpaka tupate pesa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante tunaendelea na swali lingine linalofuata Wizara ya Miundombinu, Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo.

Na. 239

**Kupandishwa Hadhi Barabara ya Mtwara – Tandahimba – Newala Masasi**

**MHE. JUMA A. NJWAYO** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Mtwara – Tandahimba – Newala – Masasi iliidhinishwa na kupitishwa na Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Mtwara kuwa ya Kitaifa kutokana na umuhimu wake kiuchumi na kijamii:-

Je, ni hatua gani zimechukuliwa na Serikali za kuipandisha hadhi barabara hiyo hadi sasa?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mbunge wa Tandahimba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Barabara namba 13 ya mwaka 2007, barabara za Kitaifa zinajumuisha barabara kuu na barabara za Mikoa.

Barabara ya Mtwara – Tandahimba – Newala – Masasi yenye urefu wa kilometa 211, ni barabara ya Mkoa na kwa hiyo ni barabara ya Kitaifa inayosimamiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara nchini (*TANROADS*).

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la kuzipanga barabara zote nchini katika madaraja stahili kulingana na vigezo vilivyowekwa katika Sheria ya barabara Na. 13 ya Mwaka 2007 pamoja na Kanuni zake za Januari 2009, umekamilika mwezi Mei, 2009. Pendekezo la Mkoa wa Mtwara kupitia Bodi ya Barabara ya Mkoa la kupandisha hadhi barabara ya Mtwara – Newala – Masasi kutoka hadhi yake ya Mkoa na kuwa barabara

kuu, halikuafikiwa kwa sababu barabara hii kwa sasa haikukidhi vigezo vilivyowekwa ambavyo vimewekwa kwa mujibu wa sheria.

**NAIBU SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Njwayo.

**MHE. JUMA ABDALLAH NJWAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa matengenezo yanayofanywa kwenye barabara hiyo inaigharimu sana Serikali kutokana na mizigo mizito inayopita na hivyo kuifanya ihitaji matengenezo ya mara kwa mara na kuiletea Serikali gharama kubwa. Je, Serikali haioni kuwa ufumbuzi wa kudumu ni kuweka lami?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa barabara ya Mtwara-Tandahimba - Masasi -Newala ndiyo barabara kuu ya kiuchumi ya Mkoa wa Mtwara na ndiyo inayounganisha Wilaya zote za Mkoa wa Mtwara na nchi jirani ya Msumbiji. Je, kigezo hiki hakitoshi kupata hadhi ya kuwa barabara kuu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, naafikiana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kwamba matengenezo ya mara kwa mara hugharimu Serikali fedha nyingi. Lakini kama ambavyo sote tunajua kwamba Serikali na wananchi kwa ujumla wote tungependa kujenga barabara hizi kwa kiwango cha lami ili tupate ufumbuzi wa kudumu wa matengenezo ya mara kwa mara, lakini kinachotutatiza ni ufinyu wa bajeti na kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Mbunge kwa sasa tuendelee kuvumilia kuendelea na matengenezo haya ambayo sasa hivi Serikali inayafanya kuhakikisha kwamba barabara hii inapitika wakati wote na kuweza kuwahudumia wananchi wa Mkoa wa Mtwara na Mikoa ya jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, nimeeleza hapa katika majibu yangu ya msingi kwamba, vigezo vlivyowekwa kwa mujibu wa Sheria sasa hivi pamoja na kanuni zake, havikuweza kufikiwa na barabara hii kuweza kupandishwa hadhi. Lakini kama nilivyosema, zoezi la kupandisha hadhi au maombi ya kupandishwa hadhi barabara ni zoezi la kudumu, litakuwa linaendelea huko mbele ya safari tunaweza tukaangalia uwezekano kama barabara hii inaweza ikakidhi vigezo vilivyowekwa.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Alivyozungumza Mheshimiwa Naibu Waziri ni vizuri. Lakini kusema kweli kama akiangalia vigezo mbalimbali vilivyopo pale, ulinzi, mambo mengi kabisa kwa nini wasibadili nia hii ya barabara hii kuwa ya kawaida badala yake waone umuhimu huu wa kuwa barabara kuu? Hili linatutesa sana kwa kipande kile ambacho kinapitisha korosho zote na kila kitu.

**NAIBU SPIKA:** Mrope uwe unauliza swali la nyongeza, uliza swali la nyongeza.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo. Mheshimiwa Waziri tafadhali hebu ubadili hali hii kusudi iwe Barabara kuu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri nawe kwa kifupi maana yake limeshajibiwa.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi kwamba, kwa taratibu za sasa hatuna uwezo wa kukiuka kanuni zile ambazo tumejiwekea kufatana na Sheria ya Barabara, Sheria namba 13 ya mwaka 2007, kwa hiyo tutaendelea kupanga barabara katika staili husika kwa kutumia Sheria na kanuni hizo. Lakini nimwambie Mheshimiwa Mrope na Waheshimiwa Wabunge kwamba kufuatana na kanuni sio kwamba hatutojenga barabara hiyo kwa lami, tayari barabara hiyo imeanza taratibu za kuijengea kwa lami, kuna kilomita 15 katika barabara hiyo ambayo tayari ziko katika kiwango cha lami na mwaka huu wa fedha 2009/2010 kuna kilomita tisa ambazo zinatarajiwa kujengwa katika kiwango cha lami. Mwisho barabara nzima itakuwa imejengwa katika kiwango cha lami.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha na maswali yenyewe yamekwisha. Waheshimiwa Wabunge, lazima nikiri kwamba, Mawaziri wengi wamejitahidi sana sana kujibu maswali yao kwa kifupi, kwa sababu ukiangalia majibu yao ni *page* moja tu jibu limetosha. Lakini tatizo lililopo si kwa Mawaziri peke yao hata Waheshimiwa Wabunge katika maswali ya nyongeza, mnaungana na gazeti moja lililosema Wabunge mnatakiwa kulipa muda mnaotumia. Sasa Mheshimiwa Mbunge ukianza nashukuru, nafanya hivi na hivi, muda wa saa za asubuhi hautoshi kushukuru, uliza tu swali.

Ni kweli maswali ya nyongeza yanatakiwa kuwa matatu na ni dakika tano. Pia kwa upande wa Mawaziri likiulizwa swali akiliona ni zito anatakiwa ajibu yeye, basi asimame kwa sababu inakuwa ni rahisi zaidi kuliko tukitumia muda mara mbili. Kwa hiyo tunakwenda hivyo kwa sababu tukiwa na tabia za kuwa tunazembea, tutakuwa tunazembea. Kwa hiyo, ndiyo maana nimekuwa *strict*, lakini nafurahi kwamba Mawaziri wengi wametumia muda mchache. Kama safari hii nilikuwa naandika kila swali limetumia dakika ngapi. Maswali yaliyotumia dakika kumi ni moja, dakika nane ni moja na dakika saba ni moja. Wengine wote wamejitahidi dakika tano tano. Kwa hiyo, napenda kuwapongeza na tutaendelea na hilo kwa sababu hatuwezi kuwa tunafanya vitu kama hatupo Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge tuna matangazo, naanza na matangazo ya wageni. Wageni walioko Bungeni kwanza ni wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki Dk. Kamala. Hawa ni Mheshimiwa Dk. Amani Walid Kabourou, Mbunge wa zamani huyu sasa ni Mbunge wa Afrika Mashariki. Tumefurahi sana kukuona. Tuna Balozi Juma Mwapachu, Katibu Mkuu Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, tumefurahi pia kukuona karibu katika ukumbi huu. Tuna Dk. Mshokorwa Katibu Mkuu wa *Pan Africanism Movement* yuko wapi? Pia kuna Mrs Adelaida Kamala, mke wa Mheshimiwa Dk. Kamala karibu sana mama kwa kumuunga mkono Dk. afanye kazi yake vizuri.

Tuna Mrs Rose Kamala mama mzazi wa Mheshimiwa Dk. Kamala, wewe ndiyo unastahili kupata heshima zaidi na zaidi. Ahsante sana. Tunae mtoto wake Miss Catherine Kamala bado ka-*baby* na mtoto wake mwingine Miss Carine-Rose Kamala na tunae mdogo wake Mr. Frank Filbert, ahsanteni. Kwa hiyo familia nzima mmekuja kumuunga mkono.

Vile vile tunao wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mohamed Abood ambae ni watoto wake wawili yuko Ahmed Abood na Ali Abood wote wasimame. Kuna mwanafunzi wa *Feza Boy Sekondari School* Yuperious Tax, hili jina kwa kweli ni gumu sana, karibu sana nafikiri nae ni katika wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri.

Halafu tunao watumishi wa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki ambao ni Katibu Mkuu Dk. Stegomena Tax, kumbe yule Taxi mwingine ni mtoto wake Katibu Mkuu, ni juzi umehamia kule, tunakufahamu vizuri.

Tuna Naibu Katibu Mkuu, Mrs Uledi Mussa aaha Mr, wameandika, *ok* nimekosea, wameandika Mr Uledi, yupo? *Ok*, ahsante sana. Tuna Mkurugenzi wa Idara ya Sera na Mipango Miss Joyce Mwakisalya, karibu sana mama tunafurahi sana kukuona. Tuna Mkurugenzi wa Idara ya Siasa, Ulinzi na Usalama, Job Msima karibu sana. Tuna Kaimu Mkurugenzi wa Utawala na Utumishi, Mary Stella Mjura naona ana kazi nyingine. Tuna Kaimu Mhasibu Mkuu, Neema Limunge, ahsante sana, tuna Kaimu Mkuu Wa Kitengo cha Ugavi na Manunuzi, Fred Issa, nashukuru sana na wako wanao kaimu wengi katika Wizara hii. Kwa hiyo, shughuli lazima ifanyike kuwahalalisha. Pamoja na Maafisa waandamizi wa Wizara wengine, wote mnakaribishwa.

Pia kuna wageni wa Mheshimiwa Charles Mwera wa Jimbo la Musoma, ambao yupo George Marwa, yuko Denis Samo na Samuel Mwita, sasa hawa sijui watoto wake au nani lakini hawa kina Samo, Samo naona kama watoto wake, karibuni sana.

Wengine ni wageni wa Mheshimiwa Ephraim Madeje, Mbunge wa Dodoma Mjini, hawa ni Katibu wa CCM, Wilaya ya Dodoma Mjini, ndugu David Mzuri, ahsante sana. Yupo msaidizi wa Mbunge Dodoma Mjini, Rita Chibile, wapo Makatibu Kata 30 wa Mjini Dodoma, wapo wapi Makatibu Kata wote? *Oooh*, wapo hapo, karibuni sana, ahsanteni sana. Halafu yupo na Eva Jeremia, Katibu Muhtasi wa CCM Wilaya ya Dodoma Mjini, ninyi ni wenyeji wetu tunawakaribisha wakati wowote mnapopata nafasi.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Grace Kiwelu ambao ni Ndugu Lamek Daniel Mbungu, ni mwalimu kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma akiongozana na wanafunzi 40, mwalimu Mbungu yupo wapi na wanafunzi wote wa Chuo Kikuu cha Dodoma? *Ok*, karibuni na nyie ndiyo majirani zetu hapa. Kwa hiyo, mnakaribishwa wakati wowote mnapopata nafasi.

Vile vile tuna wageni wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, Mheshimiwa Sofia Simba ambao ni Asia Firdaus kutoka Dar es Salaam, ni

mwanamitindo akiambatana na kundi lake ambao ni wanamitindo. Wanamitindo hawa wako wapi? Wote wasimame wana mitindo hao. Sasa muano chini ya Deo Mwanambili, Kiongozi wa Karunde Band, yupo Sharon, Hidaya, Tasha na Presha. Karibuni sana wanamitindo sijui mmekuja na mitindo gani hapa leo.

Kuna wageni wa Mheshimiwa Idd Azzan, Mbunge wa Kinondoni, ni kundi la Jahazi Modern Taarab likiongozwa na kiongozi wao ambaye ni Mzee Yussuf, Mfalme akiwa na mwimbaji wao mpya Bi. Mwanahawa Ally. Tuanze kumwona Mzee Yussuf, Mfalme na Bi. Mwanahawa Ally. Nadhani hawa watakuwa kule *basement* kwa sababu humu nafasi haitoshi.

Pia kuna mgeni wa Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Mwenyekiti wa Bunge na Mbunge wa Kwamtipura, ambaye ni kaka yake aliyemlea na kumsomesha toka akiwa mdogo na ni Kanali Mstaafu ambaye ni Hussein Azam Nyange naona na yeye amekosa nafasi. karibuni sana.

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Mariam Mfaki ambao ni watoto wa shule ya msingi ya Kata ya Lamaiti, Wilaya ya Bahi ambao wamefanya vizuri katika mtihani wa muhula wa kwanza 2009. Watoto hawa ni wale walioshika nafasi ya kwanza na ya pili kwa darasa wa tatu hadi la saba.

Wapo wageni wa Mheshimiwa Martha Mlata ambao ni Nasma Sufiani Kalonga, Amina Habib Salehe na Mariam Salehe. Karibuni sana kwenye ukumbi wetu.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa na Mheshimiwa Mwananzila hawa wanatoka *FDME Bank Ltd Dar es Salaam.* Nao ni Mr. Albert Mkongwa, *Deputy Manager Credit*. Hawa wakina Mkongwa wanatoka kwetu, sasa sijui inakuwaje. Halafu tuna Miss Catherine Charles *Business Development and Trade Advisor*, Mr. Wang, General Manager wa Kampuni ya Matrekta ya Caltic. Sasa hawa watu wa Benki Waheshimiwa Wabunge mnaweza kwenda kujifunza habari zao.

Vile vile tuna wageni wa Mheshimiwa Dr. Zainab Gama na Wabunge wanamichezo ni waamuzi wa mpira wa miguu waliomaliza mitihani yao *cooper test* kituo cha Dodoma wakiongozwa na ndugu Riziki Majala, Mkufunzi wa Waamuzi wa *TFF*. Karibuni sana.

Pia Mheshimiwa Dr. Gama ana wageni wengine ambao ni wanafunzi wa shule ya Sekondari ya Wasichana Huruma hapa Dodoma ambao ni wanafunzi 33 wakiongozwa na Sister Auleria. Karibuni sana na tunategemea mtafanya vizuri katika shughuli zenu za masomo.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Prof. Mark Mwandosya ambao ni Bwana Bakari Luanda, Mwenyekiti wa *TUGHE*, Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Shinyanga Mjini, yupo Bi. Paulina Shangili, Katibu wa *TUGHE*, yupo Bwana Charles Mituha Mjumbe wa *TUGHE*. Karibuni sana na wamekuja kujifunza Dodoma jinsi wanavyofanya kazi zao.

Tuna viongozi 30 wa Asasi ya Dira ya Vijana Tanzania. Jana Wizara yenu ilikuwa inasomwa sijui mlikuwepo? Karibuni sana. Tuna Bwana Richard Kasesela wa *Pan African Business Coalition ya* Dar es Salaam, amekuja kwa ajili ya kutembelea Bunge. Tuna wanafunzi 40 na walimu wawili kutoka shule ya msingi Kizota. wako wapi wanafunzi wa Kizota, wale pale, karibuni sana. Kuna wageni wengine ambao hatukuwataja, Bunge liko wazi kwa wageni wote, kwa hiyo, mnakaribishwa sio lazima mtambulishwe.

Waheshimiwa Wabunge huo ndiyo mwisho wa matangazo ya wageni. Sasa naingia katika matangazo ya kazi. Mheshimiwa Mwenyekiti, wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Jenista Mhagama anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati kuwa kutakuwa na Kikao cha Kamati leo saa saba mchana katika ukumbi wa Pius Msekwa B.

Mheshimiwa Ali Ameir Mohammed, Katibu wa Wabunge wa CCM, anatangaza kwamba kile kikao cha uongozi mlichopewa barua zake kimeahirishwa mpaka mtakapoambiwa tena.

Mheshimiwa Idd Azzan, Mbunge wa Jimbo la Kinondoni anaomba niwatangazie Wabunge wote kuwa leo tarehe 17 kutakuwa na burudani ya taarab ya kikundi cha Jahazi Modern Taarab ikiongozwa na Mzee Yussuf (Mfalme) katika ukumbi wa *Royal Village Hotel* Area D, kuanzia saa mbili usiku. Kiingilio ni bei rahisi kabisa, *VIP* shilingi elfu kumi, mbona mnashituka nyie vipi? Viti vya kawaida shilingi elfu saba, hii ni kwa Waheshimiwa Wabunge, tiketi zinapatikana mapokezi yetu ya Bunge, jengo la utawala nadhani pale mapokezi. Kwa hiyo, mnakaribishwa saa mbili *Royal Hotel Area D*.

Waheshimiwa Wabunge huo ni mwisho wa matangazo, samahani kuna tangazo sikuliona, tangazo kwa Wabunge, kutakuwa na onyesho la vazi la kanga linaloletwa na mwanamitindo Asia Firdaus, toka Dar es Salaam, leo jioni. Tena leo hii hii tarehe 17 katika Ukumbi wa Kilimani saa moja jioni. Kiingilio wao ni hela kidogo zaidi shilingi kumi na tano elfu. Tiketi zinapatikana katika *canteen* ya Bunge karibu sehemu ile ile, kwa hiyo leo jamani mtajimwaga mtakavyojua na huu ndiyo mwisho wa matangazo. Waheshimiwa Wabunge kutokana na shughuli zingine za kuweza kukamilisha baadhi ya mambo kule ofisini, naomba Mwenyekiti wa Bunge, Mheshimiwa Maulid aweze kupokea kazi hii na ataendelea mpaka jioni.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea. Sasa naomba kumwita Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, kutokana na Taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lipokee, lijadili na kupitisha Mpango wa

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kukamilisha kwa mafanikio makubwa kipindi chake cha Uenyekiti katika Umoja wa Afrika. Katika kipindi hicho Mheshimiwa Rais ameweza kusimamia kikamilifu mtangamano wa Bara la Afrika ikiwa ni pamoja na kusimamia migogoro na kurejesha demokrasia na utawala wa sheria katika Visiwa vya Comoro kwa kumuondoa kiongozi muasi Kanali Mohamed Bakary.

Aidha, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa hatua yake ya kutoa wazo la kuanzishwa kwa Eneo Huru la Kibiashara (*Free Trade Area*), hatimaye Umoja wa Forodha wa Kanda za Ushirikiano za Soko la Pamoja la Mashariki na Kusini Mwa Afrika (*COMESA*), Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini Mwa Afrika (*SADC*) na Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC*) ambalo lilikubaliwa na Viongozi wenzake katika kikao cha Wakuu wa Nchi kilichofanyika Jijini Kampala, Uganda mwezi Agosti 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama chini ya Mwenyekiti, Mheshimiwa Willson Masilingi, Mbunge wa Muleba Kusini akisaidiwa na Makamu Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala kwa uchambuzi wao wa kina wa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2008/2009 na mapendekezo ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa 2009/2010. Wizara itauzingatia ushauri na mapendekezo yaliyotolewa ambayo yataiwezesha Wizara katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ushiriki wake wa dhati na hoja zenye tija ambazo zimekuwa zikiiwezesha Tanzania kushiriki kwa ufanisi katika shughuli za majadiliano mbalimbali katika jumuiya ya Afrika Mashariki. Nina imani kuwa udugu na mshikamano huu utaendelezwa na kufanya ushiriki wa nchi yetu katika mpambano wa Afrika Mashariki kuwa wa manufaa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru kwa dhati wapiga kura wa Jimbo langu la Nkenge kwa imani yao kwangu na kwa kuendelea kunipa ushirikiano mkubwa kama Mbunge wao katika kutekeleza majukumu yangu. Wananchi wa Nkenge wameendelea kunionyesha upendo mkubwa na hivyo kunipa nguvu katika kuwatumikia. Nawaahidi kupitia Bunge lako Tukufu kuwa nitaendelea kutekeleza jukumu langu la kuwawakilisha na kuwatumikia kwa uwezo wangu wote. Nawaomba na ni matumaini yangu makubwa kuwa ushirikiano huo utaendelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumshukuru sana mke wangu mpendwa Adelaida Kamala na familia yangu kwa ujumla kwa upendo wao, ushirikiano na mshikamano ambao umeniwezesha kufanya kazi yangu kwa furaha na ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu kipindi cha bajeti cha mwaka jana, tumeshuhudia matukio mbalimbali hapa Bungeni. Napenda kuchukua nafasi hii, kuungana na

Waheshimiwa Mawaziri walionitangulia kutoa hotuba hapa Bungeni, kuwapongeza Wabunge wapya ambao ni Mheshimiwa Mchungaji Luckson Ndaga Mwanjale, Mbunge wa Mbeya Vijijini; Mheshimiwa Lolesia Masele Bukwimba, Mbunge wa Busanda; Mheshimiwa Charles Mwera Nyanguru, Mbunge wa Tarime; na Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi. Nawatakia kila la kheri na mafaniko katika kutekeleza majukumu yao mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majonzi makubwa, naungana na wenzangu katika kuwaombea marehemu na kutoa salamu zangu za rambirambi kwa familia na wapiga kura wao kwa kuwapoteza Waheshimiwa Wabunge wafuatao: Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe, aliyekuwa Mbunge wa Tarime; Mheshimiwa Richard Said Nyaulawa, aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini; Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba, aliyekuwa Mbunge wa Busanda; na Mheshimiwa Fares Kabuye, aliyekuwa Mbunge wa Biharamulo Magharibi. Mwenyezi Mungu, awalaze mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maandalizi ya hotuba hii, Wizara ya Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki imezingatia maudhui yaliyotolewa katika Bunge lako Tukufu na Hotuba ya Mheshimiwa Mizengo Pinda, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, hotuba hii imezingatia Hotuba za Hali ya Uchumi na Bajeti ya Serikali zilizowasilishwa na Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Waziri wa Fedha na Uchumi. Nawapongeza kwa hotuba zao nzuri zilizoweka mwelekeo wa shughuli za Serikali na dira ya Bajeti ya Taifa katika mwaka wa 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii, kuwashukuru kwa dhati Waheshimiwa Mawaziri na Wadau kutoka Sekta na Taasisi mbalimbali za Kiserikali na kutoka Sekta Binafsi, kwa michango mikubwa wanayoitoa na ushiriki wao katika kuendeleza mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ushiriki wao umeweka nguvu na msukumo katika majadiliano na shughuli mbalimbali za kuendeleza mtangamano wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kwa maslahi ya Taifa na Jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niishukuru kwa njia ya pekee, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ushiriki wake wa dhati katika shughuli na majadiliano mbalimbali katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Nina imani kuwa, ushiriki na mshikamano huu utaendelezwa na kufanya ushiriki wa nchi yetu katika mtangamano wa Afrika Mashariki kuwa wa manufaa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Wilson Mutagaywa Masilingi, Mbunge wa Muleba Kusini, akisaidiwa na Makamu wake Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, Mbunge wa Ilala, kwa uchambuzi wao wa kina wa Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka 2008/2009 na Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka 2009/2010. Wizara itauzingatia ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati katika kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwashukuru viongozi wenzangu katika Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, nikianzia na Mheshimiwa Mohamed Aboud, Naibu Waziri wa Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki; Dkt. Stergomena L. Tax, Katibu Mkuu; Wakuu wa Idara na Vitengo; na Watumishi wote wa Wizara. Vilevile, napenda kumshukuru Katibu Mkuu Mstaafu, Bwana Bakari Mahiza, kwa kazi nzuri aliyofanya katika kipindi cha utumishi wake na hususan katika Wizara ya Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki. Pia napenda kumpongeza Bwana Uledi A. Mussa, aliyeteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchukua nafasi hii kumshukuru Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kuichapisha Hotuba hii kwa umakini na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaratibu masuala mbalimbali ya kisekta yanayogusa sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii, yanayohusiana na uendelezaji wa mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Majukumu haya ni mtambuka na yanagusa sekta mbalimbali. Kwa hiyo, utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika mwaka 2008/2009, umeendelea kuongozwa na sera na mikakati ya kisekta na kuzingatia ushirikishwaji wa wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuongozwa na sera za kisekta katika shughuli za mtangamano, Wizara imebaini kuwa kuna haja ya kuwa na Sera ya Mtangamano katika ushirikiano wa kikanda. Maandalizi ya awali ya Sera ya Mtangamano yameanza katika mwaka 2008/2009. Sera hii inatarajiwa kutoa dira na mwongozo katika kuendeleza mtangamano wa Afrika Mashariki. Vilevile, sera ya mtangamano itasaidia kubuni mikakati na mipango madhubuti ya kuimarisha ushiriki wa Tanzania katika jumuiya na kukabiliana na changamoto zilizopo na zinazojitokeza. Hatua hii italeta manufaa zaidi kwa taifa katika kutumia fursa zitokanazo na mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kanda nyingine za kiuchumi ambazo Tanzania ni mshiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa wito kwa wadau kuendelea kushirikiana na Wizara yangu ili kuhakikisha kuwa Tanzania inakuwa na Sera ya Mtangamano madhubuti, itakayoiwezesha Tanzania kutoa mchango mkubwa zaidi katika kuimarisha mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 inalenga kujenga uchumi imara na wenye uwezo wa kuhimili ushindani kwa kuhakikisha kuwa Taifa linakuwa na vianzio mbalimbali vya uzalishaji na uchumi ambao una maendeleo ya viwanda yaliyo karibu sawa na nchi zenye mapato ya kati. Katika kutekeleza, azma hii, Serikali kwa kushirikiana na Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, zimekubaliana kuandaa Mkakati wa Maendeleo ya Viwanda *(Industrial Development Strategy)*. Lengo la mkakati huu ni kukuza uwiano wa maendeleo ya viwanda, kuboresha ushindani katika sekta ya viwanda ili kuwezesha ukuaji wa biashara katika bidhaa za viwandani *(industrial goods)* na kukuza mauzo ya bidhaa nje ya Jumuiya ili kuleta mabadiliko na maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Maandalizi ya mkakati huu yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, nchi za Rwanda na Burundi zimeshirikishwa katika uongozi wa Jumuiya ikiwemo Sekretarieti. Hivi sasa, Naibu Katibu Mkuu anayesimamia Mipango na Miundombinu anatoka Rwanda na Naibu Katibu Mkuu anayesimamia Sekta za Uzalishaji na Jamii anatoka Burundi, ambazo zinatumia mfumo tofauti. Aidha, hatua zinachukuliwa ili kuwa na mfumo wa mwaka wa fedha unaofanana kati ya Nchi Wanachama Waanzilishi wa Jumuiya na nchi za Rwanda na Burundi. Kama mlivyoshuhudia, tayari nchi ya Rwanda imebadili mfumo wake kwa kusoma bajeti ya mwaka wa fedha 2009/10 sanjari na nchi za Tanzania, Kenya na Uganda. Burundi inaendelea na maandalizi ili kuweza kusoma bajeti yake sanjari na Nchi Wanachama wengine. Hatua hii itawezesha Nchi Wanachama kubuni mipango ya maendeleo na kutekeleza Programu na Miradi ya Kikanda kwa urahisi na ufanisi mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, mwaka huu Jumuiya inatimiza miaka kumi tangu kuanzishwa kwake hapo mwaka 1999. Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, inaendelea na maandalizi ya sherehe ya kutimiza miaka kumi ya Jumuiya. Katika maadhimisho haya, Jumuiya inalenga kuitangaza Jumuiya kwa Wananchi wa Afrika Mashariki kupitia vipindi maalum; kuainisha malengo makuu ya Jumuiya hadi mwaka 2020; michezo na sanaa; na maonesho ya utalii na uwekezaji. Maadhimisho haya yanatarajiwa kufanyika Mjini Arusha na kaulimbiu ikiwa ni Miaka Kumi ya Mafanikio Afrika Mashariki: Jamii Moja, Mwelekeo Mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa rai kupitia Bunge lako Tukufu, kuwaomba wadau na wananchi kwa ujumla kushiriki kikamilifu katika maadhimisho haya muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2008/2009, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, imeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ikiwa ni pamoja na kubuni sera; kuratibu maandalizi ya mikakati na programu za kisekta; kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Itifaki zake; kuratibu, kusimamia na kushiriki katika majadiliano kuhusu shughuli za mtangamano katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki; kuhimiza ushiriki na kukuza uelewa wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kuhusu fursa za kiuchumi na kibiashara zitokanazo na mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki; na kuimarisha utendaji kwa kujenga uwezo wa watumishi wa Wizara ili kuimarisha huduma bora kwa wateja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo na shughuli zilizopangwa kufanywa na Wizara katika mwaka 2008/09 ilikuwa ni:-

(a) Kuendelea kuratibu utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Forodha ikiwa ni pamoja na kusimamia mpango wa kuondoa ushuru wa forodha miongoni mwa Nchi Wanachama *(Internal Tariff Elimination)* na kusimamia uondoaji wa Vikwazo Visivyo vya Kiforodha *(Elimination of Non Tariff Barriers);*

(b) Kuratibu na kushiriki kikamilifu katika Majadiliano ya Itifaki ya Soko la Pamoja la Afrika Mashariki;

(c) Kuratibu utekelezaji wa miradi na programu za kisekta katika Jumuiya;

(d) Kuratibu ziara za mafunzo ya wajasiriamali, wafanyabiashara na wazalishaji wa Tanzania katika nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ili kujifunza, kubadilishana uzoefu na kubaini fursa na changamoto za kibiashara zilizopo;

(e) Kutoa elimu kwa wananchi katika Mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar kuhusu masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(f) Kufanya tathmini ya utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki kwa lengo la kubaini mafanikio na changamoto katika utekelezaji na kutoa mapendekezo ya hatua zinazostahili kuchukuliwa;

(g) Kutumia Balozi zetu nchini Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi katika kuendeleza biashara na uwekezaji;

(h) Kushirikiana na Wizara, Sekta Binafsi na wadau wengine katika kuandaa na kuhuisha Sera, Mikakati na Programu za nchi ili ziendane na za Jumuiya; na

(i) Kuimarisha uwezo wa Wizara kiutendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo ya bajeti ya Wizara kwa mwaka 2008/2009, yalizingatia utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005; Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini (MKUKUTA); Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Itifaki zake; Mkakati wa Tatu wa Maendeleo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (2006-2010); na Maamuzi mbalimbali ya Wakuu wa Nchi Wanachama na Baraza la Mawaziri wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na malengo mengine, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 inalenga kukuza uchumi imara na wenye uwezo wa ushindani katika masoko ya nchi jirani na ya dunia kwa ujumla. Kifungu cha 40(a) cha Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005, kinabainisha kuwa Serikali itaweka mikakati itakayowezesha kuhimili ushindani wa kibiashara kimataifa na kuwa na uwezo wa kushiriki na kufaidika na mfumo wa biashara wa kimataifa kwa kuzingatia mazingira ya utandawazi; na kifungu 40(b) kinabainisha kuwa, Serikali itachukua hatua ya kuendelea kuimarisha ushirikiano wa kikanda na wa Kimataifa kwa lengo la kupanua soko la bidhaa zetu na kuvutia wawekezaji. Aidha, katika Malengo ya Maendeleo ya Milenia, lengo namba moja linaainisha nia ya kuondoa umaskini uliokithiri na njaa. Pamoja na mambo mengine, malengo haya yatawezekana kwa kuendeleza mtangamano, kukuza biashara na kuwawezesha Watanzania kunufaika na fursa zitokanazo na mtangamano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, azma hii ya Serikali ya Awamu ya Nne imetekelezwa kwa mafanikio makubwa. Chini ya Umoja wa Forodha, Tanzania imeendelea kutekeleza mpango wa kuondoleana Ushuru wa Forodha *(Internal Tariff Elimination),* ambapo bidhaa zinazoingia katika soko la Kenya kutoka Tanzania na Uganda hazitozwi ushuru tangu mwaka 2005. Bidhaa za Kundi A *(category A),* ambazo ni pamoja na malighafi na madawa zinaingizwa nchini kutoka Kenya bila kutozwa ushuru. Aidha, bidhaa za Kundi B (*Category B*), ambazo ni bidhaa zilizosindikwa kwa kiwango cha kati (*semi-finished)* na zilizokamilika *(finished goods)* kutoka Kenya zinapoingia Tanzania na Uganda, zinatozwa ushuru ambao umekuwa ukipungua mwaka hadi mwaka na ifikapo mwaka 2010 utakuwa umefikia kiwango cha sifuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, nchi za Tanzania, Kenya na Uganda, zimeweza kutekeleza ratiba ya uondoaji ushuru wa forodha kama ilivyokubalika. Aidha, Nchi Wanachama zimefanikiwa kuwa na Sheria moja ya Ushuru wa Forodha na kuhuisha taratibu na nyaraka za kiforodha zinazotumika mipakani. Chini ya makubaliano ya kuziingiza nchi za Rwanda na Burundi katika Jumuiya, nchi hizo zimeanza kutekeleza Itifaki ya Umoja wa Forodha kuanzia tarehe 1 Julai, 2009. Kwa hatua hii, bidhaa zitakazoingia Rwanda na Burundi kutoka Tanzania hazitatozwa ushuru. Vilevile, bidhaa zitakazotoka Rwanda na Burundi kuingia Tanzania hazitatozwa ushuru. Natoa wito kwa Watanzania kutumia fursa hii kwa kuongeza biashara baina ya Tanzania na nchi hizi za Rwanda na Burundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kuanzishwa kwa Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, mauzo ya bidhaa za Tanzania katika soko la Afrika Mashariki yameendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka. Mauzo yaliongezeka kutoka Dola za Kimarekani milioni 142.0 mwaka 2005 hadi kufikia Dola za Kimarekani milioni 147.4 mwaka 2006, sawa na ongezeko la asilimia 3.8. Katika mwaka 2007 mauzo yaliongezeka kufikia Dola za Kimarekani milioni 169.5, sawa na ongezeko la asilimia 15.0. Ongezeko hili lilifikia Dola za Kimarekani milioni 272.2 mwaka 2008, sawa na ongezeko la asilimia 60.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bidhaa ambazo Tanzania inauza kwa wingi katika nchi za Afrika Mashariki ni pamoja na bidhaa za chumvi, umeme na vifaa vya umeme, mafuta ya kupikia, chuma, magunia, nafaka, sabuni, nyama, vifaa vya plastiki, kahawa iliyosindikwa, nondo na bidhaa nyinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa manunuzi ya bidhaa toka Nchi Wanachama wa Jumuiya, Tanzania ilinunua bidhaa zenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 176.0 mwaka 2005 na kufikia Dola za Kimarekani milioni 220.6 mwaka 2006; manunuzi yalishuka hadi kufikia Dola za Kimarekani milioni 109.9 mwaka 2007 na kuongezeka tena hadi Dola za Kimarekani milioni 201.9 mwaka 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bidhaa zilizoagizwa kwa wingi katika soko la Tanzania kutoka Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni pamoja na nondo, sukari, nafaka, mafuta ya kupikia, nguo, chupa za chai, vifaa vya umeme, madini, bidhaa za plastiki, chupa za chai na vioo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mauzo ya bidhaa za Tanzania katika Soko la Jumuiya, yanaendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka na hivyo kupunguza nakisi ya urari wa biashara kwa Tanzania. Nakisi katika urari wa biashara kati ya Tanzania na Nchi Wanachama ilikuwa Dola za Kimarekani 34.0 milioni mwaka 2005 na kuongezeka tena hadi Dola za Kimarekani 73.2 milioni. Kadiri utekelezaji wa Umoja wa Forodha ulivyoimarika, nakisi katika urari wa biashara inapungua na hivyo Tanzania kupata urari chanya wa mauzo katika soko la Jumuiya. Mwaka 2007 ilipata urari chanya kwa takriban Dola za Kimarekani 59.6 milioni na kuongezeka tena hadi Dola za Kimarekani 70.3 milioni mwaka 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** pamoja na jitihada nyingine za kuvutia wawekezaji zinazoendelezwa na Serikali, utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Forodha ulilenga pia kutoa fursa zitakazokuza uwekezaji baina ya Nchi Wanachama. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, juhudi hizo zimewezesha kukuza uwekezaji baina ya Nchi Wanachama. Miradi iliyowekezwa hapa Nchini kutoka Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 2005 ilikuwa 35 yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 39.65. Katika mwaka 2006 palikuwa na ongezeko la miradi mipya 38, yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 41.06. Ongezeko la miradi mipya katika mwaka 2007 lilikuwa miradi 27 yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 50.88. Mwaka 2008 uwekezaji uliongezeka kwa miradi mipya 77 yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 310.35.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta zilizoongoza katika uwekezaji kutoka Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki katika kipindi cha mwaka 2005 hadi 2008 ni pamoja na Sekta ya Uzalishaji, ambapo jumla ya miradi mipya 55 yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 261.94 iliwekezwa; Sekta ya Kilimo iliingiza miradi mipya saba yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 27.02; Sekta ya Utalii iliingiza miradi mipya 23 yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 19.39; Sekta ya Ujenzi iliingiza miradi mipya 29 yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 32.85; na Sekta ya Usafirishaji iliyoingiza miradi mipya 18 yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 20.32.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ongezeko la uwekezaji baina ya Nchi Wanachama, nafasi za ajira zitokanazo na uwekezaji huu zimekuwa zikiongezeka mwaka hadi mwaka. Katika mwaka 2005 ajira mpya zilikuwa 2,643, katika mwaka 2006 ajira mpya zilikuwa 5,379, ajira mpya katika mwaka 2007 zilikuwa 2,605 na katika mwaka 2008 ajira mpya zilikuwa 1,424. Sekta zilizoongoza katika kuongeza nafasi za ajira ni pamoja na uzalishaji, kilimo, utalii, ujenzi na usafirishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadhalika, wawekezaji wa Kitanzania wameweza kuwekeza katika Nchi Wanachama ili kunufaika na fursa zilizomo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika mwaka 2005, wawekezaji toka Tanzania waliweza kuwekeza miradi saba yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 12.3; katika mwaka 2006 miradi miwili mipya iliwekezwa, yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 2.2; na katika mwaka 2007 uwekezaji uliendelea kwa miradi mingine mipya miwili yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 4.0 na katika mwaka 2008 miradi iliongezeka hadi kufikia

miradi mipya mitano yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 6.21. Sekta zilizoongoza katika uwekezaji ni pamoja na utalii, usafiri na uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa wito kwa wazalishaji wa bidhaa na wafanyabiashara wa Tanzania, kuendelea kuzitumia fursa za kibiashara zinazopatikana katika Soko la Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, zitokanazo na juhudi za kuendeleza mtangamano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuondoa vikwazo visivyo ya kiforodha, katika kutekeleza Umoja wa Forodha Nchi Wanachama zilikubaliana kuondoa vikwazo visivyo vya kiforodha. Vikwazo vilivyobainishwa ni pamoja na urasimu katika usimamizi wa masuala ya forodha, taratibu ngumu za ukaguzi wa ubora na viwango vya bidhaa, vizuizi visivyo vya lazima barabarani, mlolongo wa vyombo vinavyosimamia masuala ya forodha yanayofanana na taratibu ngumu za usajili na upatikanaji wa leseni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, zimepiga hatua katika uondoaji wa vikwazo visivyo vya kiforodha kwa kuandaa na kutekeleza programu ya kuondoa vikwazo visivyo vya kiforodha. Kila nchi imeunda Kamati za Kitaifa za kushughulikia uondoaji wa vikwazo hivyo. Kamati ya Kitaifa ya Tanzania inaundwa na Wajumbe kutoka katika Wizara, Taasisi za Umma na Sekta Binafsi. Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ndiyo mratibu wa Kamati ya Kitaifa kwa upande wa Tanzania.
Kuwapo kwa chombo hiki, kumewawezesha wafanyabiashara na wasafirishaji mizigo nchini, kuwasilisha kero wanazokabiliana nazo katika kufanya shughuli zao za kibiashara. Kero zilizowasilishwa zimefuatiliwa, zimejadiliwa na kupatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio yaliyofikiwa na hatua zilizokwishachukuliwa katika uondoaji wa vikwazo vya kibiashara visivyo vya kiforodha, bado ni changamoto katika utekelezaji wa Umoja wa Forodha. Naziomba Nchi Wanachama na wadau wote, tujitahidi kuongeza kasi ya kuondoa vikwazo visivyo vya kiforodha na kuepuka kuanzisha vikwazo vipya. Napenda kuliahidi Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara yangu itaendelea kufuatilia na kushughulikia suala hili ili kuwawezesha wafanyabiashara wa Tanzania na nchi nyingine za Jumuiya kunufaika na fursa za kibiashara katika soko la Afrika Mashariki. Aidha, nachukua nafasi hii kwa mara nyingine, kuwahimiza wafanyabiashara kuitumia kikamilifu Kamati ya Kitaifa ya Kushughulikia Uondoaji wa Vikwazo Visivyo vya Kiforodha, inayosimamiwa na Wizara yangu kwa kuwasilisha taarifa pale wanapokumbana na vikwazo visivyo vya kiforodha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inalo jukumu la kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Forodha ili kupima kama wananchi wanazielewa, wanazitumia na wananufaika na fursa zilizopo katika soko la Afrika Mashariki. Katika kufanikisha azma hii, Wizara ilifanya ziara za kikazi kwa lengo la kutoa ushauri na elimu kuhusu fursa za kibiashara katika Soko la Afrika Mashariki na jinsi ya kuzingatia viwango vya ubora wa bidhaa ili kuongeza mauzo nje ya nchi. Inatarajiwa kuwa ushauri uliotolewa katika ziara hizo na uchambuzi wa changamoto zilizobainishwa utaimarisha shughuli za uzalishaji, kukuza biashara na kuongeza mauzo katika Soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa kufanya tathmini ili kuweza kupima matokeo kama yanakidhi matarajio ya Umoja wa Forodha na ili kuweza kubainisha kama kuna changamoto na kujipanga vyema, Kikao cha Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki kilichofanyika Mwezi Julai, 2008 Mjini Arusha, kiliiagiza Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, kufanya tathmini ya utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki. Taarifa ya awali ya tathmini hiyo imeonesha kuwa, Nchi Wanachama zimenufaika na Umoja wa Forodha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa inaonesha kuwa, manufaa yaliyopatikana kutokana na Umoja wa Forodha ni pamoja na kuongezeka kwa biashara, kuongezeka kwa mapato ya Serikali na kuongezeka kwa uwekezaji. Mapato ya Serikali yameongezeka kutokana na kuimarika kwa uchumi wa Nchi Wanachama, pamoja na usimamizi bora wa ukusanyaji mapato. Mapato ya Serikali ya Tanzania yameongezeka kwa wastani wa asilimia 35.9 katika kipindi cha mwaka 2005/2006 na 2007/2008 ikilinganishwa na asilimia 23.3 kwa mwaka 2003/2004 na 2004/2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kujipanga vyema kama nchi, Wizara ya Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki, inaendelea na mchakato wa kufanya tathmini ya utekelezaji wa Umoja wa Forodha katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ili kuelewa kwa kina mafanikio na changamoto zinazotukabili katika utekelezaji wa Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki. Tathmini hii inatarajiwa kukamilika ifikapo mwishoni mwa robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2009/2010. Matokeo ya tathmini hii pamoja na Tathmini iliyofanywa katika ngazi ya Jumuiya, yatawezesha Tanzania kujipanga ipasavyo, ikiwa ni pamoja na kukamilisha majadiliano na maandalizi ya Itifaki ya Soko la Pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imeendelea kushiriki katika majadiliano ya uundaji wa Soko la Pamoja la Afrika Mashariki. Majadiliano husika yalianza rasmi mwezi Aprili, 2008 na inatarajiwa kuwa yatakamilika ifikapo mwezi Novemba, 2009. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, katika maandalizi na majadiliano yanayoendelea ya kuanzisha Soko la Pamoja, maslahi ya Nchi zote Wanachama ikiwa ni pamoja na maslahi ya Tanzania yamezingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kikao cha Wakuu wa Nchi Wanachama kilichofanyika tarehe 29 Aprili, 2009 Mjini Arusha, Wakuu wa Nchi waliamua kuwa masuala ya ardhi na ukazi katika Itifaki ya Soko la Pamoja, yazingatie sheria za kila Nchi Mwanachama. Aidha, iliamuliwa kuwa, Pasi za Kusafiria zitumike kama nyaraka za kusafiria baina ya Nchi Wanachama na kwa Nchi Wanachama ambao watapenda na wako tayari kutumia vitambulisho vya uraia kama hati za kusafiria waendelee kwa makubaliano baina ya nchi na nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara itahakikisha kuwa, maamuzi ya Wakuu wa Nchi Wanachama yanazingatiwa ipasavyo katika majadiliano yanayoendelea katika kukamilisha maandalizi ya Itifaki ya Soko la Pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuwashukuru kwa dhati wadau wote ikiwa ni pamoja na Wizara na Taasisi mbalimbali toka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Taasisi za Elimu ya Juu na Utafiti, Taasisi na Asasi toka Sekta Binafsi na Asasi Zisizo za Kiserikali kwa ushirikiano wa hali ya juu na michango yao muhimu katika majadiliano ya maandalizi ya Itifaki ya Soko la Pamoja yanayoendelea. Ushirikiano huu na michango iliyotolewa, imeiwezesha Tanzania kuhakikisha kuwa maslahi ya Tanzania katika mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki yanazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa rai kwa wadau wote kupitia Bunge lako Tukufu kuendelea kutoa ushirikiano kwa Wizara yangu ili maandalizi ya Itifaki hii yaweze kukamilishwa kwa wakati na kwa ufanisi unaotarajiwa na Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua kuwa Soko la Pamoja litafungua fursa mbalimbali za kiuchumi na kijamii na kwa kuzingatia changamoto mbalimbali, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine inaendelea na maandalizi ya Mkakati wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Soko la Pamoja. Mkakati huo utalenga katika kuiwezesha Tanzania kujipanga vyema katika kutumia fursa za Soko la Pamoja na pia kukabiliana na changamoto zake kikamilifu. Utekelezaji wa Soko la Pamoja ni suala mtambuka linalohusisha sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Katika hali hii, haja ya kubuni mikakati ya utekelezaji wa Soko la Pamoja ni suala la pamoja linalohusisha Mikakati ya Kitaifa, lakini pia Mikakati ya Kisekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nchi Wanachama zimekubaliana kuendesha zoezi la kubainisha idadi na aina ya wataalamu waliopo katika Nchi Wanachama *(Manpower Survey).* Zoezi hili litaziwezesha Nchi Wanachama kutambua idadi ya wataalamu waliopo ndani ya nchi, ikilinganishwa na mahitaji halisi katika fani mbalimbali. Zoezi hili litaziwezesha Nchi Wanachama kujipanga ipasavyo ili kuweza kuajiri wataalamu kutoka nje ya nchi husika kwa utaratibu unaofaa. Vile vile, Nchi Wanachama zimekubaliana kuwianisha mifumo ya Elimu baina yao ili kuwa na mifumo ya elimu inayofanana na hivyo kuwepo uwiano katika kuwatambua wataalamu na taaluma zao katika Nchi zote Wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha kuwa uanzishwaji wa Sarafu Moja *(Monetary Union)* unafanyika ipasavyo, Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki, limeunda Kamati ya Masuala ya Fedha *(Monetary Affairs Sub-Committee)* na Kamati ya Sera za Kodi na Bajeti *(Fiscal Affairs Sub-Committee),* ambazo zimepewa jukumu la kuwianisha vigezo vya Kuimarisha Uchumi *(Macro-Economic Stability and Convergence),* ikiwa ni maandalizi ya uundwaji wa Sarafu Moja uliopangwa kutekelezwa mwaka 2012. Aidha, Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki imeelekezwa kuanzisha utafiti utakaobainisha ni jinsi gani lengo la kuwa na Sarafu Moja katika Jumuiya ya Afrika Mashariki litafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Viongozi Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya za Afrika Mashariki (EAC), Soko la Pamoja la Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika

(COMESA), na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), walikutana Jijini Kampala Uganda mwezi Agosti, 2008. Lengo kuu la mkutano huo lilikuwa kujadili uwezekano wa kuunda eneo huru la kibiashara, litakalohusisha kanda hizo tatu za maendeleo ya kiuchumi *(EAC* – SADC - *COMESA*, *Tripatite Trade Arrangement).* Katika kikao hicho, Viongozi wa Nchi katika kanda hizo walikubaliana kuanzisha Ukanda Huru wa Kibiashara kwa nia ya kuendeleza mtangamano zaidi *(deeper intergration),* ikiwa ni pamoja na kuunda Umoja wa Forodha wa EAC – SADC - COMESA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufanikisha azma hii, Sekretarieti za EAC, SADC na COMESA, ziliagizwa kufanya uchambuzi na kuandaa mpango wa utekelezaji utakaobainisha hatua za kuchukua *(road map*) katika kuanzisha Ukanda Huru wa Kibiashara *(Free Trade Area)* na hatimaye Umoja wa Forodha. Zoezi hili linaendelea na inatarajiwa kuwa taarifa kuhusu mchakato huu, itatolewa katika kikao cha pili cha Ushirikiano wa Utatu wa Kibiashara wa Kanda EAC- SADC- COMESA kilichopangwa kufanyika mwishoni mwa mwaka 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua nyingine inayoendelea katika kuendeleza biashara baina ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Kanda nyingine ni majadiliano kuhusiana na Mkataba wa Ubia wa Uchumi (*Economic Partnership Agreement - EPA),* baina ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Ulaya *(European Union – EU).* Mkataba huu unalenga kuendeleza mahusiano ya kibiashara baina ya Jumuiya hizo mbili kwa kupeana upendeleo wa kimasoko. Sehemu kubwa ya majadiliano ya Mkataba huu imekamilika. Kwa sasa, Jumuiya ya Afrika Mashariki inaendelea kujadiliana na Umoja wa Ulaya kuhusu maeneo ya Biashara ya Huduma, Kilimo, Ushirikiano wa Maendeleo ya Kiuchumi na kifungu cha Upendeleo Maalum kwa Nchi Zinazoendelea *(Most Favoured Nations Clause).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya ya Afrika Mashariki imeendelea na jitihada za kukuza mahusiano ya kibiashara baina ya Jumuiya na nchi nyingine duniani. Mwezi Julai, 2008, Jumuiya ya Afrika Mashariki ilitiliana saini ya makubaliano ya kibiashara na uwekezaji *(Trade and Investmentment Framework Agreement – TIFA)* na Marekani. Makubaliano hayo yanalenga kuimarisha ushirikiano wa kibiashara na uwekezaji baina ya Nchi Wanachama wa Jumuiya na Marekani. Makubaliano haya yataziwezesha Nchi Wanachama kunufaika na fursa mbalimbali za kibiashara na uwekezaji zipatikanazo Marekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kupitia katika Bunge lako Tukufu kwa Watanzania wote kwamba, sasa hivi Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, zinaendelea na maandalizi ya Mkutano wa Nane wa *African Growth and Opportunity Act (AGOA).* Mkutano huu unatazamiwa kufanyika Mjini Nairobi, Kenya kuanzia tarehe 4 hadi 6 Agosti, 2009. Natoa wito kwa Watanzania kutumia Mkutano huu unaotoa fursa za kukuza mahusiano ya kibiashara na uwekezaji baina na Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na Marekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 50(e) cha Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, kinabainisha kuwa Serikali itawawezesha wananchi kiuchumi ikiwa ni

pamoja na kukuza ujasiriamali. Ilani inaelekeza Serikali kubuni mipango ya kuwapa fursa wajasiriamali Watanzania wanaoinukia. Katika kutekeleza azma hii, Wizara yangu kwa kushirikiana na *Tanzania Private Sector Foundation*, mnamo Mwezi Agosti, 2008 iliandaa ziara ya wafanyabiashara wa Tanzania nchini Burundi, Kenya, Rwanda na Uganda. Madhumuni ya ziara hii yalikuwa ni kuwawezesha Wafanyabiashara wa Tanzania kubaini fursa za masoko na uwekezaji katika Nchi hizo, kubadilishana ujuzi na kupata uzoefu. Kutokana na ziara hiyo, wafanyabiashara mbalimbali walipata masoko ya bidhaa zao na ubia wa kibiashara katika Sekta za Ujenzi, Biashara, Utalii na Hoteli, Madini, Bidhaa za Vyakula vilivyosindikwa na bidhaa za nguo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuendeleza mafanikio yaliyotokana na ziara hiyo, Wafanyabiashara wa Tanzania chini ya uratibu wa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika ya Afrika Mashariki na *Tanzania Private Sector Foundation,* wameunda Umoja ujulikanao kama *Friends of the East African Community*. Umoja huu utawezesha wafanyabiashara kubadilishana taarifa kuhusu fursa mbalimbali za biashara na uwekezaji zilizopo Jumuiya ya Afrika Mashariki. Vilevile Umoja huu utatoa fursa kwa serikali kupokea maoni ya wafanyabiashara na kuweka mikakati sahihi ya kusaidia kuimarisha biashara miongoni mwa Nchi Wanachama wa Jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara yangu imeendelea kuratibu ushiriki wa Tanzania katika maonesho ya kila mwaka ya Wajasiriamali yajulikanayo kama Jua Kali/Nguvu Kazi. Maonesho haya huzishirikisha Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Maonesho ya Nguvu Kazi/Jua Kali ni fursa nzuri kwa Wajasiriamali wetu kukutana na kubadilishana mawazo na uzoefu juu ya kukuza na kuendeleza biashara zao, kujifunza na kuanzisha uhusiano wa kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008, Maonesho hayo yalifanyika mwezi Desemba, 2008 Mjini Kigali, Rwanda, ambapo jumla ya Wajasiriamali 850 walishiriki. Katika Maonesho hayo Wajasiriamali walipata fursa ya kuuza bidhaa zao, kupata soko la bidhaa zao kama nguo za batiki, vinyago, vyakula vilivyosindikwa, asali, bidhaa za ngozi, madawa yatokanayo na miti shamba, vifaa vya ujenzi na bidhaa zilizotengenezwa kwa vyuma kama majiko ya kuokea mikate na kadhalika. Wajasiriamali wa Tanzania waliibuka washindi wa kwanza kwa ujumla katika vigezo vya ubora wa bidhaa, ufungashaji na ubunifu. Mwaka huu maonesho haya yanatarajiwa kufanyika mwezi Novemba, 2009 Mkoani Arusha. Napenda kutoa wito kwa wajasiriamali wa Tanzania na wananchi kwa jumla, kujitokeza kwa wingi kushiriki katika maonesho hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 35 cha Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005, inaelekeza Serikali kuchukua hatua kuhakikisha kuwa Sekta ya Utalii inatoa mchango mkubwa katika uchumi wa nchi yetu na Nchi za Afrika Mashariki kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa Sekta ya Utalii na ili kuwezesha kukuza mchango wa Sekta hii katika Pato la Taifa na mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Tanzania ilishiriki kikamilifu katika maandalizi ya Rasimu ya Itifaki ya Wakala wa Uratibu wa Utalii na Wanyamapori *(Protocol on East African*

*Tourism and Wildlife Coordination Agency (EATWCA)).* Itifaki hii itawezesha kuundwa kwa Wakala wa kuratibu masuala ya Utalii na Wanyamapori katika Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005, katika kifungu cha 35(h), inaelekeza hatua ambazo Serikali inatakiwa kuchukua ili kuendeleza utalii kwa nguvu ambapo Serikali itachukua hatua za kuzitathmini hoteli na kuzipanga katika madaraja ya nyota zinayostahiki na kuhakikisha kuwa hoteli zinakuwa katika hali ya unadhifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza azma hii na kuhakikisha kuwa huduma bora zinapatikana kwa watalii waingiapo Afrika Mashariki ikiwemo Tanzania, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, inaratibu mpango wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa kuziweka hoteli katika makundi yenye viwango vinavyokubalika kimataifa *(EAC Standardization and Classification of Hotels).* Kwa upande wa Tanzania, zoezi hili limefanyika Mjini Arusha na linaendelea kufanyika katika Jiji la Dar es Salaam. Kwa kuwa zoezi hili litafanyika nchi nzima, napenda kutumia fursa hii kuwahimiza wenye hoteli kuanza kuziboresha shughuli zao ili wakati wa tathmini waweze kufikia vigezo vilivyowekwa. Wasipofanya hivyo, hawataweza kufaidi matunda ya utalii kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la kwanza la milenia linatilia mkazo kuondoa umaskini uliokithiri na kupambana na janga la njaa. Aidha, umuhimu wa usalama na uhakika wa chakula ni miongoni mwa vipaumbele katika mihimili ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na MKUKUTA. Katika kutekeleza malengo haya, Wizara yangu imeendelea kuratibu maandalizi ya rasimu ya Mpango Mkakati wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa kuhakikisha kuwa, kunakuwa na chakula cha kutosha *(EAC Action Plan for Food Security).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia maelekezo yaliyomo katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005, hususan katika kifungu cha 32(h), ambapo msisitizo umewekwa katika ubora wa mifugo na sio wingi, Serikali imeelekezwa kuchukua hatua za kuendeleza mikakati ya kukuza Sekta ya Mifugo kupitia ugani, tiba, kinga, usambazaji wa maji na uboreshaji wa malisho. Katika kutekeleza maelekezo hayo, Wizara yangu inaendelea kuratibu majadiliano na maandalizi ya Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Kusimamia Biashara na Viwango vya Ubora wa Mazao ya Wanyama na Mimea *(EAC Draft Protocol on Sanitary and Phyto Sanitary).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, inaelekeza uimarishaji wa miundombinu ili kuziwezesha sekta nyingine za uzalishaji. Aidha, kifungu cha 44(c) cha Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005, kinaelekeza kuendelea kuchukua hatua za kuimarisha barabara nchini zitakazounganisha nchi yetu na nchi jirani kwa barabara za lami na zinazopitika wakati wote. Aidha, kifungu cha 45(e) kinaeleza kuwa, Serikali itachukua hatua za kuvutia uwekezaji katika miundombinu ya usafiri na uchukuzi wa reli, barabara, maji na anga katika Kanda za Maendeleo ili kuimarisha biashara kati ya nchi yetu na nchi jirani na kuwafanya wawekezaji kuvutiwa na soko kubwa la bidhaa na huduma zitakazozalishwa. Uwekezaji katika kanda hizi utaiwezesha

Tanzania kutumia nafasi yake ya kijiografia na kuendeleza fursa ya kuzihudumia nchi jirani zisizo na bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu ni mhimili mkuu katika kuziwezesha Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kunufaika na fursa zitokanazo na mtangamano. Kijiografia, Tanzania ni nchi pekee inayopakana na nchi zote tano za Afrika Mashariki. Kufanikisha miradi ya miundombinu iliyoainishwa katika programu na mipango mbalimbali ya Afrika Mashariki, kutaifanya Tanzania kuwa kiungo na kitovu cha biashara katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa kulitambua hili, uendelezaji wa miundombinu umepewa umuhimu wa pekee katika uendelezaji wa mtangamano.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zinaendelea kutekeleza mpango wa uboreshaji na upanuzi wa mradi wa mtandao wa barabara za Afrika Mashariki *(The East African Road Network Project - EARNP).* Mtandao huu unajumuisha kanda *(corridor)* tano.

Kanda ya kwanza *(Corridor 1):* Mombasa – Malaba – Katuna – Kigali – Kanyaru – Haut – Bujumbura – Gatumba (Burundi/DRC border), ikijumuisha Marangu – Tarakea, Chalinze – Segera, Segera – Himo na Tanga – Sadani – Bagamoyo na Arusha – Himo – Holili.

Kanda ya pili *(Corridor 2):* Dar es Salaam – Isaka – Lusahunga – Mutukula – Masaka, Lusahunga – Nyakasanza – Rusumo – Kigali – Gisenyi.

Kanda ya tatu *(Corridor 3):* Biharamulo –Mwanza – Musoma – Sirari – Lodwar – Lokichogio.

Kanda ya Nne *(Corridor 4):* Tunduma –Sumbawanga – Kigoma – Manyovu (Mugina) – Rumonge – Bujumbura – Ruhwa (Bugarama) – Karongi – Gisenyi.

Kanda ya tano *(Corridor 5)*: Tunduma –Iringa – Dodoma – Arusha – Namanga – Moyale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtandao huu wa barabara umepanuliwa kuzijumuisha nchi za Rwanda na Burundi. Upanuzi huo umejumuisha barabara za Rwanda na Burundi katika kanda ya 1, 2 na ya 4, ambapo Tanzania imeongeza barabara zenye urefu wa Kilometa 150 ili kuzijumuisha Rwanda na Burundi katika mtandao wa barabara za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Barabara hizo ni Lusahunga – Nyakasanza – Rusumo (Km 91) na Nyakasanza (Ngara) – Kobero (Km 59).

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 28 Aprili, 2009 Viongozi Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, walizindua rasmi ujenzi wa Barabara ya Arusha –Namanga – Athi River, yenye jumla ya kilometa 240, ambapo kilometa 105 zipo upande wa Tanzania (Arusha – Namanga), na kilometa 135 zipo upande wa Kenya (Namanga – Athi River). Huu ni mradi wa kwanza wa barabara ambao umefanikiwa kupata ufadhili wa ujenzi kupitia ushirikiano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, kupitia

ufadhili wa *Japan Bank for International Cooperation (JBIC)* na Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Bunge lako Tukufu, napenda kutoa shukrani kwa *Japan Bank for International Cooperation (JBIC)* na Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa kukubali kufadhili mradi huu muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wengine, imeendelea kuratibu uboreshaji na uendelezaji wa Sekta ya Anga. Mwezi Februari, 2009, Bunge lako Tukufu liliridhia Itifaki ya Usafiri wa Anga ya Afrika Mashariki *(East African Protocol on Civil Aviation Safety and Security Oversight Agency – (CASSOA)).* Itifaki hiyo inatarajiwa kuboresha usalama, na kuendeleza sekta ya usafiri wa anga katika Nchi Wanachama wa Jumuiya. Hadi sasa CASSOA imefanikiwa kuboresha usalama wa anga kulingana na viwango vilivyowekwa na Shirika la Kimataifa la Usalama wa Anga (ICAO).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, Jumuiya ya Afrika Mashariki imekuwa kanda ya kwanza katika Afrika kuandaa na kutumia kanuni zilizowianishwa na Kanuni za Usalama wa Anga za Kimataifa *(East Africa Harmonized Safety and Security Aviation Regulations),* ambazo zinatambulika na Shirika la Kimataifa la Usalama wa Anga *(ICAO)*. Mafanikio haya, yametokana na juhudi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kupitia *CASSOA*. Hivi sasa taratibu hizi zinatumika katika Nchi za Tanzania, Kenya na Uganda, wakati nchi za Rwanda na Burundi zinakamilisha maandalizi ili zianze kutumia kanuni hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, CASSOA imeanzisha mpango wa mafunzo ya pamoja kwa marubani na waongoza ndege katika Nchi Wanachama ili kuendana na mabadiliko yanayotokea katika sekta ya usafiri wa anga duniani na hivyo kutoa leseni ya urubani ya Afrika Mashariki. Vile vile, Jumuiya kupitia CASSOA imefanya utafiti unaolenga kubainisha mfumo wa kuratibu na kusimamia masuala ya usalama wa anga kwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC Upper Flight Information Regional Project)*. Sanjari na hatua hizi, Jumuiya ya Afrika Mashariki kupitia CASSOA imeanzisha mfumo wa mawasiliano ya Anga (*Cheaper Navigation System)*, utakaotumia mfumo wa *Global Navigation Satellite System (GNSS)*. Mfumo huu utapunguza gharama za mawasiliano ya anga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zinaendelea kuandaa Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Mtandao wa Reli ya Afrika Mashariki *(The EAC Railway Development Master Plan)*. Katika mpango huu, Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kubadilisha mfumo wa reli wa Nchi Wanachama kutoka *meter gauge* na kuwa na *standard gauge*. Mfumo huu utaziwezesha Nchi Wanachama kupata mabehewa kwa urahisi zaidi na kuziunganisha Nchi Wanachama na mitandao mingine ya reli katika nchi zinazoizunguka Jumuiya ambazo tayari zinatumia mfumo huu. Aidha, mfumo huu utaongeza uwezo wa reli kubeba mizigo mizito na abiria wengi zaidi kwa gharama ndogo za uendeshaji na

matengenezo. Maandalizi ya mpango huu yanatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Julai, 2009, ambapo miradi husika itaanza kutafutiwa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika juhudi za kuendeleza Mtandao wa Reli ya Afrika Mashariki, mwezi Januari, 2009, Serikali za Tanzania, Rwanda na Burundi, zimekubaliana na kuingia mkataba wa kuendeleza Reli ya Isaka (Tanzania) – Kigali (Rwanda) na Keza (Tanzania) – Gitenga (Burundi) – Musongati (Burundi) na matawi yote yanayoiunganisha kanda ya kati ya mtandao wa reli na Bandari ya Dar es Salaam. Jitihada hizi zitaimarisha shughuli za biashara na uchumi kati ya Tanzania, Rwanda na Burundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo kuu ni kuweza kuunganisha Nchi Wanachama zisizokuwa na bandari *(landlocked countries)* na Nchi Wanachama zenye bandari *(maritine ports);* na kuziunganisha Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Nchi nyingine jirani kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 45(e) cha Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupambana na majanga mbalimbali yanayoweza kutokea katika Maziwa, Nchi Wanachama zimekubaliana kuanzisha Kituo cha kuratibu shughuli za uokoaji na kukabiliana na Majanga Katika Maziwa ya Ukanda wa Afrika Mashariki *(EAC Maritime Rescue Coordination Centre - MRCC).* Makao Makuu ya kituo hiki yatakuwa Jijini Mwanza. Mwezi Februari, 2009 Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki iliwasilisha maombi ya ufadhili wa shughuli za kituo hiki kwa serikali ya Ubelgiji nao wameonesha nia ya kufadhili kituo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendeleza juhudi za kukabiliana na majanga mbalimbali kwenye anga na katika bahari, Nchi Wanachama zinaendelea na mchakato wa kuandaa mfumo wa kutekeleza Mkataba wa Ushirikiano wa Uokoaji katika Nchi Wanachama *(Framework for Operationalization of the East African Search and Rescue Agreement).* Mkataba huu ulitiwa sahihi na Nchi Wanachama mwaka 2002.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 43 cha Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005, kinaainisha kuwa Serikali itachukua hatua zenye lengo la kuongeza nishati na hasa umeme unaozalishwa na kuongeza uhakika wa upatikanaji na usambazaji wake ili kuwafikia wananchi wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha kuwepo na umeme wa kutosha, wa uhakika na wa bei nafuu na hivyo kukuza uchumi wa nchi zetu, Jumuiya ya Afrika Mashariki imeandaa Mpango wa kuendeleza nishati katika Jumuiya *(East Africa Power Master Plan).* Katika mpango huu, miradi ya nishati chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki iko katika sekta ndogo za umeme, mafuta na nishati mbadala. Katika kufikia lengo hili, Serikali imeweza kubainisha mradi wa kuipatia umeme miji midogo ya mipakani, ambapo Mji wa Namanga (Tanzania), tayari umepata umeme kutoka Namanga (Kenya). Aidha, majadiliano ya kuupatia umeme Mji Mdogo wa Mutukula Tanzania kutoka Uganda yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikiano katika nyanja ya kijamii umejikita katika elimu, utamaduni, afya, michezo, sayansi na teknolojia. Katika kuimarisha ushirikiano katika maeneo haya, Nchi Wanachama zimesaini Itifaki za kuanzisha vyombo (Kamisheni), vitakavyosimamia masuala ya Elimu, Afya, Kiswahili, Sayansi na Teknolojia. Kamisheni hizo ni Kamisheni ya Sayansi na Teknolojia ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*East African Science and Technology Commision - EASTECO);* Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*East African Kiswahili Commision*); Kamisheni ya Utafiti wa Afya ya Jumuiya ya Afrika Mashariki *(East African Health Research Commision – EAHRC)*; na Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki *(Inter-University Council for East Africa).*

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** hadi sasa Tanzania ni nchi pekee iliyoomba kuwa mwenyeji wa Makao Makuu ya Kamisheni ya Kiswahili na kuwa yawe Zanzibar. Mwezi Januari, 2009, Kamati ya Ukaguzi ya Jumuiya ilitembelea maeneo yaliyopendekezwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), taarifa imekwisha wasilishwa katika Jumuiya na inasubiri maamuzi ya Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti aidha, Jumuiya ya Afrika Mashariki, inaendelea na mchakato wa kupata mwenyeji wa Makao Makuu ya Kamisheni ya Utafiti wa Afya ya Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Nchi Wanachama. Tanzania ni miongoni mwa Nchi Wanachama zilizoomba kuwa mwenyeji wa Makao Makuu ya Kamisheni hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nchi Wanachama zinatekeleza mradi wa kudhibiti UKIMWI katika Bonde la Ziwa Victoria. Mradi huu ni wa miaka mitatu na unafadhiliwa na AMREF kwa kiasi cha Dola za Kimarekani 6.4 Milioni. Mradi umezilenga jamii zilizo katika mazingira hatarishi ya kuambukizwa UKIMWI katika Bonde la Ziwa Victoria, ikiwa ni pamoja na jamii ya wavuvi, wakulima kwenye mashamba makubwa, wasafiri na wasafirishaji katika Ziwa na wanafunzi wa Vyuo Vikuu. Utafiti wa tabia ya jamii hizi umekamilika na zimeundwa Kamati mbalimbali na vikosi kazi vya kutoa elimu kuhusu masuala ya UKIMWI katika Kanda kuu za usafiri na usafirishaji *(East Africa Transport Corridors).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu mengine yaliyotekelezwa kwa kipindi cha mwaka 2008/09 katika Sekta za Elimu, Afya na Sayansi ni pamoja na kuanza kwa zoezi la kuhuisha mitaala ya elimu katika Jumuiya, kuendesha mashindano ya uandishi wa insha ambapo Vijana wa Kitanzania, Bikombo Juma Suleiman, kutoka Shule ya Sekondari Mchangamdogo, Pemba, alifanikiwa kushinda na kupata tuzo ya mshindi wa pili kwa mwaka 2008. Tuzo hiyo alikabidhiwa katika Mkutano Mkuu wa Viongozi Wakuu wa Nchi Wanachama uliofanyika mwezi Oktoba, 2008, Kampala, Uganda. Aidha, kijana mwingine, Daniel Andondile kutoka Shule ya Sekondari Masukila, Mkoani Mbeya, alifanikiwa kupata tuzo ya mshindi wa pili kwa mwaka 2009 na kukabidhiwa tuzo hiyo katika Mkutano wa Viongozi wa Wakuu wa Nchi Wanachama uliofanyika mwezi Aprili, 2009, Mjini Arusha, Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa vijana wetu hawa na kupitia Bunge lako Tukufu, naomba kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge, kuwahamasisha

wanafunzi wengi zaidi kutoka katika shule zilizoko katika majimbo yao kushiriki kwenye mashindano haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato wa kubainisha taasisi zenye sifa za kuwa vituo vilivyobobea vya Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC Centres of Excellence)*katika maeneo mbalimbali unaendelea. Tanzania imeshawasilisha jumla ya vituo 17 katika Sekretarieti ya Jumuiya ili vitambuliwe kama vituo vilivyobobea. Kamati ya Wataalamu inatarajiwa kufanya ukaguzi wa vituo hivyo kuanzia mwezi Julai, 2009 ili kutathmini kama vinakidhi vigezo vilivyowekwa. Vituo vilivyowasilishwa kwa upande wa Tanzania ni Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam *(Dar es Salaam Institute of Technology);* Chuo cha Bandari; Chuo cha Uhandisi na Teknolojia cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (CoET); Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA) kwa ajili ya Kiswahili; Taasisi ya Sanaa Bagamoyo; KCMC – Chuo Kikuu cha Tumaini Moshi; Chuo cha Wanyamapori - MWEKA; Chuo Kikuu cha Mzumbe; Chuo Kikuu cha Ardhi; Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi; Chuo Kikuu cha Sokoine; Chuo cha Diplomasia Kurasini na Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 112 cha Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005, kinaelekeza Serikali kuendeleza juhudi za kukabiliana na tatizo la uharibifu wa mazingira na kutoa elimu kwa wananchi ili kuongeza uelewa wao kuhusu hifadhi ya mazingira. Katika kutekeleza azma hii, Tanzania imekubaliana na Nchi nyingine Wanachama kutekeleza mradi wa pamoja wa utunzaji wa mazingira katika Bonde la Ziwa Victoria; *Lake Victoria Environment Management Project (LVEMP)* ili kukidhi haja ya matumizi endelevu ya rasilimali muhimu zinazopatikana katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya kwanza ya mradi huu *(Lake Victoria Environment Management Project LVEMPI 2005 - 2008)*, ilikamilika mwezi Juni, 2008. Katika awamu ya kwanza, mradi ulifanikiwa kuondoa magugu maji kwa asilimia 80 katika Ziwa Victoria, kufahamu hali ya ziwa (Ecosystem), hususan kujua kina cha Ziwa, aina na idadi ya samaki katika Ziwa. Utafiti huu umefanywa kwa kutumia meli ya RV Jumuiya. Mradi umewezesha pia uboreshaji wa makazi ya jamii inayolizunguka Ziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya pili ya mradi wa LVEMP wa utunzaji wa mazingira katika Ziwa Victoria *(Lake Victoria Environment Management Project II - LVEMP II 2008-2014)*, utagharimu jumla ya Dola za Kimarekani Milioni 114.8. Kati ya fedha hizo, Dola za Kimarekani Milioni 90 ni mkopo kutoka Benki ya Dunia, Dola za Kimarekani Milioni saba ni mkopo kutoka *Global Environmental Facility (GEF)*, Dola za Kimarekani Milioni 10 ni msaada kutoka Sweden kupitia shirika lake la misaada *SIDA*, na Dola za Kimarekani Milioni 7.8 ni michango toka Nchi Wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi unalenga kuanzisha mfumo wa ushirikiano baina ya Nchi Wanachama katika kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali hii ya Bonde la Ziwa Victoria *(Establishing a cooperative framework for the sustainable management of the shared resources of the Lake Victoria Basin)* na kuendelea kutilia mkazo hatua za

kuzuia uharibifu wa mazingira na kuboresha maisha ya jamii inayozunguka Bonde la Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mradi huu, Nchi Wanachama zitaimarisha mfumo wa usimamizi na matumizi ya Ziwa na kuweka taratibu za ukaguzi na udhibiti wa uchafuzi wa mazingira. Mradi huu utaimarisha pia usimamizi wa maliasili hai katika Ziwa Victoria kupitia sera, sheria na mwongozo wa utunzaji mazingira. Aidha, mradi huu utainua uchumi wa wakazi wa maeneo ya Ziwa kwa kutambua maliasili za uwekezaji zilizopo na zinazoweza kutumika bila ya kuharibu mazingira na utaongeza uelewa kwa umma kupitia programu za mafunzo na mawasiliano ya moja kwa moja kwa kuanzisha vituo vya habari na kwa kuwaelimisha waandishi wa habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika mwaka 2008/09, Nchi Wanachama zimeendelea na maandalizi ya kanuni na taratibu za utekelezaji wa Sheria ya Usafiri katika Ziwa Victoria ya mwaka 2007. Kanuni hizi zinatarajiwa kukamilika na sheria kuanza kutumika ifikapo mwishoni mwa mwaka 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** kifungu cha 107 cha Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005, kinaelekeza Serikali kuchukua hatua za kuendelea kuendesha Serikali kwa kufuata Katiba ya nchi, sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa kidemokrasia. Katika kutekeleza azma hii, Serikali imekubaliana na nchi wanachama kuandaa mfumo wa Utawala Bora wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau, imeendelea kuratibu na kusimamia maandalizi ya mfumo wa Utawala Bora wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mfumo huo unatarajiwa kuzingatia nguzo kuu tano za Utawala Bora ambazo ni kuheshimu Katiba; Utawala wa Sheria na haki za kisheria; Kulinda na Kudumisha Haki za Binadamu na kutoa fursa sawa kwa wote; Mfumo wa Kupambana na Rushwa na Kuheshimu Maadili na Mgawanyo wa Mamlaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 110(b) cha Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005, inaielekeza Serikali kuchukua hatua katika kupambana na rushwa kwa kujenga mazingira mazuri zaidi yatakayowapa wananchi uwezo, ari na ujasiri zaidi katika kupambana na rushwa, wizi na ubadhirifu wa mali ya umma. Katika kutekeleza azma hii, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi yetu ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, imeendelea na mchakato wa kuandaa Itifaki ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wengine, inaendelea kuratibu maandalizi ya Itifaki hii. Kwa sasa, Nchi Wanachama zinaendelea na mchakato wa kukusanya maoni toka kwa wadau ili kuweza kuanza majadiliano. Nchini Tanzania kikao cha kukusanya maoni ya wadau kilifanyika Dar es Salaam tarehe 12 Juni, 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha kuwa haki za binadamu zinalindwa na kuheshimiwa, Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, zinaendelea

kutekeleza Mpango Kazi wa Kuendeleza na Kulinda Haki za Binadamu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki *(*EAC *Action Plan on Promotion and Protection of Human Rights).* Aidha, mchakato wa kuhuisha sera na mipango mikakati ya Nchi Wanachama inaendelea. Hatua hii inazingatia maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi katika kifungu CHA 99(d) kinachoelekeza Serikali kuchukua hatua ili kulinda na kudumisha haki za binadamu, kwa kusimamia utekelezaji wa haki za binadamu kama zilivyoelezwa katika Katiba ya Zanzibar na ile ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tamko la haki za Binadamu la Umoja wa Afrika na la Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuratibu na kusimamia Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Nchi Wanachama zinaendelea kukamilisha majadiliano ya rasimu ya Itifaki ya Uratibu wa Sera za Nje *(EAC Protocol on Foreign Policy Coordination).* Kukamilika kwa Itifaki hii kutaziwezesha Nchi Wanachama kuimarisha mahusiano ya kiuchumi na nchi nyingine duniani, kwa kuwezesha Balozi za Nchi Wanachama kutoa huduma za kibalozi pale ambapo Nchi nyingine Mwanachama haina huduma hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwezesha Nchi Wanachama kupata nafasi za uwakilishi katika Taasisi na Mashirika ya Kimataifa na pia wananchi kutoka Nchi za Afrika Mashariki kupata ajira katika Taasisi na Mashirika ya Jumuiya za Kimataifa, Nchi Wanachama zimekubaliana kushirikiana kuwaunga mkono wananchi kutoka Nchi Wanachama wanaowania nafasi za ajira katika Mashirika na Taasisi za Kimataifa. Makubaliano hayo yamewezesha Nchi Wanachama kupata nafasi za uwakilishi kama ifuatavyo: Uganda imepata nafasi katika Bodi ya Uendeshaji ya Mamlaka ya Anga ya Kimataifa *(International Civil Aviation Organization)* na Kiti cha Kudumu cha Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa; Kenya imepata nafasi katika Bodi ya Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki *(International Atomic Energy Agency)* na pia katika *Centre for Agricultural and Rural Cooperation*; wakati Tanzania imepata nafasi katika Bodi ya *International Hydrological Programme*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia utaratibu huu, jumla ya wananchi 13 kutoka Nchi Wanachama wamefanikiwa kupata nafasi za ajira katika Taasisi na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa kwa kipindi cha kuanzia mwezi Agosti, 2007 hadi kufikia mwezi Juni, 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii, kutoa rai kupitia Bunge lako Tukufu kwa Watanzania wanaoomba kazi kwenye Taasisi na Mashirika ya Kimataifa, kuwasilisha majina yao kwenye Wizara yangu ili tuweze kuyafikisha kwenye vikao husika ili waweze kuungwa mkono na Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika kifungu cha 125 unahimiza ushirikiano wa karibu katika masuala ya ulinzi na usalama. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Nchi Wanachama zimekamilisha maandalizi ya kuanza majadiliano ya Itifaki ya Ushirikiano katika Sekta ya Ulinzi. Itifaki hii itakapokamilika, itachukua nafasi ya Hati ya Makubaliano Maalum

ya Ushirikiano inayotumika kwa sasa na hivyo kuimarisha zaidi ushirikiano katika masuala ya ulinzi na usalama. Aidha, Nchi Wanachama zimeidhinisha Sera ya Utafiti na Maendeleo katika Sekta ya Ulinzi, ambayo inatoa mwongozo katika utekelezaji wa ushirikiano katika nyanja za utafiti na maendeleo ya sayansi na kiteknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza kifungu cha 111(d) cha Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005, kinachohimiza kuongeza uwezo wa Taifa wa kupambana na ujambazi na kuzagaa kwa silaha ndogo ndogo, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wadau wengine, inaendelea kuratibu utekelezaji wa Mradi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa kupambana na kuzagaa kwa silaha ndogo ndogo na za kati. Mradi unashughulika na kukusanya na kuharibu silaha ndogo ndogo na nyepesi; kuhuisha sheria za umiliki wa silaha ndogo ndogo na nyepesi miongoni mwa Nchi Wanachama; kuzijengea uwezo kiutendaji ofisi za madawati simamizi *(National Focal Points)* na kuelimisha wananchi juu ya madhara ya silaha ndogo ndogo. Serikali ya Ujerumani kupitia Shirika la Misaada la Ujerumani (GTZ), limetoa msaada wa fedha kiasi cha Euro Milioni 4.55 ambazo zitatumika kugharamia mradi huu kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwezi Julai, 2009. Nachukua nafasi hii, kuishukuru Serikali ya Ujerumani kwa msaada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 katika vifungu 113 na 114, imeielekeza Serikali kuchukua hatua za kujenga uwezo wa kudhibiti na kukabiliana na majanga makubwa kama tsunami, tetemeko la ardhi, tufani, mvua za kimbunga, mafuriko na ukame mkubwa. Nchi Wanachama wa Jumuiya, kwa kutambua gharama na hasara kubwa zitokanazo na majanga mbalimbali, zimekubaliana kuanzisha Mfumo wa Tahadhari wa Kukabiliana na Maafa *(Early Warning Mechanism)*. Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wengine, inaendelea kuratibu na kusimamia majadiliano ya kuanzisha Mfumo huo na majadiliano yanatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Agosti, 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki**,** Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, zimeiainisha Miradi itakayotafutiwa fedha kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki. Miradi hiyo imekwishawasilishwa na kukubalika katika ngazi ya Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Miradi hiyo ni Mradi wa Kuendeleza Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Zanzibar; Mradi wa Umeme wa Upepo; Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Maruhubi; na Miradi Minne ya Kilimo inayohusu utafiti wa kilimo cha Baharini; Magonjwa ya Wanyama; Teknolojia za Kuongeza Ubora wa Mazao; na Uimarishaji wa Karantini za Mazao na Mifugo. Mradi mwingine ni wa Uanzishwaji wa huduma za *Roll on Roll Off Services (RORO)* kati ya bandari za Zanzibar, Dar es salaam na Mombasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia mpango wa ufadhili wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Ulaya *(EU)*, imeonesha nia ya kufadhili mradi wa ukarabati wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Zanzibar na mazungumzo yanaendelea. Aidha, Mradi wa Uwanja wa Ndege wa Karume uliopo Pemba ni moja kati ya miradi iliyopewa kipaumbele nchini, ambayo imeombewa ufadhili kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB), chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mwezi Januari, 2009 Wizara ya Fedha na

Uchumi iliwasilisha orodha ya miradi hiyo ya kipaumbele kwenye Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB), ikiomba ufadhili kupitia Programu ya *African Development Fund 11 (ADF11)* kwa mwaka 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Ibara ya 49 ya Mkataba wa Uanzishaji wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, Bunge la Afrika Mashariki ni chombo cha Jumuiya ambacho majukumu yake makuu ni pamoja na kutunga sheria za Jumuiya; na kujadili na kupitisha Bajeti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika kutekeleza jukumu la kutunga Sheria za Jumuiya, Bunge la Afrika Mashariki katika mwaka 2008/2009, lilijadili na kupitisha Miswada minane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Bunge la Afrika Mashariki lilijadili na kupitisha Maazimio yafuatayo: Uundwaji wa Sera na Sheria ya Nishati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki; Msimamo wa Pamoja wa kuitaka Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu wa Mauaji ya Rwanda (ICTR) kumaliza kesi zake; Kumaliza mgogoro katika Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo kwa njia ya amani; Kuzitaka Nchi Wanachama kuridhia Azimio la Haki za Watu Wenye Mahitaji Maalum; Uundwaji wa Sera ya Kulinda Mazingira na Maliasili ya Jumuiya ya Afrika Mashariki; Pongezi kwa Rais Barrack Obama kwa kushinda Kiti cha Urais wa Marekani; na Azimio la kuzitaka Nchi za Kenya na Uganda kumaliza mgogoro wa umiliki wa Kisiwa cha Migingo kwa njia za amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii, kupitia Bunge lako Tukufu, kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya katika kutekeleza majukumu yao, inayochangia kuendeleza na kuimarisha mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Ibara ya 23 ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, inaeleza kuwa Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ni chombo chenye mamlaka ya kuhakikisha kuwa Mkataba wa Jumuiya unazingatiwa kwa ukamilifu na kutoa tafsiri sahihi juu ya utekelezaji wa Mkataba huo pale inapohitajika. Mahakama hiyo imegawanyika katika vitengo viwili; Kitengo cha Awali *(First Instance Division);* na Kitengo cha Rufaa *(Appellate Division)*. Kila Kitengo cha Mahakama kina Majaji watano ambapo kila Nchi Mwanachama ina Jaji mmoja katika kila kitengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Ibara ya 27 ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mahakama ya Afrika Mashariki ina mamlaka ya kutoa ushauri *(Advisory Opinion)*, kwa Jumuiya juu ya tafsiri na matumizi sahihi ya Mkataba wa Jumuiya ya Arika Mashariki; kutatua migogoro ya kikazi baina ya Jumuiya na waajiriwa wake; kusuluhisha migogoro inayotokana na kipengele cha usuluhishi *(Arbitration Clause)*, kinachoipa mamlaka Mahakama kusuluhisha migogoro kwenye Mikataba inayohusisha Jumuiya au Taasisi zake; na pia kusuluhisha migogoro inayotokana na kipengele cha usuluhishi *(Arbitration Clause)*, kwenye Mikataba ya kibiashara. Mpaka sasa Mahakama ya Afrika Mashariki, imeweza kutoa maamuzi katika kesi tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkutano wa Viongozi Wakuu wa Nchi Wanachama (*Summit)*, uliofanyika Kampala, Uganda tarehe 24 Octoba, 2008, ulimteua na kumwapisha Mheshimiwa Jaji Benjamin Patrick Kubo kutoka Kenya kuwa Jaji wa Mahakama ya Afrika Mashariki katika kitengo cha awali. Jaji Kubo amechukua nafasi ya Mheshimiwa Jaji Kasanga Mulwa kutoka Kenya, ambaye alistaafu rasmi tarehe 29 Novemba, 2008. Aidha, Mkutano huo ulifanya uteuzi wa Viongozi wa Mahakama ya Afrika Mashariki kama ifuatavyo: Mheshimiwa Jaji Harold R. Nsekela (Tanzania) aliteuliwa kuwa Rais wa Mahakama ya Afrika Mashariki; Mheshimiwa Jaji Philip K. Tunoi (Kenya) aliteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Mahakama hiyo; Mheshimiwa Jaji Johnson Busingye (Rwanda) aliteuliwa kuwa Jaji Kiongozi wa Mahakama ya Afrika Mashariki, na Mheshimiwa Jaji Mary Stella Arach-Amoko (Uganda) aliteuliwa kuwa Naibu Jaji Kiongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkutano wa Viongozi Wakuu wa Jumuiya (*Summit)* uliofanyika Arusha, Tanzania tarehe 29 Aprili, 2009, Mheshimiwa Jaji James Ogoola kutoka Jamhuri ya Uganda, aliteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Afrika Mashariki katika kitengo cha Rufaa, kuchukua nafasi ya Mheshimiwa Jaji Joseph Mulenga (Uganda), ambaye alistaafu rasmi tarehe 22 Oktoba, 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uteuzi uliofanywa na Wakuu wa Nchi, Majaji waliopo kwenye Kitengo cha Awali cha Mahakama ya Afrika Mashariki ni Mheshimiwa Jaji Johnson Busingye (Rwanda), Jaji Kiongozi; Mheshimiwa Jaji Mary Stella Arach-Amoko (Uganda); Naibu Jaji Kiongozi; Mheshimiwa Jaji John Mkwawa (Tanzania); Mheshimiwa Jaji Jean Bosco Butasi (Burundi); na Mheshimiwa Jaji Patrick Benjamin Kubo (Kenya). Aidha, Majaji waliopo kwenye Kitengo cha Rufaa ni Mheshimiwa Jaji Harold R. Nsekela (Tanzania), Rais wa Mahakama; Mheshimiwa Jaji Philip K. Tunoi (Kenya), Makamu wa Rais; Mheshimiwa Jaji Laurent Nzosaba (Burundi); Mheshimiwa Jaji Emilie R. Kayitesi Rusera (Rwanda); na Mheshimiwa Jaji James Ogoola (Uganda).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kama ilivyoainishwa katika Ibara ya 136(1), Makao Makuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yatakuwa Arusha, Tanzania. Mchakato wa ujenzi umekwishaanza, ambapo uratibu na usanifu wa mradi umekamilika. Aidha, uchambuzi wa zabuni, majadiliano ya mkataba, kupitisha kandarasi na kumpata mkandarasi, vinatarajiwa kukamilika ifikapo mwishoni mwa mwezi Julai, 2009. Kulingana na ratiba, baada ya Mkandarasi kuteuliwa, atapewa muda wa wiki nne za kufanya maandalizi (kupeleka mitambo eneo la kazi na kuajiri wafanyakazi). Ujenzi halisi unatarajiwa kuanza mwezi Septemba, 2009. Mradi unategemea kuchukua miezi 24 baada ya kuanza hadi kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali ya Ujerumani imetoa jumla ya Euro milioni kumi na nne kwa ajili ya kugharamia ujenzi huo. Naomba kupitia Bunge lako Tukufu, nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali ya Ujerumani kwa kukubali kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi huu wa Makao Makuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki huko Arusha, Tanzania. Kwa kuwa tayari

tumepata fedha hizi, tutahakikisha ujenzi unaanza haraka itakavyowezekana ili gharama za ujenzi zisije zikaongezeka, tukarejea tena kwa Wajerumani kuomba fedha nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09, Wizara imeendelea na jukumu lake la kuwaendeleza na kuwahudumia wafanyakazi wake kijamii na kitaaluma na kuboresha mazingira ya utendaji kazi ili kuongeza tija na ufanisi kama inavyoelekezwa na kifungu cha 124 cha Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005. Kifungu hicho kinaitaka Serikali kuendelea kuwa karibu na wafanyakazi na kuhakikisha kuwa, zinayashughulikia kwa ukamilifu na kwa wakati kero zao. Katika kutekeleza kifungu hicho, Wizara iimeweza kutoa mafunzo, kuwapatia watumishi stahili zinazoendana na ajira, kudumisha utawala bora, kushirikisha wafanyakazi katika maamuzi mbalimbali kupitia Baraza la Wafanyakazi, vikao vya menejimenti na vikao vya TUGHE. Msisitizo maalumu uliwekwa katika utendaji wenye tija na matokeo, kusimamia utawala bora, kudhibiti nidhamu, kutoa huduma bora kwa wateja na kuongeza kasi ya mapambano dhidi ya maambukizi ya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/2009, Wizara imepandisha vyeo watumishi wawili wa kada za utawala na manunuzi, kuwathibitisha kazini watumishi 13 na kuwaajiri katika masharti ya kudumu na malipo ya uzeeni watumishi 10 na watumishi 8 waliajiriwa katika masharti ya kawaida. Wizara iliajiri Wachumi sita, Mhandisi mmoja, Afisa Tawala mmoja, Mhasibu mmoja, Afisa Ugavi mmoja, Madereva wanne na Wahudumu wanne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha uwezo wa watumishi kiutendaji, watumishi 28 walipelekwa katika mafunzo ya muda mrefu na mfupi, ambapo kati yao, watumishi 6 wanaendelea kupata mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi katika fani za Sheria (mtumishi 1), Uchumi na Menejimenti (mtumishi 1), Uhasibu (mtumishi 1), Kutunza Kumbukumbu (watumishi 2), Uhazili (mtumishi 1). Watumishi 22 walipata mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi katika taaluma za Udereva, Uhazili, Uchambuzi, Majadiliano, Takwimu, Fedha na Utunzaji wa Kumbukumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha kuwa, majukumu ya Wizara yanaendana na malengo na muundo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na hivyo kuiwezesha Tanzania kunufaika na mtangamano wa Afrika ya Mashariki, muundo wa Wizara umehuishwa, ambapo Wizara itakuwa na Idara tano badala ya Idara nne kama ilivyokuwa hapo mwanzo. Katika zoezi hili, Kitengo cha Siasa, Ulinzi na Usalama, kimepandishwa hadhi na kuwa Idara kamili. Vilevile Idara za Uwekezaji na Sekta za Uzalishaji, Idara ya Miundombinu ya Kiuchumi na Sekta za Kijamii na Idara ya Siasa, Ulinzi na Usalama, zimepatiwa sehemu za Wakurugenzi Wasaidizi wawili wawili kila Idara. Nafasi hizo zitajazwa mwaka wa fedha 2009/2010 na tayari Wizara imempata Mkurugenzi wa Idara ya Siasa, Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu itaendelea na zoezi la kuwapandisha vyeo watumishi watano na kuwapatia mafunzo mbalimbali watumishi arobaini ndani na nje ya nchi. Lengo ni kuwaongezea ujuzi na ufanisi katika

kazi zao. Aidha, Wizara inatarajia kuwathibitisha kazini watumishi tisa na kuajiri watumishi wapya thelathini na sita wa kada mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi la Mfumo wa Wazi wa Mapitio ya Tathmini ya Utendaji Kazi (MWAMTUKA) au *OPRAS* ni agizo muhimu linalogusa utendaji katika Utumishi wa Umma. Katika mwaka 2008/09, Wizara imefanya maandalizi ya kutumia utaratibu wa kupima utendaji wa kazi kwa Mfumo wa MWAMTUKA. Wizara imetoa mafunzo kwa watumishi kuhusu namna ya kupanga malengo yanayopimika kwa kuwianisha malengo hayo na Mpango Mkakati wa Wizara. Mafunzo hayo yamefanyika katika miezi ya Novemba, 2008 na Januari, 2009. Inatarajiwa kuwa mfumo huu utaanza kutumika katika mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Chama cha Mapinduzi katika kifungu cha 66(f), inaielekeza Serikali kuchukua hatua za kuimarisha vita dhidi ya UKIMWI, ikiwa ni pamoja na kutumia vizuri misaada ya wahisani na kuelimisha wananchi dhidi ya unyanyapaa na kuongeza jitihada za kufikisha elimu kuhusu Ugonjwa wa UKIMWI kwa wananchi. Katika kutekeleza hili na kwa kutambua umuhimu wa kutekeleza mkakati wa kudhibiti UKIMWI mahala pa kazi, ikiwa ni pamoja na kuunga mkono juhudi za Mheshimiwa Rais za kuimarisha vita dhidi ya UKIMWI, Wizara imefanya tathmini ya hali ya UKIMWI katika Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha uelewa kuhusu janga hilo la kitaifa, Wizara yangu imeendelea kutoa mafunzo, ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo kwa watumishi wote jinsi ya kujilinda na maambukizi ya UKIMWI. Kupitia semina hizo, watumishi wamehamasika kupima afya zao kwa hiari. Katika mwaka 2008/2009, watumishi 43 wamepima na kuweza kuzitambua hali zao. Zoezi hili ni endelevu na litaendelea katika mwaka 2009/2010. Wizara inatarajia kuendesha mafunzo zaidi katika mwaka wa fedha 2009/2010, kwa waelimisha rika na kutoa ushauri nasaha kwa wale watakaodhihirika kuwa na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Chama cha Mapinduzi kifungu cha 107(b), inaelekeza Serikali kuendelea kutoa mafunzo juu ya Utawala Bora kwa Watendaji katika ngazi zote na kuhakikisha kwamba, matokeo ya mafunzo hayo yanaiweka Serikali kwenye utendaji ulio wazi. Kwa kutambua umuhimu wa kuboresha maadili sehemu ya kazi kama moja ya misingi ya Utawala Bora, Wizara yangu imeunda Kamati ya Maadili ili kusimamia mwenendo wa maadili ya Watumishi wa Umma na kudumisha Utawala Bora.

Wajumbe wa Kamati hiyo wamepatiwa mafunzo ya maadili na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) tarehe 4 Juni, 2009. Mafunzo haya yatatolewa kwa watumishi wote katika mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha 110(d) cha Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005, kinaelekeza Serikali kuzidi kuziba mianya ya rushwa katika utendaji wake. Katika kutekeleza hili, Wizara yangu imeendelea kuzingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma Namba 21 ya mwaka 2004. Aidha, utendaji wa

Wizara umezingatia na kuongozwa na Sheria na Kanuni za Fedha za Umma Namba 6 ya mwaka 2001 kama ilivyorekebishwa mwaka 2004. Wizara imeendelea kusimamia nidhamu katika matumizi ya fedha za Umma, kwa kuhakikisha kuwa ukaguzi wa mahesabu unafanywa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati za Usimamizi na Udhibiti wa Mapato na Matumizi ya Serikali zilizoundwa kufuatia agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu, zinakutana chini ya Uenyekiti wangu kila robo mwaka na taarifa zinawasilishwa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kama ilivyoelekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu iliendelea kutekeleza masuala ya Jinsia kwa kuanzisha Dawati la Jinsia na kuteua *focal person*. Aidha, Wizara ilitoa mafunzo kwa watumishi ili kujenga uelewa wa pamoja kuhusu uingizwaji wa masuala ya Jinsia katika Mipango na Mikakati ya Wizara. Lengo likiwa ni kutekeleza maagizo ya Serikali ya kuingiza masuala ya jinsia katika mipango na majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kuelimisha umma na jamii kwa ujumla kuhusu shughuli za Wizara yangu na maendeleo katika mtangamano kwa ujumla, Wizara imeendelea kukiimarisha Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano, kwa kununua vitendea kazi. Kitengo hiki kimekuwa ni kiungo muhimu kati ya Wizara na wadau mbalimbali na jamii kwa ujumla, kwa kutoa habari na elimu kwa njia ya mikutano, warsha, semina, makala, tovuti na maonesho mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa lengo la kujenga uelewa na kuimarisha ushiriki wa Watanzania katika masuala ya Jumuiya, Wizara iliendelea kuelimisha wananchi kuhusu masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kupitia Programu Maalum ya Wizara ya kutoa elimu kwa wananchi kuhusu fursa mbalimbali zilizopo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Wizara ilifanya ziara katika maeneo mbalimbali, kutoa elimu kuhusu masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuelezea fursa na changamoto zilizopo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Vilevile, Wizara ilishiriki katika Maonesho ya Nane Nane yaliyofanyika kitaifa mwezi Agosti, 2008 Mjini Dodoma na kuweza kutumia fursa hiyo kuwaelimisha wananchi kuhusu masuala mbalimbali ya Jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara iliandaa kikao maalum kwa Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Novemba, 2008 na Baraza la Wawakilishi Zanzibar mnamo mwezi Januari, 2009. Lengo lilikuwa ni kutoa taarifa kwa Waheshimiwa Wabunge na Baraza la Wawakilishi, juu ya maendeleo ya majadiliano ya Soko la Pamoja la Afrika Mashariki. Mwezi Desemba, 2008 Wizara ilifanya ziara ya kikazi na kukutana na wananchi katika Wilaya zote za Unguja na Pemba, kwa lengo la kutoa elimu juu ya masuala ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika juhudi za kuboresha mawasiliano, utoaji habari na elimu kwa Umma, Wizara imekamilisha maandalizi ya Tovuti ya Wizara. Tovuti hii inapatikana kupitia *www.meac.go.tz.* Wizara inaendelea na maandalizi ya mfumo wa kutunza kumbukumbu, utakaowezesha wadau mbalimbali kupata taarifa mbalimbali

kuhusiana na mtangamano wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na shughuli za Wizara kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara itaandaa vipindi maalumu kupitia radio na rluninga kuelezea matukio mbalimbali ya mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, Wizara itaandaa majarida kwa wakati maalum kutoa taarifa kwa Umma, yakayosambazwa kwa wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine tena, napenda kuwashukuru wadau wote ambao wamekuwa wakishirikiana na Wizara katika shughuli za kuendeleza Mtangamano wa Afrika ya Mashariki, ikiwa ni pamoja na Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali, toka Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Taasisi mbalimbali za Sekta binafsi, Asasi zisizo za kiserikali, wadau wa Maendeleo na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano na Wabunge wa Bunge la Afrika ya Mashariki.

Shukrani za pekee, ziende kwa Viongozi, hususan Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa miongozo thabiti ambayo imeiwezesha Wizara yangu kujiamini katika majadiliano mbalimbali na katika kuendeleza mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika mwaka wa fedha 2008/2009, zipo changamoto ambazo lazima tukabiliane nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na fursa zilizopo na zinazoendelea kupatikana kutokana na mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, bado wazalishaji na wafanyabishara wa Tanzania, wanakabiliwa na changamoto ya kuhakikisha kuwa uzalishaji unaongezwa, bidhaa zinaongezewa thamani na zinakuwa na ubora unaokidhi mahitaji ya soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Serikali na wadau wa maendeleo, wanachukua hatua mbalimbali kukabiliana na changamoto hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikilinganishwa na Nchi nyingine Wanachama wa Jumuiya, Tanzania imejaliwa kuwa na ardhi kubwa inayofaa kwa kilimo. Changamoto iliyopo ni kujipanga kimkakati ili kuhakikisha nchi yetu inakuwa mzalishaji mkuu wa mazao ya kilimo na kulisha Afrika Mashariki na nje ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na jiografia, Tanzania inayo kila nafasi ya kuwa kitovu cha usafirishaji. Changamoto ni kujipanga kimkakati kwa kuimarisha miundombinu, hususan barabara, reli na bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vikwazo vya kibiashara visivyo vya kiforodha, *(Non Tariff Barriers – NTB)*, vimeendelea kuwa changamoto katika utekelezaji wa Umoja wa Forodha. Naendelea kutoa wito kwa wafanyabishara wote, kuwasilisha malalamiko yatokanayo na vikwazo visivyo vya kodi ili Wizara iweze kuchukua hatua husika na hivyo kuwawezesha wafanyabishara wetu kunufaika kama inavyotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

(a) Kukamilisha maandalizi ya Sera ya Taifa ya Mtangamano wa Kikanda wa Afrika Mashariki.

(b) Kuratibu na kusimamia Utekelezaji wa Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na itifaki zake.

(c) Kukamilisha majadiliano ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(d) Kuandaa na kusimamia Mkakati wa Utekelezaji wa Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(e) Kufanya tafiti na tathmini za utekelezaji wa Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Itifaki zake na kuishauri Serikali ipasavyo.

(f) Kuratibu na kushiriki katika kufanya tathmini ya utekelezaji na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa Miradi na Programu za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(g) Kuratibu na kushiriki katika mikutano na Vikao vya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuanzia ngazi ya Wataalam hadi Mkutano wa Kilele.

(h) Kufanya maandalizi ya majadiliano ya Sarafu Moja ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(i) Kushirikisha Sekta binafsi katika masuala mbalimbali ya uendelezaji wa Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(j) Kutoa elimu kwa umma na kwa wakati kuhusu fursa na changamoto zilizopo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(k) Kuimarisha uwezo wa Wizara kiutendaji, kuwaendeleza watumishi na kutoa huduma bora kwa wateja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki, na kwa niaba ya Jumuiya ya Afrika Mashariki napenda kuwashukuru kwa dhati, wale wote walioshirikiana nasi katika kipindi cha mwaka 2008/09 katika kutimiza malengo yetu, ikiwa ni Wizara na Taasisi mbalimbali za Umma, Sekta Binafsi, Taasisi Zisizo za Kiserikali kama nilivyokwishaainisha katika Hotuba yangu. Pamoja na Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, inayoongozwa na Mtanzania Mwenzetu, Balozi Mwapachu. Aidha, shukrani zetu ziwaendee pia washiriki wenzetu wa maendeleo, wanaoshirikiana nasi katika kutekeleza programu na mipango mbalimbali ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, hususan Jumuiya ya Ulaya, Serikali ya Shirikisho la Ujerumani, Shirika la Misaada la Watu wa Ujerumani, *Gorovo Environmental Facility, UN Habitat,* Shirika la Misaada la Sweden, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Serikali ya

Japani, Benki ya Japani ya Maendeleo ya Kimataifa na Benki ya Dunia na nyinginezo ambazo hatukuzitaja, sio kwa makusudi, lakini kwa sababu zisizoweza kuzuilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Wizara ya Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki iweze kutekeleza majukumu na kufikia malengo yake kwa mwaka 2009/2010, naomba sasa nitoe hoja kuwa, Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 14,065,789,000 kwa ajili ya Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka 2009/10. Kati ya fedha hizo, shilingi 13,300,000,000 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo *(OC)*, shilingi 619,000,000 ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi *(PE)* na shilingi 146,789,000 kwa ajili ya Fedha za Mradi wa Maboresho *(PSRP II)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tena kuchukua nafasi hii, kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara kwa anuani ya www.meac.go.tz.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, kabla sijaanza kuwasilisha Hotuba ya Kamati ya Ulinzi na Usalama, nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kupata fursa hii na kunijalia nimesimama mbele yako. Pia nichukue nafasi hii, kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Iramba Magharibi, kwa ushirikiano wanaonipa muda wote katika kutekeleza majukumu yangu na kutekeleza Ilani ya CCM. Nimshukuru Mke wangu Hajra, wanangu Siti, Latifah, Feisal na Fahad, kwa kunitia moyo muda wote katika kazi zangu, hasa katika kulitumikia Jimbo la Iramba Magharibi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii, niweze kuwashukuru Madiwani wenzangu wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, chini ya Mwenyekiti wetu, Peter Kim Muna, kwa kazi ambayo tumekuwa tukiifanya, pamoja na Mkurugenzi wetu, Fortunatus Fwema, Watendaji, pamoja na *DC* wa Wilaya ya Iramba, Mama Grace Mesaki. Nasema nawashukuru sana, kwa sababu tumekuwa tukishirikiana nao vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije moja kwa moja kwenye Taarifa ya Kamati. Kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, Kanuni ya 99 (7) na Kanuni ya 114(11), naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa Fedha 2008/2009 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo, kwa mwaka wa Fedha 2009/2010 na kuliomba Bunge lako tukufu liipokee na kuijadili Taarifa hii na hatimaye kukubali kuidhinisha Makadirio ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kukushukuru wewe mwenyewe, kwa kunipatia nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 3 Juni, 2009, Kamati ilikutana kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kuhusu Utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha wa 2008/2009 na kufikiria Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yetu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, ilijadili Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka 2008/2009. Katika taarifa hiyo, Kamati ilielezwa yafuatayo:-

(i) Utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Forodha katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, iliyojikita katika kuondoa ushuru wa Forodha miongoni mwa nchi wanachama na kuondoa vikwazo visivyo vya kiforodha.

(ii) Kushiriki kikamilifu katika majadiliano ya kuanzisha soko la pamoja la Afrika Mashariki.

(iii) Utekelezaji wa Mkataba wa uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Itifaki zake na Maamuzi mbalimbali ya vyombo vya Jumuiya ikiwemo Mkutano wa Wakuu wa Nchi, Baraza la Mawaziri, Bunge na Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(iv) Utekelezaji wa Miradi na Programu za Kisekta katika Jumuiya ya Afika Mashariki. Hii ni pamoja na Sekta ya Miundombinu, Nishati, Afya, Elimu na Sayansi, Sheria, Maji na Mazingira, Kilimo na Mifungo, Ulinzi na Usalama.

(v) Kutoa Elimu kwa wananchi kwa ujumla katika Mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar kuhusu Masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(vi) Kutumia Balozi zetu nchini Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi katika kuendeleza biashara na uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kwa kiasi kikubwa, Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki imejitahidi katika utekelezaji wa majukumu yake, sambamba na kutekeleza ahadi za Serikali Bungeni. Hata hivyo, Kamati hii ilielezwa changamoto zilizojitokeza kwa mwaka wa fedha uliopita. Changamoto hizo ziligusa maeneo yafuatayo:-

(i) Kuongeza uzalishaji na ubora wa bidhaa ili kukidhi mahitaji ya soko la Jumuiya ya Nchi za Afrika Mashariki na kuhimili ushindani.

(ii) Kunahitajika miundombinu ya kisasa mathalani barabara, reli, uhifadhi na usafiri wa anga, maabara za kisasa za kudhibiti ubora wa bidhaa kwa ajili ya soko la Afrika Mashariki.

(iii) Uchanga wa Sekta binafsi ambao ni mdau mkubwa katika kuimarisha biashara katika soko la nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kuna umuhimu wa kuweka mikakati mahususi ya kuendeleza sekta binafsi inayohimili ushindani na kuwa na uhakika wa soko.

(iv) Kuwawezesha Watanzania kunufaika na fursa zilizopo na kupambana na changamoto zitokanazo na mtagamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(v) Matumizi ya teknolojia iliyopitwa na wakati katika uzalishaji na nyenzo duni za uzalishaji zisizoweza kuhimili ushindani.

(vi) Taratibu za kiutawala zinazokwaza mwenendo wa bidhaa ndani na mipakani kama vile kuendelea kuwepo na kuongezeka kwa vikwazo visivyo vya kiforodha.

(vii) Kuhakikisha kuwa Tanzania inao mkakati madhubuti wa kitaifa utakaotumika kama mwongozo katika majadiliano na shughuli za kuendeleza Mtangamano wa Jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kupitia na kuchambua Makadirio ya Matumizi ya Wizara hii, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali kuhusu Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, katika mwaka wa fedha wa 2008/2009, Serikali imetoa ushirikiano na inaendelea kutekeleza ushauri wa Kamati. Kwa mfano, Serikali imezingatia ushauri kuhusu utaratibu wa kisheria wa kuwalinda Watanzania na ardhi yao dhidi ya wageni. Kamati ilielezwa kuwa Katika kikao cha Wakuu wa Nchi za Afrika Mashariki *(Summit),* kilichofanyika tarehe 29 Aprili, 2009, nchi wanachama zimekubaliana kuwa masuala ya ardhi na ukazi wa kudumu yaongozwe na Sheria za kila nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ajira katika Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki;, tulielezwa kuwa Baraza la Mawaziri wa Sekta ya Mambo ya Nje (*Sectoral Council on Foreign Policy Coordination*), wanaendelea na majadiliano juu ya namna ya kutekeleza Mkataba wa Makao Makuu (*The Headquater Agreement*) hususan suala la ajira kwa nchi wenyeji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka uliopita, Mheshimiwa Dokta Diodorus Kamala, Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, aliieleza Kamati hii kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010, pamoja na kuwasilisha Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na yale ya Maendeleo kwa Fungu 97. Katika Makadirio hayo, Kamati ilielezwa kuwa, Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 14,144,000,000. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida *(OC)* ni shilingi 13,300,000,000. Mishahara *(PE)* shilingi 619,000,000 na fedha za Maendeleo ni shilingi 146,789,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilichambua na kutafakari kwa kina, Taarifa ya Utekelezaji wa Wizara kwa Mwaka wa Fedha uliopita na kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2009/2010, kama zilivyoainishwa kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri ilivyowasilishwa hivi punde. Kamati inaunga mkono hoja ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki na kuliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha maombi hayo, pamoja na maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inayo maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Serikali iweze kunufaika na fursa za kibiashara zinazotolewa na nchi wanachama, suala la uwiano wa fursa hizi lizingatiwe ili kuondoa vikwazo mbalimbali katika uingizwaji wa bidhaa katika nchi wanachama. Uzoefu unaonesha kwamba, bidhaa za Tanzania katika nchi wanachama, zinakutana na vikwazo vya kibiashara vinavyoathiri upatikanaji wa bidhaa hizo, ikilinganishwa na bidhaa za nchi wanachama nchini Tanzania. Hivyo basi, Serikali iweke utaratibu makini na madhubuti, utakaosaidia uingizwaji wa bidhaa zetu katika soko la nchi wanachama, ikilinganishwa na upatikanaji wa bidhaa za nchi wanachama katika masoko yetu.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nchi yetu imepewa heshima ya kuwa Mwenyeji wa Makao Makuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki Jijini Arusha, fursa ambayo ni kichocheo katika kuinua uchumi wa nchi yetu, juhudi za makusudi zichukuliwe ili kuharakisha ukamilishwaji wa ujenzi wa Miundombinu ya Makao Makuu ya Jumuiya ya nchi za Afrika Mashariki.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali yetu imekusudia kuwainua kiuchumi Wajasiriamali wa ndani kwa kuwapa fursa ya kupata masoko ya bidhaa zao katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, juhudi za makusudi za kuboresha na kuimarisha utendaji kazi wa Mashirika ya Viwango zinahitajika ili kuwapa Wajasiriamali uwezo wa kuinua viwango vya bidhaa zao katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(d) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iongeze kasi ya kuelimisha na kuwahamasisha Watanzania, kununua na kutumia bidhaa za hapa nchini, ambazo zina ubora wa kuridhisha na kuwezesha uuzaji wa bidhaa zetu kwenye masoko ya Afrika ya Mashariki na Nje. Aidha, Wakuu wa Mikoa na Wilaya zote nchini, wawaelimishe wananchi kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu Jumuiya ya Afrika Mashariki

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Itifaki ya Umoja wa Forodha inatarajiwa kuanza rasmi ifikapo mwaka 2010, ambapo ushuru wa bidhaa kati ya nchi anzilishi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, yaani Tanzania, Kenya na Uganda, utakuwa umeondolewa kabisa, Kamati inaitahadharisha Serikali kutoharakisha kuingia katika utaratibu huu ili kuandaa mazingira sahihi, mkakati makini na madhubuti wa kitaifa, ambao utawawezesha Watanzania kunufaika kikamilifu na Itifaki ya Umoja wa Forodha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kukupongeza wewe binafsi, kwa jinsi unavyoliongoza Bunge letu Tukufu. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, kwa jinsi wanavyokusaidia kuongoza vikao. Napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Dokta Diodorus Kamala, Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Mheshimiwa Mohamed Aboud, Naibu Waziri na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dokta Stergomena L. Tax, Katibu Mkuu, pamoja na Wataalam wa Wizara hiyo, kwa ushirikiano wao na kazi nzuri sana katika kutetea maslahi ya taifa na kuimarisha ushirikiano katika Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa, nachukua fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano wao na kwa kufanya Uchambuzi wa kina, uliowezesha hoja hii kufikia hatua iliyopo sasa. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kwa majina kama ifuatavyo: Mheshimiwa Wilson M. Masilingi - Mwenyekiti, Mheshimiwa Musa A. Zungu - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Anna M. Abdallah, Mheshimiwa Mohamed A. Abdulaziz, Mheshimiwa Col. Mst. Saleh A. Farrah, Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa, Mheshimiwa Hassan C. Kigwagilo, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa William J. Kusila, Mheshimiwa Edward N. Lowassa, Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mheshimiwa Dokta John S. Malecela, Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, Mheshimiwa Col. Mst. Feteh S. Mgeni, Mheshimiwa Ali A. Mohamed, Mheshimiwa Dokta Ibrahim S. Msabaha, Mheshimiwa Balozi Abdi H. Mshangama, Mheshimiwa Thomas A. Mwang'onda, Mheshimiwa Brig. Jen. Mstaafu Hassan A. Ngwilizi, Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu, Mheshimiwa Masoud A. Salim, Mheshimiwa Muhammad I. Sanya, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo na Mheshimiwa Magalle J. Shibuda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, lakini si kwa umuhimu, napenda niwashukuru Dokta Thomas D. Kashililah, Katibu wa Bunge na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge, kwa kufanikisha shughuli za Kamati kama zilivyopangwa. Shukrani maalum ziwaendee Makatibu walioihudumia Kamati hii; Ndugu Athuman Hussein na Ndugu Stella Mlambo, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu, likubali kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kama alivyowasilisha mtoa hoja muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii na ninaomba kuwasilisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SALIM YUSUF MOHAMED (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA USHIRIKIANO WA AFRIKA YA MASHARIKI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kusimama hapa leo na kutoa maoni ya Kambi yetu. Pia napenda nitoe shukrani zangu za dhati kwako, kwa kunipa fursa hii ya kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu ushirikiano wetu wa Umoja wa Afrika ya Mashariki, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 99(3) na (7), Toleo la 2007. Kabla sifanya hivyo, naomba nitoe pole kwa wale

wote waliofikwa na misukosuko ya kimaisha, ikiwemo vifo vya wanafamilia au kuumia, tunamwomba Mwenyezi Mungu, awape subira kwa mitihani hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Chama Changu cha Wananchi *CUF*, Chama Kikuu cha Upinzani hapa Tanzania. Pia nawashukuru Wananchi wa Jimbo langu la Kojani, kwa ushirikiano mzuri wanaonipa. Aidha, naushukuru Uongozi wa Kambi ya Upinzani, chini ya Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Naibu wake, Mheshimiwa Dokta Slaa, kwa kutuongoza vyema katika Kambi yetu. Kipekee, nawapongeza wanafunzi; Dikombo Juma Suleiman kutoka Shule ya Sekondari Mchanga Mdogo, Pemba, kwa kupata tuzo ya Mshindi wa Pili kwa uandishi wa insha katika mashindano ya Jumuiya kwa mwaka 2008; na Daniel Andondile kutoka Shule ya Sekondari Masukila, Mkoani Mbeya, kwa Tuzo ya Mshindi wa pili kwa mwaka 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki, yaani Burundi, Kenya, Uganda, Ruanda na Tanzania, bado haijakomaa na kwa maana hiyo ushirikiano huu bado unahitaji usimamizi mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti kubwa zilizopo baina ya nchi tano hizi kijamii, kiuchumi na hata kisiasa, bado zinaufanya umoja huu kuwa mgumu. Lazima tujielekeze katika mikakati ya kuweka pamoja utaratibu wa sheria za jamii na soko la pamoja. Ibara ya 76(1) ya Mkataba wa Jumuiya, imeainisha nyanja za ushirikiano katika soko la pamoja kuwa ni pamoja na uhuru wa watu kwenda wanakotaka, uhuru wa kutoa huduma kibiashara na uhuru wa kuhamisha mitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vikwazo hivi bado vipo na pale tutapojaribu kuvitatua ndio tunaongeza wigo wa suala zima la ushirikiano baina ya nchi hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 104(2) ya Mkataba wa Jumuiya, inatoa uhuru wa kuishi popote katika Jumuiya. Nalo hili pia lina matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vigumu sana kwa suala la ardhi tukaliacha holela. Haitokuwa vyema kwa Wanachama wa Jumuiya kutoka nchi jirani kujipatia ardhi ya Tanzania bila kuwepo na utaratibu wowote wa kisheria. Suala hili, Wananchi wa Tanzania hawalihitaji kuwemo ndani ya soko la, pamoja. Hivyo ni lazima tuhakikishe kuwa ardhi ya Tanzania haichukuliwi na wasiokuwa Watanzania. Kwa maana hiyo, Sheria za Ardhi ni lazima zirekebishwe na au kubadilishwa ili rasilimali hii iendelee kuwa mikononi mwa Watanzania wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Mtandao wa Miundombinu utasaidia sana ukuaji kiuchumi wa Nchi Wanachama wa Afrika Mashariki hasa katika zile barabara zilizoko katika mlango *(corridor)* nambari moja mpaka tano. Hata hivyo, jambo moja la kusikitisha ni kuwa, harakati hizi za miundombinu kwa Mwambao wa Pwani ya Afrika Mashariki umesahaulika kiuchumi na kimaendeleo.

Je, ni kweli kuwa hakuna uwezekano wowote wa kuunganisha Mtwara – Dar es Salaam – Zanzibar – Pemba – Tanga – Mombasa – Lamu kwa kuwa na bandari zinazokidhi haja kwa ukubwa, ubora na usafiri wa uhakika wa kuunganisha bandari zetu kama zilivyobuniwa Barabara za Mombasa – Kigali – Himo *(Corridor No. 1);* Dar es Salaam – Kigali (*Corridor No. 2);* Biharamulo – Lodwan – Lokichogio (*Corridor No.* 3); Tunduma – Gisenyi (Rwanda) (*Corridor No. 4);* na Tunduma – Namanga – Moyale (C*orridor No. 5)*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wanaoishi pembeni mwa Ziwa Victoria, nao wanafaidika na ushirikiano huu wa pamoja kwa kuwa na mradi wa kuendeleza Bonde la Victoria, ambao lengo lake ni kuwasaidia raia wa nchi hizi wanaoishi pembezoni mwa Ziwa hilo.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna mpango wa kuinua uchumi wa wakazi wa maeneo ya Ziwa Victoria, kwa kutambua maliasili za uwekezaji zilizopo na zinazoweza kutumika bila ya kuharibu mazigira kwa kuuwezesha umma kuwekeza na kutunza mazingira na miradi ya wakazi. Haya pia yanaweza yakafanyika kwa watu wanaoishi Mwambao wa Afrika ya Mashariki. Je, ni kitu gani kilichozuia hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Forodha nao una matatizo yake. Bado kuna baadhi ya nchi kama vile Kenya, hazifanyi wajibu wake kama wanavyotakiwa wafanye chini ya mkataba wa kuanzishwa Jumuiya hiyo. Mifano ipo mingi:-

*(i)* *Internal Tariff Elimination* ambayo ina lengo la kuondoa ushuru wa forodha miongoni mwa nchi wanachama haijatekelezwa vizuri na hivyo kuleta matatizo miongoni mwa jamii ya Wana-Afrika Mashariki.

*(ii)* *Elimination of Non Tariff Barriers* ni tatizo lingine kubwa, kwa mfano, viwanda vya Tanzania vinapangiwa *quarter* ya kupeleka Kenya na pia kutozwa ushuru, ambapo hili ni kinyume na utaratibu wa itifaki wenyewe. Je, Serikali imechukua hatua gani hadi sasa ili kuvihami viwanda vyetu na hivyo kutoa motisha kwa Watanzania katika kuimarisha viwanda vyetu; kwa mfano, viwanda vya maziwa Kenya ni *zero tariff* wakati Tanzania kodi ni asilimia 25 na kadhalika? Leo viwanda 12 vya maziwa vimefungwa na vilivyopo vinazalisha wastani wa lita 60,000 kwa siku, wakati Kenya vinazilisha 1.2 million liters kwa siku. Hivi Watanzania wanafaidika na soko hili la Afrika Mashariki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Soko la Pamoja bado halijafikia ufumbuzi wa uhakika. Je, ni maamuzi yapi yachukuliwe baina ya nchi na nchi bila ya pingamizi yoyote?

Ufumbuzi wa Soko la Pamoja utakuwa ni ufumbuzi wa njia za kiuchumi na kijamii na hivyo ni lazima tulitafutie ufumbuzi wake haraka, ikiwa tuna lengo la kweli la kukuza uchumi na maendeleo ya kijamii. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima maandalizi ya kukamilisha mikakati hii ya kisekta ya soko la pamoja yajumuishe wadau wote ili Tanzania inufaike kikweli kweli katika nyanja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina Balozi zake katika nchi za Burundi, Kenya, Uganda na Rwanda. Tukizitumia vizuri Balozi hizi zinaweza kuwasaidia sana Watanzania kibiashara. Tunajua kama Balozi hizi zimewahi kuwahamasisha wananchi wetu hususan wafanyabiashara, kutembelea nchi hizo na kukutana na wafanyabiashara wao. Suala ni kuwa je, Wafanyabiashara hawa wa Tanzania wamesaidia Tanzania yetu kuingizia fedha za kigeni kwa kiasi gani? Uwiano wa biashara na nchi husika ukoje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaamini kuwa, bado kazi kubwa haijafanyika na Watanzania tusipochangamkia suala hili, basi siku zote tutabaki nyuma na kuwaacha hata Burundi na Rwanda waliojiunga na shirikisho hili hivi karibuni, kutupita katika shughuli hizi za biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na Zanzibar: Kama tulivyosema katika hotuba zetu za nyuma kwamba, Zanzibar bado ni mtoto yatima katika Jumuiya hii. Mambo kadhaa ambayo si ya Muungano, ambayo kikatiba zetu yanapaswa kushughulikiwa na Zanzibar yenyewe au na Tanzania Bara yenyewe, sasa yamo katika orodha ya Afrika Mashariki; ambayo kwayo yanashughulikiwa na Tanzania! Hii ndio maana kukawa hakuna mkazo mkubwa wa kuhimiza ile miradi iliyoombewa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti mbili zilizopita tuliambiwa kuwa, Tanzania imewasilisha mapendekezo ya miradi inayoweza kutekelezwa Zanzibar chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Miradi hii ni pamoja na: Uwanja wa Ndege wa Kimataifa; uwekaji wa vituo vya umeme wa upepo; ujenzi wa Bandari ya Maruhubi; magonjwa ya Wanyama; uongezaji wa ubora wa mazao; uanzishwaji wa *Roll on Roll off services* kati ya Bandari ya Zanzibar, Dar es Salaam na Mombasa; na Mradi wa Uwanja wa Ndege wa Karume na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Mheshimiwa Waziri anaweza kutuambia kwa uhakika ni mradi gani kati ya hiyo niliyoitaja angalau umefikia asilimia kumi ya utekelezaji wake? Tunaamini kwamba hakuna, kwani Mheshimiwa Waziri bado anaendelea kutupa hadithi ile ile ya miaka ya nyuma. Huu ni kama ule msemo wa Kiswahili unaosema; "Kuku lalala Kipanga yuaja." Sasa upungufu huu unazidi kuweka mazingira ya Zanzibar kama ni ya kutengwa na kwa maana hiyo, kuleta picha mbaya ndani ya Muungano wetu na katika shirikisho lenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili Mheshimiwa Waziri ameliona; na vipi ataweza kulitatua? Imedhihirika kwamba, katika Wizara nzima ya Afrika Mashariki, Wazanzibari hawafiki wawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli zozote zile za Jumuiya, huendeshwa kwa kuzingatia Kanuni na Sheria zinazotawala sekta hizo. Tatizo kubwa liliojitokeza katika

Jumuiya yetu ni kucheleweshwa kwa kupitishwa kwa sheria hizo na hususan kucheleweshwa kwa kupata saini za wakuu wa nchi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa Kambi ya Upinzani ni kuwa, pawepo muda maalum wa kuwataka wakuu hao wa nchi, kuweka sahihi zao ili lengo lililokusudiwa liweze kuanza haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba wa Jumuiya ulisainiwa Novemba, 30, 1999 na ukaanza rasmi Julai, 7, 2000. Kuna mambo yamebadilika na ambayo ni vyema yakaangaliwa upya kimkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji huu wa kisiasa pamoja na kuingiza wanachama wapya wawili na tukiangalia mazingira yalivyo, sisi tuna imani kubwa kuwa, sasa ni wakati wa kuutazama upya mkataba huu kwa njia ya kurekebisha baadhi ya vifungu ambavyo tunaamini kuwa vimepitwa na wakati au vinahitaji mabadiliko. Hii ni kuisaidia zaidi Jumuiya yetu kwa maana ya kuifanya iwe imara zaidi kuliko hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya hii ya Afrika Mashariki, ikiwa tutayatekeleza vyema masharti ya mkataba wake, basi itawasaidia sana wanachama na kuwachochea wafanyabiashara binafsi. Tunaweza kusema Jumuiya hii inaweza kabisa kuwa *people centred na private sector drive;* hivyo ni muhimu kwa jumuiya hii:-

(a) Kwa wanachama wake, yaani nchi wanachama, wanaaminiana na kuheshimu uhuru wa kila nchi.

(b) Kuendeleza mbele ujirani mwema na kuishi bila ya kugombana.

(c) Kupigania Utawala Bora pamoja na kila mwanachama kuwa mstari wa mbele katika kutatua mgogoro wa mwenzake unapotokea.

(d) Kujitahidi kugawana sawa sawa faida zinazotokana na ushirikiano huo.

(e) Kuwa Utaifa wa Afrika Mashariki lazima uwekwe mbele kuliko ule Utaifa wa nchi kwa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiyaweza hayo, ninaamini kuwa Jumuiya yetu inaweza kuwa Jumuiya ya kupigiwa mfano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nawashukuru wote kwa kunisikiliza. Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Salim Yussuf Mohamed, Mbunge wa Kojani, kwa niaba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwenye Sekta hii ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Waheshimiwa Wabunge, orodha niliyonayo hapa mezani ni ya wachangiaji wanne mpaka sasa hivi na nitawataja wote ili kwa wale ambao watakuwa wako nje, waweze kurudi ndani na kuweza kujitayarisha.

Msemaji wetu wa kwanza ni Mheshimiwa Joseph J. Mungai, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah na Mheshimiwa Prof. Philemon Sarungi, atafuata baada ya hapo.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Joseph Mungai aanze kuchangia leo; karibu.

**MHE. JOSEPH J. MUNGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niwe mchangiaji wa kwanza asubuhi hii. Ninapenda niseme tangu mwanzo kwamba, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni muhimu sana katika lengo la kuunda muundo mkubwa zaidi wa kiutawala na kiuchumi katika Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muundo wetu wa sasa wa nchi tulizonazo tofauti Kenya, Uganda, Tanzania, Rwanda na Burundi, kwa kweli si wa kujitakia sisi wenyewe. Ukiangalia katika *record* ya historia, nchi hizi na mipaka yake inatokana na Kongamano la Berlin, yaani *Berlin Conference of 1884*, ndipo walipokaa nchi wanaonyemelea maeneo yatu na wakakubaliana mgawanyo na ndiyo tukawa na mipaka hii ya leo. Haikuwa tu hilo Kongamano, lakini pia walisaini mkataba *unaoitwa The Limitation Treaty of 1885* na wakaweka mipaka na zikaja zikawekwa *beacons* za kuonesha hii mipaka.

Kwa hiyo, napenda kusisitiza jambo hili kwamba, Muundo wa nchi hizi siyo wa kujitakia sisi wenyewe, lakini muundo wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki huu ndiyo wa kujitakia kukubaliana mipaka iwe mikubwa zaidi na tuwe nchi kubwa zaidi na tuwe soko kubwa zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nasema Wizara hii ni muhimu sana na ningependa kuchukua nafasi hii kutoa wito kwamba, ipo haja ya kuongeza kasi ya kuelekea kwenye kukamilisha muundo tunaoutaka, ambao ni kufikia hatua ya *federation*, yaani kuwa na Serikali kamili ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunapoelekea huko ni muhimu sana pia ndani ya vichwa vyetu na ndani ya matamko yetu, tusiwe wang’ang’aniaji sana wa muundo huu tulioundiwa na watu wa Ulaya, tusizidishe mno kung’ang’ania Utanzania, Ukenya, Uuganda na Urundi na hata tukafikia kuchelewa kutengeneza muundo ambao tunaona unatufaa ambao ni huu wa kuwa ni nchi inayoitwa *Federation of East Africa* yenye nchi tano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kusema kwamba, wakati mchakato wa kuelekea *federation* bado unaendelea, ziko hatua ambazo tunaweza kuzichukua na kuzianzisha upesi zaidi za ushirikiano wa kiuchumi, ambao utafanya soko hili lianze

kutumika vizuri zaidi. Mimi ninapenda kushauri kwamba, pamoja na hatua za kuelekea kwenye soko la pamoja na kuelekea kwenye *federation*, hatua ya mapema ichukuliwe chini ya Uongozi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ya kuyaunda upya na kuyafanya yafanye kazi mashirika manne yafuatayo:-

Kwanza, Shirika la Reli la Afrika Mashariki. Mimi naona tumesahau tunaangalia mambo mengine, usafiri wa reli ni muhimu sana katika kuhudumia uchumi na katika kukuza uchumi, vilevile katika kusafirisha bidhaa kutoka nchi moja kwenda nyingine, katika kulihudumia soko kwa unafuu na kwa unafuu zaidi. Kwa hiyo, Jumuiya ya Afrika Mashariki itoe uongozi na ifanywe juhudi maalum kwamba, *East African Railway*, yaani Shirika la Reli la Afrika Mashariki liundwe upya kuliko kuwa na mashirika tofauti ya Tanzania, Uganda, Kenya na sasa Reli yetu inapanuliwa kwenda Rwanda na Burundi, nao wawe na mashirika tofauti.  Tuliunde upya Shirika la Reli la Afrika Mashariki.

Pili, Shirika la pili ni Shirika la Ndege la Afrika ya Mashariki, yaani *East African Airways.* Mimi nilikuwa Mjumbe wa Baraza la Mawaziri, lililokuwa linasimamia mambo ya mawasiliano katika Afrika ya Mashariki katika kipindi cha kwanza nilipokuwa Waziri wa Kilimo na niliona *record* zinazoonesha kwamba, *East African Airways i*liyokuwepo ilifanya faida tangu mwaka 1947 ilipoundwa mpaka mwaka 1977*, it was a profitable airline* na ilipigwa vita na wakubwa kwa kuwatumia baadhi ya wenzetu katika Afrika ya Mashariki.

Hiyo ni *record* sahihi kwamba, ushirikiano katika biashara ya ndege ni jambo lenye faida kwa sababu tulikwishakuwa nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusing'ang'anie tu ule mtindo, ulikuwepo mtindo wa kila nchi kuwa na shirika lake la ndege. Nchi zetu zilivyopata uhuru, mambo matatu yalikuwa yanajitokeza katika kila nchi. La kwanza ni bendera ya taifa, wimbo wa taifa la pili, shirila la ndege la tatu.  Sasa wakati wa *honey moon* hiyo ya kupata uhuru imekwisha na biashara ya ndege inatambulika kabisa kimataifa kwamba, haiwezekani kwa nchi moja moja peke yake kuwa na shirika la ndege likaleta faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri Jumuiya ya Afrika Mashariki iongoze mjadala wa kuyaunganisha kiuchumi *Kenya Airways, Air Tanzania, Uganda Airlines*, *Air Rwanda na Air Burundi* na mkakati ulio sahihi kwa leo ni kujiunga na lile shirika katika mashirika yote haya linaloonekana linaendeshwa kwa faida ni *Kenya Airways* kwa *Kenya Airways,* tayari lina ushiriki wa  Tanzania kupitia *Precision Air na Kenya Airways* ina ushiriki pia wa muunganiko na KLM, ambao ndiyo mtindo wa sasa kwa biashara ya ndege, lazima uunganike na shirika lililo na *network*. Kenya Airways ni tayari liko katika Soko la Hisa la Dar es Salaam, Nairobi na Soko la Hisa la Uganda, yaani Kampala. Kwa hiyo, mimi nafikiri *East African Community* itoe uongozi kuyaweka pamoja mashirika haya yaweze kuunganika, lakini katika muunganiko ambao ni *private sector driven,* yaani unaoongozwa na sekta binafsi. Kwa hiyo, hilo ni shirika la pili.

Shirika la tatu ambalo nashauri ingefaa lifufuliwe mapema iwezekanavyo ni Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki, yaani *East African Currency Board.* Sitaki kulisemea

sana hili kwa sababu Mheshimiwa Waziri ameeleza baadhi ya hatua ambazo wanazichukua; kamati imekwishaundwa ya kutuelekeza kwenye sarafu ya pamoja. Kwa hiyo, naona hizo ni hatua za kuelekea kuianzisha upya ile *East African Currency Board* iliyokuwepo ili tufikie kuwa na aina moja ya fedha katika Afrika Mashariki, itasaidia sana kukuza uchumi wetu.

Shirika la nne ambalo nashauri kuna haja ya kuunganishwa kwa masoko ya hisa ya nchi zetu, yaani badala ya kuwa na *Dar es Salaam Stock Exchange au Nairobi Stock Exchange,* yaendelee kuwepo lakini masoko haya yaunganishwe kwa pamoja na ninashauri kwamba, Jumuiya ya Afrika Mashariki ingechukua hatua ya kutoa uongozi katika kuyafanya masoko ya hisa ya nchi zetu hizi yashirikiane kwa karibu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningependa pia hapa kuongeza shirika la tano nalo ni Baraza la Mitihani la Afrika ya Mashariki, yaani *East African Examination Council*. Mnapoelekea kwenye uchumi wa pamoja ni vizuri sana masuala ya Elimu yaendeshwe katika nchi zetu kwa kuzingatia *standard* moja ili tuwe pia na *coordination* ya *Curriculum* inayofundishwa tuwe na mitihani ya aina moja katika Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia kusema kwamba, yapo mambo yanayoathiri *speed* ya mchakato wa kuelekea kwenye soko la hisa la pamoja. Nikiangalia suala la kuelekea kwenye *federation* au muunganiko wa Afrika ya Mashariki, hivi karibuni limejitokeza kama kikwazo suala la ardhi. Upo uoga wa kila nchi kufikiria ardhi yetu tukiunganika na kufungua mipaka ardhi yetu italimwa na wengine na wapo wanaofikiri ni afadhali ardhi ibaki mapori hailimwi kuliko ikilimwa na wengine katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni yangu, siyo vizuri kwa nchi yoyote kuwa *land rich and income poor,* yaani tajiri wa ardhi lakini maskini wa mapato na hivi ndivyo Tanzania tulivyo ni tajiri sana wa ardhi. Ardhi ile inayolimwa uzalishaji ni karibu 10% mpaka 15% na sehemu kubwa ya ardhi yetu hailimwi. Bado kuna kufikiri kwamba, tukifungua mipaka italimwa na wengine maana afadhali ibakie wazi. Mimi nadhani mtazamo huu siyo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni yangu, ardhi ya ziada ni afadhali ilimwe na wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wabunge, mimi kwa maoni yangu kuhusu kuhodhi ardhi isiyo na mazao ni kuhodhi umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza kuwa tajiri sana wa ardhi isiyo na mazao, lakini ukaja ukafa maskini wa kupindukia. Kwa hiyo, mimi nasema ni afadhali jambo hili la ardhi litazamwe upya, litazamwe kwa makini sana ili tuwe na sera iliyo sahihi. Nchi zetu hizi za Afrika Mashariki zina utajiri mkubwa sana wa ardhi, maji mengi ya mito na maziwa na utajiri mkubwa sana wa jua. Unajua kwa sababu jua tunaliona kila mara, tuna-*take for granted* lakini ukweli ni kwamba, sisi tuna utajiri mkubwa sana wa jua kuliko

nchi za Ulaya; na ili mazao yaote unahitaji ardhi, maji na jua na ukiwa na mwanga mwingi wa jua na joto jingi mazao ya kilimo yanakuwa kwa upesi. Tukiunganika tutakuwa na utajiri mkubwa wa soko, sasa ili hizi *natural resources*, yaani utajiri huu wa maliasili nilizozitaja uweze kuwa na faida ni muhimu sana suala la ardhi lipewe mtazamo upya, unaozingatia kuendeleza ardhi na siyo kuihodhi, unaozingatia wawekezaji wa ndani na badala ya kufikiria tu wawekezaji wa ndani ya nchi moja moja, tuwatazame wawekezaji wa ndani ya soko la pamoja la Afrika ya Mashariki na kuwakaribisha wawekezaji wa kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo haya, naomba nimalizie kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Wasaidizi wake. Napenda pia kuwapongeza sana Watendaji wote katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, chini ya Mtanzania mwenzetu Balozi Juma Mwapachu, ambaye nafurahi kusema kwamba, ni *class mate* wangu kule *Tabora School* tukiwa darasa moja. Anatenda vizuri sana, kwa sababu alisoma katika shule nzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Mungai na sasa namwita Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi na Kiongozi wa Upinzani Bungeni. Karibu sana.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Awali ya yote, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, niwapongeze sana; Waziri, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na mambo machache tu; la kwanza nataka niungane na Mheshimiwa Joseph Mungai, kwa kumalizia kwamba, pamoja na vyombo alivyovitaja, kuna suala zima la wanafunzi wanaosoma Kenya, Tanzania, Uganda, Rwanda na Burundi. Viwango vya malipo yao vinatofautiana sana, nafikiri kuna haja ya kuweka utaratibu kwa sababu sasa tunaingia kwenye *common market,* baadaye tuone hawa wanafunzi wetu ni vipi tunaweza tukaweka uwiano wa malipo yao.

Kwa mfano, wanafunzi wanaotoka hapa Tanzania wakienda Kenya, bado hawawi *treated* kama ni wanafunzi wa *East Africa*, bali wanakuwa kama ni wageni tu na ninafikiri hata na sisi tunafanya hivyo. Sasa nasema hili nalo lingeangaliwa.

La pili, ambalo ningependa nilisemee vilevile ni hii *process* nzima ya kushirikiana, msingi wake mkubwa ni kwamba kwanza, tungekuwa na *process* ya kisiasa, yaani *Democratic Process* yetu iwe sahihi. Kila nchi sasa hivi ina utaratibu wake, hakuna nchi ambayo tuna mfumo mmoja wa kupata wagombea. Kadhalika, tumeshuhudia hata ule uchaguzi wa East Africa, pia nao una tofauti baina ya Bunge na Bunge kutegemea na Kanuni tulizonazo. Sasa nasema, pengine hili halitusidii sana, kama tunataka kuingia

kwenye *Political Federation* baadaye ni vizuri ile *process* yenyewe ya kiuchaguzi na kuwapata wagombea na kuwapata wapiga kura na kadhalika, basi ikawa *unified*, yaani ikawa namna moja ambayo inaweza kuwa ya wazi, inayoaminika na inayokubalika, ambayo itaondoa migongano kama ile hatua ambayo wenzetu wa Ghana wamefikia. Nafikiri hiyo itatusaidia kujenga misingi mingine; bila kujenga huo msingi wa kwanza kabisa huo wa kiutawala, hayo mambo mengine yatakuwa yanatupa tabu sana.

Lingine ambalo nafikiri vilevile tuliangalie ni suala la lugha. Jana mimi sikufurahi hata kidogo, kumwona Rais wetu wa Jamhuri na Rais wa Kenya, wanazungumza Kiingereza wakati tuko kwenye *East Africa* na Mabunge yetu yote haya wanasema lugha ya kwanza ni Kiswahili. Sasa nikasema kama hawa wakubwa wa nchi wote wanakubali kuwa lugha yetu ni Kiswahili halafu tuko tena Tanzania mnazungumza na Kiingereza, hivi hiki Kiswahili kitazungumzwa na nani ? Kwa hiyo, nikasema bado tuna matatizo ya msingi hatujataka kuyaelekeza, moja ni suala la lugha. Kama kweli tumekubaliana kuungana na kushirikiana, suala la lugha ni msingi sana na lazima lipewe *priority* na kuwe na *program* inayoeleweka juu ya suala zima la lugha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ni suala la ardhi. Hili suala liteleta mgogoro, lazima tukubali tu, kama hatukuwa waangalifu. Wenzetu kwa mfano Kenya, wameshafikia hatua nzuri kwamba, kila mtu anayo hati ya ardhi anayoimiliki. Kwa Watanzania hatujafika hapo, tumemwacha Rais ndiye tumempa mamlaka ya ardhi yetu yote. Sasa kama hatukuwa na mfumo wa aina moja wa kumiliki ardhi, tutakuwa na mgogoro mkubwa sana. Nafikiria kama hatujafikiria jambo lingine, kwa sababu utajiri wa kwanza wa kila mtu ni ardhi, pale unapozaliwa ndiyo rasilimali yako ya kwanza unayoimiliki. Sisi tumemwambia Rais wetu kwamba, wewe tunakukabidhi kila kitu, kwa wenzetu mfumo wao ni tofauti. Kama mifumo hii haijaoana na leo tunakubali wenzetu na wamefanya *investment* kubwa huku Tanzania, wako kwenye kilimo, viwanda na kadhalika, tutaendelea hivyo hivyo na kwa sababu sisi tuna rasilimali kubwa hatuitumii na hatuimiliki, tutapata matatizo makubwa sana. Mimi nafikiri ni lazima tuiwezeshe Wizara yetu ya Ardhi, tuipatie fedha, ipime maeneo yote wakabidhiwe Wananchi, tuseme haya ni kwa ajili ya *investment* na haya ni kwa ajili ya wenzetu wageni, lakini haya ni kwa ajili ya Watanzania na tunazaliana na vizazi na vizazi vijavyo vipate mahali pa kuishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia vijiji vya ujamaa tulivyokuwa navyo leo havipo tena. Gezaulole ilisifiwa kweli, lakini nenda kaangalie kama ipo tena. Haya ni mazingira halisi tu tuliyonayo. Kwa hiyo, suala la ardhi ni *crucial* kabisa, wala tusilipuuze hata kidogo ni suala *crucial,* lazima tuli-*address properly* na tulifanyie kazi halafu tutoe maamuzi, hata kama haizalishi lakini watoto wetu watakuja baadaye watazalisha mradi mtoto ana *own* kwamba hapa ndiyo mahali kwangu, leo haizalishi lakini kesho itazalisha ni akiba. Hiyo akiba lazima iwe na maana kwamba, mtu amegawiwa sehemu yake na anajua kwamba, hii ni sehemu yake anaimiliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la nne, nimefurahi sana wenzetu wa Kenya wamekuwa wa pili katika kuweka *investments.* Napenda nilishukuru sana Shirika letu la NSSF wamefanya kazi nzuri tu; wameisaidia Wizara ya Mambo ya Nje, kwani wamewekeza

kule lakini nasema twende mbali zaidi ya hapo na wamefanya hivyo kwa sababu ya uongozi imara na mahiri uliopo pale katika Shirika na Bodi yao nzuri tu inayofanya kazi. Tungeisaidia hii na vyombo vingine hata vya watu binafsi wakaweza, tatizo lililopo ni kwamba, Kenya wameweka utaratibu mzuri wa vyombo vya fedha. Vyombo vyao vya fedha vimeshaingia kwenye biashara, kwa muda mrefu wamejenga imani na watu wao, lakini sisi bado Tanzania vyombo vyetu vya fedha havijachangamkia kuwawezesha Watanzania kuweza kuwekeza na hili ndiyo tatizo kubwa tulilonalo. Kwa hiyo, tutakuwa na tatizo la pili ukiacha la ardhi la kwamba, tuna wawekezaji wengi kutoka sehemu moja, lakini wawekezaji kutoka sehemu nyingine hawaonekani na hiyo nayo italeta *conflict* mbele ya safari.

Kwa hiyo, ni vizuri nalo tukali-*address* vilevile; tunawawezeshaje Watanzania ukiacha haya mashirika kama NSSF na kadhalika. Tunawawezeshaje Watanzania na wao waweze kwenda kuwekeza katika sehemu nyingine za Afrika Mashariki. Nafikiri hilo hatujalifanya vizuri na ningeomba nalo tulifanye vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuanzisha mfumo mpya huu wa Afrika Mashariki, tulikuwa nayo ile *East African Community* ya zamani, ambapo tulikuwa na Tanzania, Kenya, Uganda na Zanzibar. Sasa ukiangalia hii miradi yetu ya ushirikiano ni rahisi sana kuunganisha barabara kutoka Kenya kwenda Tanzania au Kenya, Uganda na kadhalika. Mradi kutoka Bara au Kenya kuupeleka Zanzibar, kwa sababu kuna bahati katikati *is a problem.* Waziri amesema vizuri kwamba, Zanzibar wanashiriki kwenye vikao na kadhalika. Hivi *link* gani iliyoko ya kiuchumi inayofanyika Zanzibar hatujaiona na hii *East Africa?* Hili ni tatizo lingine la msingi kwamba, kweli tunashiriki kwenye vikao na tunakwenda kwenye vikao, lakini bahati mbaya miradi inayobuniwa bado haijaweza kuwaletea manufaa na kuiona Zanzibar kama inafaidika. Kwa mfano, kuna mradi wa umeme na kadhalika, bado kama CMCC waliotusaidia East Africa yenyewe haijafanya kitu chochote. Mimi nafikiri haya ni mambo yanayotakiwa kuangaliwa vilevile.

Vilevile na sisi Tanzania tuna *opportunity* tunaziacha, kwa mfumo ambao tungependekeza kuufanya, tungeweza kuwa na Wabunge tisa kutoka Bara na tisa kutoka Zanzibar, kwa mfumo ule wa zamani wa *East African Community.* Kwa maana hiyo, tungekuwa na Wanachama wengi zaidi na tungeweza kuwa hata na uongozi katika shirika hili kwa wingi zaidi. Tumeiacha hiyo *privilege* na hatujui ni kwa sababu gani. *East African Community* iliyokuwepo zamani, pamoja na kwamba tulikuwa kwenye Muungano, lakini bado nchi hizi zote zilikuwa ndani ya *East African Community*. Kwa hiyo, nafikiri nalo hili linahitaji kuangaliwa tena, liangaliwe ni namna gani Zanzibar inaweza kushiriki kikamilifu kama ambavyo ilikuwa ikishiriki huko nyuma.

Nakubaliana sana na Mheshimiwa Joseph Mungai kwamba, katika hali halisi ya sasa, Mashirika mengi haya ya Ndege kufanya kazi ni kazi ngumu sana. *Competition* ya *Air Line Industry* ni kubwa sana, inahitaji *massive investment.* Leo naona kwenye bajeti mwaka huu tumeipa Air Tanzania 1.5 billion kwani 1.5 billion ifanye nini; ni kama kutania tu.

Kwa hiyo, nasema kuna haja ya kuangalia hasa ni maeneo gani tunaweza kushirikiana kiuchumi, ambayo kama Jumuiya ya Afrika Mashariki tuweze ku-*benefit* kwa pamoja. Tukiyafanya hayo, nafikiri tunaweza kufika mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la *tarrif* ambazo zinamalizika 2010; napata mashaka kwamba, kweli tuna bidhaa ambazo tunaweza kuuza. Ukiangalia bidhaa tunazouza nje; chumvi na kadhalika, siyo zile bidhaa hasa ambazo wenzetu wa Kenya wanatuuzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo tofauti kubwa sana, wao wana *industrial products* nyingi, sisi bahati nzuri tuna ardhi na chakula kidogo na kadhalika. Hata Kenya wanaagiza mchele si chini ya tani laki tatu kutoka Pakistan, pamoja na kwamba, sisi Tanzania tunazalisha mchele, lakini wao wanaagiza mchele kutoka Pakistan kutokana na makubaliano ambayo yapo na hili ni jambo ambalo nafikiri ni vizuri tukaliangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama kuna bidhaa wenzetu bado wanaagiza nje na ambazo zinazalishwa *East Africa* hii na sisi bado hatujajipanga kuingia katika soko hilo, maana yake hata chakula chetu sisi wenyewe hatuna na mwaka 2010 tutakuwa na *zero tariff* tutafaidika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ndio wasiwasi wangu mkubwa tu na naomba hapa Waziri atusaidie sana, kama kweli sisi tutafaidika na *zero tariff* baadae wakati uzalishaji wetu bado ni duni. Haidhuru wakati mwingine nikubaliane tu kwamba, ukiwakusanya watu ambao wana taahira ya aina fulani mnaweza msifike pahali, lakini ukiwachanganya watu waliokuwa kidogo na na akili nzuri zaidi mnapiga hatua. Inawezekana kuchanganyikana kwetu na sisi tunaweza tukachangamka, tukabadilika, inawezekana kabisa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini inawezekana vilevile hali ikawa mbaya zaidi, kwa hiyo, yote mawili tuyatazame. Kwa hiyo, suala la kuelimisha watu wetu ni la muhimu sana, tuwape watu elimu ya kutosha, tuwape rasilimali za kutosha ili tuwawezeshe kuingia kwenye ushindani, vingenevyo mimi ninadhani tunaweza kupata *social crisis* baada ya safari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuta *South Africa* pale pamoja na uchumi wao mzuri wamelalamika kwamba, wageni walioko pale wanafaidi zaidi kuliko wao. Yametokea hayo, hata mauaji yametokea na pahali pengine pengi. Juzi tumeona Australia wanapambana na Wahindi wanaosoma pale, tumeyakuta hayo. Kwa hiyo, nasema haya yatatokea kama hatukujiandaa vizuri kama nchi na ndio maana nikasema ile *process* nzima ya *democratization* ikienda vizuri, inawezekana ikatuondolea matatizo tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa ni suala zima la migogoro. Nashukuru wenzetu wa Rwanda wametulia sasa na Burundi wanajitahidi lakini hata sisi Tanzania hatujakuwa vizuri, lile doa dogo lipo bado hatujalirekebisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hili kwa nia safi kabisa. Kama leo una wapiga kura 100,000, katika uchaguzi wanakataliwa kujiandikisha, tayari unaashiria mgogoro kesho kutwa. Kwa hiyo, vile viashiria vya migogoro kama hatukujitahidi kuviondoa sisi wenyewe na sisi bahati nzuri tumekuwa wapatanishi wakubwa, mimi nafikiri bado hatujajenga utaratibu mzuri wa kulisaidia Taifa kuingia pahali pazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri haya tungekuwa tunaya-*address* vizuri yangeweza kutusaidia. Tumeona Roliondo, akina mama wanalalamika wanasema wamebakwa. Nilikuwa nazungumza na Waziri Mkuu hapa, nikamwambia ni vizuri tukalifuatilia tukapata uhakika wa *statements* zile.

Sasa matatizo kama haya ni vizuri tukaanza kuya-*address* mapema, namna gani tunayakabili matatizo au migogoro yetu tuliyonayo ndani ili tunapoingia katika Jumuiya ya pamoja, tusije tukaambukizana matatizo juu ya matatizo. Ndiyo maana tunawataka wenzetu wa Rwanda na Burundi wajitahidi kutatua matatizo yao, lakini na sisi Tanzania lazima tuweke maslahi yetu mbele, tutatue matatizo tuliyonayo, tuwape haki raia wetu, tuwape haki wanazostahili za kimsingi za kikatiba ili waweze kufanya kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana na ninaiunga mkono hii hoja. (*Makofi*)

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Afrika Mashariki. Kwanza, nimpongeze yeye mwenyewe binafsi, pamoja na Naibu wake na Katibu Mkuu na Wataalamu wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja katika mchango wangu. Kwanza, nianze mchango wangu na suala la ardhi, ambayo ndiyo inayotuunganisha nchi hizi za Afrika Mashariki. Ardhi hii kama walivyotangulia wenzangu kusema kwamba, ndio rasilimali nzuri za wananchi wetu na kila nchi ina sheria zake za ardhi. Sheria zetu za ardhi zimetoa kipaumbele kwa Wananchi wa Tanzania kumiliki ardhi yao na tumeweka taratibu mbalimbali, juu ya utaratibu wa kila mwananchi kumiliki ardhi yake, kwa sababu ndiyo rasilimali tuliyokuwa nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vigumu kusema kwamba, aje mtu yeyote kumiliki ardhi yetu. Nina hakika baada ya miaka 10 au 15, ardhi yetu wenyewe haitatutosha. Tukubali miaka 20 iliyopita siyo ya sasa, idadi ya watu imeongezeka, lakini baadae watoto wetu na wajukuu watakuja kutuhukumu vibaya sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashukuru kwamba, vijana wetu wengine wapo hapa ndani wanatoka sasa hivi, wanasikiliza dibaji za umuhimu wa ardhi. Leo ni sisi, lakini kesho ni wao na keshokutwa ni watoto wao; huku kuendelea kumiliki ardhi hakuishi. Mimi nikubali kwamba, Serikali imeweka utaratibu mzuri tu, mgeni atamiliki vipi ardhi na Mtanzania atamiliki vipi ardhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema bado Serikali ina changamoto ya kuhakikisha kwamba, tunaweka, tunafuatilia au tunatekeleza utaratibu wa MKURABITA wa jinsi kila Mtanzania anavyostahili kumiliki ardhi na hasa utaratibu wa kumiliki ardhi kwa utaratibu wa Kimila kule vijijini. Itarahisisha zaidi umilikaji wa ardhi kwa wananchi wengi wa Tanzania wanaotaka kumiliki ardhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitoe wito kwa Watanzania kwamba ni lazima kila Mtanzania amiliki ardhi. Nitashangaa Mtanzania wewe hutaki kumiliki ardhi, unataka ufanye nini? Kama hutaki wewe leo, muwekee akiba mtoto wako na mjukuu wako, itakuja kuwasaidia baadae. Hakikisha kwamba, unafanya *process* zako za kumiliki ardhi na hati inabaki kwa kila atakayekuja nyuma yako, baada ya wewe kuondoka anajua kwamba, aidha babu au baba ametuwekea rasilimali ambayo tunaweza kujivunia katika familia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iharakishe utaratibu wa umilikaji wa ardhi kwa Watanzania wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Afrika Mashariki, miradi ya maendeleo ndiyo itakayoweza kutukwamua kiuchumi vilevile. Kuna mambo mengi, Tanzania ina uhaba wa umeme, Kenya kuna uhaba wa umeme, Uganda kuna uhaba wa umeme, lakini tuna vyanzo mbalimbali vya kuweza kutusaidia sisi wenyewe na hatimaye na ziada tukawapa majirani zetu kwa kuwauzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano wa mradi wa umeme wa *Stigglers' Gorge,* ambao tumeukalia kwa muda mrefu sana na Wataalamu wa Tanzania ambao wamebuni mradi ule mpaka leo wako hai; wakati ule mradi ule ulikuwa unagharimu Serikali dola Milioni 500, lakini sasa tufike pahali tukubaliane kwamba, Serikali haiwezi ikatengeneza miradi yake kwa fedha zake yenyewe. Lazima tuingie sasa katika utaratibu wa uwekezaji, mpe muwekezaji ajenge *Stigglers' Gorge;* tunapoteza nini? *Stigglers' Gorge* itabaki Tanzania, maji yale yatabaki Tanzania, tutatumia kwa kuzalisha umeme, tutaweza kudhibiti mafuriko na kuweza kuwa na mipango mizuri ya kilimo cha umwagiliaji. Hilo ni kwa upande wa Rufiji na maeneo mengine mengi tu na tuendelee kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vikwazo vingi vinakuja kutokana na mashinikizo kwamba, mradi ule utakuwa hauna manufaa kwa sababu utaharibu mazingira. Hauharibu maeneo mengine, utakuja kuharibu pale? Mchina ndiye mwenye *Dam* kubwa sana duniani, inahifadhi maji kilomita kwa kilomita, lakini wanazalisha umeme wanajitosheleza. Sisi tuna uhaba wa umeme, lakini tuna *Stigglers' Gorge,* sio lazima Serikali iingize pesa za kujenga mradi ule, hawataweza. Tuwape wawekezaji, tukubaliane tu kuwa watauza umeme ule kwa bei nafuu. Watakaonufaika ni wananchi, tutakuwa na viwanda vingi kwa sababu *tariff* ya umeme itakuwa imepungua, uzalishaji utakuwa umeongezeka, watu wetu watapata ajira na hatimaye tutaweza kufanya ushindani ndani ya *East Africa* kwa kuuziana bidhaa.

Mheshimimiwa Mwenyekiti, leo tunashindwa ku-*compete* na Kenya kwa sababu ya *tariff* ya umeme tu, sisi bado tuko juu. Sasa hili liwe ni changamoto kwa Wizara hii ya

Afrika Mashariki katika kuhakikisha kwamba, tunaweka haya mambo ya umeme kwa maana ya uwekezaji na kubwa zaidi kuwapatia ajira wananchi wetu na kuweza kuzalisha bidhaa nyingi na za ubora lakini tupate umeme wa bei nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni la miundombinu. Nashukuru katika taarifa ya Waziri, amezungumzia barabara za *East Africa.* Mimi nizungumzie barabara ambayo inanigusa moja kwa moja, lakini ningependa Mheshimiwa Waziri, unapoizungumzia barabara ambayo wewe umeiandika Tanga – Sadani – Bagamoyo, kwa nini haiwi Tanga – Pangani – Bagamoyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sadani iko Bagamoyo, Sadani iko Pangani lakini Tanga ni Wilaya, Pangani ni Wilaya na Bagamoyo ni Wilaya, basi hebu fanya haya marekebisho ili iweze ku-*sound* vizuri kwamba, barabara hii inatoka Wilaya ya Tanga inapita Wilaya ya Pangani inaingia Wilaya ya Bagamoyo. Sadani siyo Wilaya, Sadani ni eneo ambalo sasa hivi ni hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na barabara hii, labda niulize maswali mawili, matatu; tumezungumza muda mrefu fedha zimetolewa kuifanyia upembuzi yakinifu, upembuzi umekamilika na hivi sasa tunategemea Serikali itatafuta fedha Afrika Mashariki ama Wizara yako Mheshimiwa Waziri itatafuta fedha ya kuanza utaratibu wa ujenzi. Mimi nataka kujua utaratibu ukoje, mipango ikoje, pamoja na kwamba, tunajua tuna barabara nyingi; tunayo Iringa - Dodoma, tunayo Dodoma – Babati, zote hizi ni Barabara za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema tujue tunakwenda vipi, kwa sababu sasa hivi walipokuwa wananchi wanaona wale wataalamu wanaipima ile barabara wakaanza kujiuliza, hasa wale waliokuwepo barabarani. Lazima tuwaweke wananchi wetu katika hali ya tahadhari na kujua kwamba, hii barabara inakuja, kwa hiyo msibweteke mkaja mkashtukiziwa tu kwamba, mnatakiwa muondoke. Anzeni mipango yenu sasa hivi ya jinsi ya kuhama katika maeneo ya hifadhi ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawahamasisha wananchi na wanaelewa hilo, wasije wakaambiwa mnaondoka halafu fidia itakayolipwa inakukuta hujajiandaa; huna nyumba ambayo ulijenga mapema ili uweze kuhama mapema usije ukawa unabughudhiwa na ujenzi wa ile barabara. Kwa hiyo, hizo kazi sisi tunazifanya na tunaiomba Wizara iharakishe tujue kwamba, mipango ya ujenzi wa barabara hii itakuwaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile tunawahamasisha wasiuze ardhi zao, kwa sababu sasa barabara hii ya Tanga -Bagamoyo kupitia Pangani imeshakuwa ni kitega uchumi kizuri kwa watu ambao wanaelewa mapema kwamba, hapa patapita barabara, kuna umeme, kuna maji, kuna shule ni mahala pazuri pa kuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatukatai kwamba, watu wasije kuishi lakini tunahamasisha nao wao wananchi wasiuze ardhi zao ovyo ovyo. Ardhi za *beach* zote zimekwishauzwa kwa sababu ya kupewa kitu kidogo, hawajaona fedha, wanaziona nyingi. Vilevile barabara hizi pia zijengwe kwa utaratibu wa uwekezaji. Serikali haina

pesa za kujenga hizi barabara na zikijengwa kwa utaratibu wa uwekezaji, basi tozeni ushuru wa barabara ili kurudisha gharama haraka na hatimaye kupata unafuu wa gharama za mradi na hatimaye wananchi waendelee kufaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile tuna reli ambayo tunaizungumzia ya kutoka Tanga – Arusha – Musoma. Hii ni *project* muhimu sana kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Tuna *soda ash* kule inatakiwa itolewe, *demand* ni kubwa katika dunia hii; tatizo letu ni ujenzi wa reli, mradi huu pia wapewe wawekezaji wajenge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na reli hiyo, hatuna budi kujenga bandari ambayo Serikali imekwishafanya utaratibu mzima kabisa wa kuipima Bandari ya Mwambani pale Tanga, kwa sababu ya kina chake na hatimaye iweze kufanya kazi. Bandari hizi pia zinajengwa kwa utaratibu wa uwekezeji; tukitaka kila kitu tupange sisi wenyewe, hatutaweza na hakuna miradi itakayotekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Bandari ya Mombasa pale Kenya ime-*invest* fedha nyingi kweli kweli kwa ajili ya kuboresha ile bandari, kwa sababu wamekwishaona tunakokwenda. Sisi bado tunasuasua kwa sababu labda ya kufikiria tutapata wapi pesa. Pesa ni uwekezaji na watu wa kuwekeza nina hakika wapo na ninyi mnawajua, hebu ongezeni *speed* ili waje wawekeze katika vitega uchumi kama hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yangu yalikuwa ni haya machache, ambayo nilitaka kuzungumzia kwamba, tuharakishe miradi katika *East Africa*, ambayo itaweza kuwanufaisha kwa njia moja au nyingine, Wananchi wa Tanzania na hatimaye sisi tuweze kuendelea. Tuna *advantage* kubwa na nchi jirani wanatushangaa jinsi tunavyochelewa na mambo haya. Ingekuwa wao ndio wako hapa, sasa hivi wangekuwa wako mbali sana. Sasa sijui tofauti ni nini kati yetu sisi na wao? Hakuna tofauti, tunazungumza lugha moja, nchi zetu zinafanana, wananchi ni walewale na lugha ni hiyo hiyo moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niipongeze tena hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri na niunge mkono hoja mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hoja iliyo mbele ya Bunge lako Tukufu, kuhusu Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Naunga mkono hoja na ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri, mjukuu wangu, kwa kazi nzuri anayoifanya na sisi tunaona fahari kuwa na mjukuu kama yeye. (*Makofi*/*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza mdogo wangu, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na wafanyakazi wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kutetea na kulinda maslahi ya Taifa letu katika Jumuiya hii; Mungu awabariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Wizara hii ni kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Uanzishaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Itifaki zake.

Wananchi wa Wilaya za Rorya na Tarime, wanataka kujua jinsi gani Wizara hii ilivyojipanga kushughulikia tatizo sugu la wizi wa ng'ombe mpakani, hususan katika Wilaya za Rorya na Tarime.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu shughuli ya Wizara hii ni kukabiliana na wizi wa mpakani, yaani *cross border crime* kupitia Mkakati wa Amani na Usalama wa Jumuiya, ambao uliidhinishwa na nchi wanachama mwaka 2005. Hii ni kazi ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa maeneo yaliyoidhinishwa ni kuanzisha mfumo wa kuendesha operesheni za pamoja, kupambana na wizi wa ng'ombe na kutekeleza mradi wa kudhibiti kuzagaa kwa silaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia mwaka 2006 hadi 2009, zaidi ya ng'ombe 3500 wa Wananchi wa Wilaya ya Rorya, wameporwa na majambazi, maharamia, kutoka nchi jirani wakitumia silaha za kijeshi aina ya AK-47 na LMG na wananchi 40 wamepoteza maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Tarime peke yake, ng'ombe 5000 wameporwa na Wilaya ya Serengeti ni ng'ombe 2500; jumla ni zaidi ya ng'ombe 10,000 wamevuka mipaka yetu. Huu sio wizi, huu ni uvamizi, mtu anakuja bila kukaribishwa, anavuka mpaka bila kanuni au waraka au hati za kusafiria, anabeba silaha nzito nzito na vibaya zaidi ni kwamba, wanatoa taarifa mapema kwamba, tutakuja saa fulani na wanakuja. Sasa ninapozungumzia suala hili, wengine wanasema ooh! wanataka kupeleka Jeshi na Polisi kukabiliana na mapigano ya koo na kikabila. Si sahihi! Sisi matatizo yetu ni ya ndani, mimi na Mheshimiwa Charles Mwera ni ndugu hatugombani, hawa waharifu ndio wanataka kutuvuruga ili kupotosha malengo yao kwamba, kuna tatizo la mapigano ya koo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Celina Kombani, amemaliza tatizo hili. Alikutanisha koo zote mbili, wamepatana na tangu wakati huo hatujasikia wanapigana. Tatizo hili ni ujambazi na wamesema wakishamaliza ng'ombe wote Wilaya za Tarime, Rorya na Serengeti, wataelekea Bariadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wamewaona na wanasema mbona hawa ni Wasomali, tena vijana wadogo wadogo lakini wana bunduki za kisasa? Wamefika katika sehemu moja Wilaya ya Tarime wakakuta watu wanalima na ng'ombe, wakawaamuru wawafungue ng'ombe wao wakawachukua hivi hivi! Hivi nchi hii mipaka yetu haina wenyewe? Hii ndiyo Tanzania iliyokomboa Bara la Afrika mbona tunachezewa hivi? *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nampongeza sana Amiri Jeshi Mkuu na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kukubali kuundwa kwa Kanda Maalumu ya Polisi Mkoa na kuanzisha Kikosi Maalum. Mipaka ya nchi yetu na nchi jirani inalindwa kweli kweli. Tunapofuatilia ng'ombe hawa walioibiwa baada ya kuvuka mpaka

hawaturuhusu. Ng'ombe wakishafika wanasafirishwa kwa malori, sasa huu ni uvamizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninashangaa watu wanaosema kwamba, waliona Wakurya wanapigana, sasa mbona hata Wahaya kwa Wahaya wanapigana? Wanagombana, mnagombana ndiyo. Ugomvi wa nyumbani ni ugomvi wa kawaida, lakini hili suala limevuka mipaka. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa shughuli za kuanzishwa kwa Mkakati huu wa Amani na Usalama, ilikuwa ni kuanzisha Mfumo wa Kuendesha Oparesheni za pamoja kupambana na wizi wa ng'ombe na kutekeleza Mradi wa Kudhibiti Kuzagaa kwa Silaha. Kazi hiyo ni ya Wizara hii na mimi naomba suala hili lijadiliwe katika Bunge la Afrika Mashariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa majambazi walifanya kufuru ya Karne. Mheshimiwa Waziri Mkuu, alifika katika Kata ya Mirare, Kijiji cha Nanguge, kuwapa pole wananchi ambao walipata msukosuko huo na kuuawa;, lakini baada ya mkutano huo majambazi walipiga simu kwamba, tutakuja tena na walikuja wakaiba ng'ombe 70 katika Kijiji cha Nyambogo. Safari hii vijana wa Said Mwema walipambana nao kweli kweli na walirejesha ng'ombe na waliponipigia simu nikawauliza kama wamewapata; walisema wamepotea. Sasa mimi lugha ya kupotea sijui maana yake nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwizi ni mwizi. Mwizi hana kabila, hana koo, hana ndugu na hana taifa, anaweza kuua ndugu yake. Sasa tatizo hili lichukuliwe kama tatizo la kimataifa. Wananchi wa Wilaya ya Rorya, Wananchi wa Wilaya ya Tarime na Serengeti, tunapambana na wezi, wanyang'anyi, wavamizi. Hawa watu ni hatari, tulicheza hivi hivi mpaka Idd Amini akatuathiri, huku tukisema huyu hawezi lolote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi nina imani kuwa, tumejipanga vizuri, tumejipanga kulinda mipaka yetu ndani ya nchi yetu. Sasa nje ya nchi yetu, Mheshimiwa Kamala na mdogo wangu Aboud, nimewaachia na Katibu Mkuu Mtendaji yuko pale. Suala hili lichukuliwe kama tatizo la Turkana. Hatuwezi kukubali, watu wamebaki maskini wa kutupwa, wamejua benki ya wananchi wa Wilaya za Tarime, Serengeti na Rorya ni, ng'ombe na ndio maana siku moja nilisema Serikali ikishindwa sisi tutavuka mpaka hata kama ni kufa acha tufe. Ninafarijika kwamba, Serikali imeitikia na imejali wananchi sasa itaimarisha ulinzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hayo niliyoyasema, ninapendekeza yafuatayo: Kwanza, tatizo la Tarime, Rorya na Serengeti Mkoa wa Mara, kwa kuwa limevuka mipaka yetu sasa lishughulikiwe kama tatizo ambalo liko nje ya mipaka yetu kwa kufanya yafuatayo:-

Kwanza, Jumuiya ya Afrika Mashariki kupitia Bunge la Afrika Mashariki na baadhi ya Wabunge tuliowachagua kwenda kutuwakilisha mko kule, lichukueni hili suala kama ajenda na mlijadili haraka na kulitafutia ufumbuzi wa kudumu.

Pili, Mawaziri wenye dhamana ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kwa pamoja walishughulikie tatizo hili haraka. Watembelee maeneo hayo yaliyoathirika, wazungumze na wananchi, maana tatizo letu ni kwamba, ndugu zetu wa upande ule hawataki kushirikiana na sisi. Walipokuwa wanatumia silaha za kijadi, wasingeweza hata siku moja kuthubutu kufika pale Tarime au Rorya. Mheshimiwa Mwera, anafahamu hilo, sasa kwa kuwa hatuna silaha za kisasa, wanatumaliza na ng'ombe hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mawaziri wahoji, wafanye tathmini kwa nini ndugu zetu wa upande mwingine hawataki kushirikiana na sisi mara ng'ombe wakivuka mpaka; kulikoni?

Tatu, Serikali za Tanzania na Kenya, zianzishe mfumo wa kuendesha operesheni za pamoja ili kuimarisha mawasiliano baina ya viongozi wa vyombo vya usalama na ulinzi, kutembeleana ili kubadilishana ujuzi na uzoefu wa namna ya kupambana na wizi wa ng'ombe na kudhibiti silaha za kijeshi.

Nne**,** Tanzania iimarishe ulinzi wa mipaka yake na Kenya. Kazi hii ifanywe na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), jeshi haliendi kule kutawala, mbona upande mwingine jamani wapo? Ukienda kilomita chache tu wapo na ndio wenye dhamana ya kulinda mipaka yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Wananchi wa Wilaya Rorya na nina hakika ni pamoja na wale wa Wilaya za Tarime na Serengeti, wanawapongeza sana Mheshimiwa Rais, ambaye ndiye Amiri Jeshi Mkuu, Waziri Mkuu, Mawaziri wenye dhamana ya Ulinzi na Usalama na Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama, kwa hatua walizozichukua za haraka ili kuimarisha ulinzi katika Wilaya za Tarime na Rorya.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** kwa kuwa nchi jirani wameshindwa kudhibiti wizi huu wa kuwaruhusu wavamizi kutoka nchi yao na kuvusha ng'ombe kule; wananchi wanaomba ufanywe mpango wa kurejesha ng'ombe wetu 3500, ikishindikana tulipwe fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi sisi kila siku kuwa waungwana tu, hatujaiba hata kuku mmoja kutoka upande mwingine, kwani kama tukiruhusiwa kuiba kila mtu anajua kuiba. Waliopoteza maisha, wazazi wao pia wafidiwe ama wapatiwe kifuta machozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalo gazeti hapa ambalo baadaye nitakupa, kuonesha jinsi silaha kali za kijeshi zinavyotumika katika kupora ng'ombe na kuua wananchi wetu kutoka nchi jirani. Mimi nina imani, sisi Watanzania ni wapole sana; tuna uwezo mkubwa, tumeweza kulikomboa Bara hili la Afrika, tulipambana na mataifa makubwa kama Wareno, Afrika Kusini na Wakoloni wote, sasa sisi siyo kupambana na Kenya, tunataka tuimarishe ulinzi wa mipaka yetu na mali zetu zilizoporwa zirejeshwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa, nataka nitamke kwamba, Wananchi wa Wilaya za Rorya, Tarime na Serengeti, hawana rasilimali, walikuwa

wanategemea ng’ombe na kwa kuwa ng’ombe wameisha, wananchi hao sasa hawawezi kulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na ninarudia tena kwamba, ninaunga hoja hii mkono. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante sana Mheshimiwa Philemon Sarungi, Mbunge wa Rorya, kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, mchango wa Mheshimiwa Prof. Sarungi, unatuhitimishia wachangiaji ambao wameomba kuchangia. Kwa maana hiyo, muda tulionao ningeweza kumwita Naibu Waziri ili waanze kujibu hoja mbalimbali ambazo zimechangiwa, lakini nitawapa muda kwa sababu wana watendaji wao hapa, waweze kwenda kukaa na kuweza kubadilishana mawazo na hatimaye tutakapokuja saa kumi na moja, tutaanza na Naibu Waziri na hatimaye mtoa hoja atakuja kuhitimisha hoja yake hapa na tutaweza kumalizia.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa muda bado tunao, lakini wachangiaji wamemalizika, napenda kuchukua nafasi hii, kusitisha shughuli za Bunge mpaka jioni saa kumi na moja kamili.

(*Saa 6.30 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate ufafanuzi makini: Je, Wizara hii ina mikakati gani ya kina ya kulinda na kutumia ardhi yetu hasa ambayo ipo mipakani Kagera na Kilimanjaro ambapo mipaka yetu imekaa vibaya sana? Hatuna ulinzi wa kutosha, mimi nimeshazunguka mipaka yetu Watanzania tunajivunia mali zetu.

Lakini bila ulinzi ni sawasawa na hakuna. Naomba kujua pamoja na ardhi yetu hasa Wakuu wa Mikoa kujirithisha kujidai wanawekeza mfano unao wewe Waziri, Wilaya ya Misenyi sasa hivi Wakuu wa Mkoa wanaona ni sehemu ya kupumzikia. Tunakataa kuingiza wageni: Je, wakipitia kwa viongozi hao tutajuaje? Huyu mwekezaji wa Bubale alishirikisha wananchi au alipitia kwa viongozi hao atuadhiri baadaye kwa wananchi wetu wenyewe wameshaondoka wananchi wetu wanabaki na mateso kama yaliyoko Bubale Kakunyu.

Naomba kupata ufafanuzi kama Wizara hii kwa wananchi wetu hasa wakulima Wizara hii ina mikakati gani kutafutia soko la mazao yetu ukilinganisha na umasikini kwa wakulima hao hasa wa Kahawa, zao ambalo limekua sugu. Unakuta Waganda wananunua kwa kujificha, wengine wanauawa, ni mikakati gani ya kuwasaidia? Hiyo ni

pamoja na mazao mengine kama ndizi, maharagwe, karanga na matunda. Wenzetu Waganda wanapeleka Entebe. Naomba ufafanuzi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uimarishaji wa mipaka ni hafifu sana, Serikali inatusaidiaje kuimarisha maaskari kama hawatoshi? Je, kuna mikakati gani ya kuajiri maaskari kudhibiti mipaka yetu ili tuondokane na shida hiyo ya Wasomali wanaoingia mara kwa mara ili kupunguza madhara kwa wananchi walioko mipakani baada ya kufaidika na mipaka yao? Hayo yote niliyoyauliza yananikera sana, tena sana pamoja na Waziri mwenye dhamana. Nchi yetu ina rasilimali nyingi sana, Wizara hii ina mikakati gani kwenye rasilimali hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namtakia Mheshimiwa Waziri bajeti njema. Mungu awe naye. Amina.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Mjukuu wangu, Naibu Waziri, Mdogo wangu, Katibu Mkuu na Wafanyakazi wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya katika kutetea na kulinda maslahi ya Taifa letu katika Jumuiya hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, napenda kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri katika maeneo yafuatayo:-

Kuhusu soko la pamoja la Afrika Mashariki, nashauri maslahi ya Tanzania ipewe kipaumbele. Hali ilivyo sasa, masoko ya mipakani yanatumiwa na wafanyabiashara wasio waaminifu kuvusha bidhaa na rasilimali zetu nje ya mipaka yetu. Ningependa kufahamishwa kama katika kuandaa mkakati wa kitaifa wa utekelezaji wa itifaki hii, Wilaya ya Rorya iliyo mpakani, katika Kata ya Bukara kijiji cha Kirongwe itajengwa soko la Kimataifa kama alivyosema Mheshimiwa Waziri alipotembelea eneo hilo mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2008 ujumbe wa *EAC* ukijumuisha wadau Mawaziri wenye dhamana ya masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ulitembelea Jamhuri ya watu wa China. Katika ziara hiyo China ilikubali kusaidia katika kuboresha Miundombinu ya barabara pamoja na nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la ziara hii China lilikuwa ni kuboresha barabara zinazoziunga nchi wanachama. Naomba kupata majibu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, kama barabara za Wilaya ya Rorya zinazounganisha nchi yetu na nchi jirani zitaingizwa katika mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Rorya, nawapongeza sana viongozi wa Wizara hii na wafanyakazi wote kwa kazi nzuri wanazofanya kwa kutanguliza maslahi ya Taifa.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ninapenda nichangie machache katika Wizara hii muhimu.

Katika nchi zetu za *EA* lipo tatizo kubwa la uhalifu na hasa sisi wakazi wa Mkoa wa Kigoma ni kati ya maeneo yaliyoathirika sana na vitendo vya uhalifu.

Mwaka jana mwishoni, Mji wa Kasulu ulivamiwa na majambazi waliodhaniwa kutoka nchi jirani ya Burundi na Rwanda. Majambazi haya yalikimbia na kwenda kujificha nchi hizo jirani na imekuwa tatizo kuwarejesha nchini ili wafikishwe Mahakamani.

Je, ni kwanini katika nchi za *EA* hakuna *protocal* ya kubadilishana wahalifu? Kama ndiyo, ni lini *protocal* hiyo italetwa Bungeni ili kuridhiwa na Bunge?

Ninafahamu moja ya maeneo *'interesting'* katika mahusiano ya nchi za *EA* ni Biashara. Je, Wizara ina mkakati gani endelevu kushirikiana na Wizara ya Biashara na Viwanda ili *promotion* ya biashara ndogo hasa zile za mpakani ziweze kukua na wafanyabiashara wetu wafahamu fursa zilizopo katika nchi za *EA*? Mfano, *Boarder Trade Promotion* katika mipaka ya Mkoa wa Kigoma na Burundi/*Congo DRC*.

Nchi karibu zote ukiacha nchi yetu ya Tanzania zina siasa tete na kwa kiasi kikubwa tabia za kibabe na udikiteta zinashamiri sana katika nchi hizo. Je, katika fungamano la Afrika ya Mashariki ni mkakati gani uliopo wa kuheshimu Utawala wa Kidemokrasia ili hatimaye mipango inavyopangwa iweze kutekelezwa bila kutia mashaka? Bila *Democracy* ya kweli sioni jinsi ya kufikia shirikisho la *EA* na bila *true Democracy* sioni *future* ya *EA federation*. Ni lini itawekwa *'Democratic Code'* ili nchi hizi ziheshimu kweli matakwa ya watu wao?

Nchi ya Somalia sasa haina Serikali yenye nguvu na matatizo ya kisiasa na kiulinzi ni mengi. Hata hivyo, Somalia ni jirani na nchi zetu za *EA*. Ni mkakati gani wa kisera wa nchi wanachama na zile za *IGAD* kuisaidia Somalia? Je, matatizo ya utekaji meli baharini kwenye pembe ya Afrika, nchi za *EA* zinakabili vipi hali hiyo? Kwa nini kusifanyike *a joint Military Strategy* ili kuiokoa Somalia na usalama wa nchi za *EA*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. CHARLES N. MWERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Pili, nashukuru kwa hotuba ya Waziri iliyoandaliwa vizuri kwa ushirikiano na Naibu Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki pamoja na Watendaji wote wa Wizara ya Afrika Mashariki kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizi wa mifugo umeshamiri sana katika nchi zetu za Afrika Mashariki, katika mipaka ya Tanzania, Kenya, Uganda, hali ambayo inatia mashaka, kwa namna gani tutaanza ushirikiano huo wakati kuna wezi wa mifugo ambapo majambazi/wezi wa mifugo hutumia silaha za moto kupora mifugo, ugomvi ambao hupelekea kwa uvunjaji wa amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Tarime ambayo imepakana na Wilaya ya Kurya nchini Kenya, kumekuwa na wizi wa mifugo wa mara kwa mara, wizi ambao umepelekea wananchi (Raia) wengi kuuliwa na majambazi na Ng'ombe wengi kuibwa na kupelekwa nchi jirani ya Kenya.

Watanzania wengi hasa wanaoishi mpakani katika Kata za Sirari, Nyakonga, Pemba, Mwema, Bumera, Nyamwaga, Muriba na Nyanungu, wameuliwa na ng'ombe nyingi kuporwa. Basi nashauri Serikali yetu pamoja na Serikali ya Kenya kuwa na Ulinzi wa pamoja hasa wakati wanapoanza kuwasaka majambazi yenye silaha.

Katika ushriikiano huo wa Afrika Mashariki ni vyema Serikali iwe makini katika masuala yote ya ushirikiano hasa tukifahamu kuwa nchi yetu haina viwanda vya kushindana na nchi kama Kenya yenye viwanda vingi. Sisi Tanzania hatuna viwanda na hatuna bidhaa nyingi za kuuza nje (Kenya) kulinganisha na Kenya. Kwa vile Kenya ina viwanda vingi, haikufaidika sana kwa kuanza bidhaa nyingi Tanzania.

Lugha ya Kiingereza ipewe umuhimu wa kipekee hasa tunapoingia kwenye ushirikiano huo wa Afrika Mashariki ili vijana wetu wapate ajira kwenye soko la pamoja la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

**MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalamu wote kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongelea kuhusu maji shirikishi kwa kilimo cha umwagiliaji. Katika *paragraph 63* ya hotuba ya Waziri, kwa kuwa tunavyo vyanzo vingi vya maji shirikishi vikiwemo Ziwa Victoria – Nchi za Tanzania, Kenya, Uganda; Mto Nile – Nchi za Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi; Ziwa Jipe – Kenya na Tanzania; Ziwa Challa – Kenya na Tanzania na Mito midogo midogo kama Mwiruzi na Ruguzye na mingine kadhaa ambayo vyanzo vyake vipo katika nchi jirani ya Burundi. Iko haja ya nchi zetu kuimarisha ujirani mwema kwa njia ya mazungumzo baina ya viongozi wetu katika ngazi za Wilaya na Mkoa iliyoko mipakani ili miradi ya umwagiliaji midogo midogo ijengwe kwa ushirikiano na maelewano ili hatimaye miradi yetu isiathirike pindi wenzetu katika nchi nyingine wanapoamua kutumia vyanzo hivyo vya maji.

Mfano, *DC* Kibondo amekuwa na mazungumzo ya ujirani mwema na Wilaya ya Mkoa jirani Cankuzo nchini Burundi kushirikiana (pamoja na masuala ya wakimbizi) kutafuta njia ya muafaka ya kutumia maji ya mtu Mwiruzi unaoanzia Burundi na kunufaisha kijiji cha Rumashi Wilayani Kibondo. Ziko Wilaya nyingine kama Ngara ambazo zinahusika.

Naunga mkono hoja.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalamu wa Wizara waliohusika katika kuandaa bajeti ya Wizara na kuiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu. Hata hivyo, nina mambo machache ya kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Serikali ya Kenya imekuwa ikitoa msukumo mkubwa sana wa kutaka suala la ardhi liingizwe kwenye mambo ya ushirikiano wa Afrika Mashariki. Ninavyojua mimi, mfumo wa umiliki ardhi kati ya Tanzania na Kenya na nchi nyingine ni tofauti, isingekuwa busara kulifanya suala la ardhi kuwa miongoni mwa masuala ya Muungano. Najua kwa nini Serikali ya Kenya inaweka msukumo katika suala hilo? Hata hivyo, naishukuru sana Serikali yetu kwa kupitia Wizara hii kuendelea kukataa kuliingiza suala la ardhi kwenye masuala ya Muungano. Napenda kuishauri Serikali iendelee na msimamo huo na kwa kweli umefika wakati suala hili lisiendeleee kuzungumzwa tena. Halina maslahi yoyote kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikiano kati ya nchi zinazounda Jumuiya ya Afrika Mashariki umefika hatua nzuri sana. Tumeona taasisi mbalimbali zikianzishwa kwa manufaa ya nchi hizi. Hata hivyo, jambo moja linalonisikitisha ni kuona jinsi ambavyo viongozi wa nchi hizi (wakati mwingine) wanakosa kuaminiana. Mfano hai ni mgogoro uliopo sasa hivi kati ya Kenya na Uganda. Mgogoro huu ni wa kugombea Kisiwa kidogo sana cha Migingo kilichopo ndani ya Ziwa Victoria. Mimi nimekuwa najiuliza maswali mengi sana, hivi kama viongozi wa Kenya na Uganda wanashindwa kuelewana na kukubaliana katika mambo madogo kama hayo: Je, kwenye mambo makubwa itakuaje? Je, viongozi hawa kweli wana dhamira ya kweli ya kuunda umoja wa nchi za Afrika Mashariki? Kwangu mimi naona huu ni Ushirikiano wa Mashaka.

Aidha, napenda kujua ni hatua gani zimefikiwa katika kutatua mgogoro huo? Jambo la ziada, hivi Rais Kibaki wa Kenya na Mseveni wa Uganda wanapokutana kwenye vikao na kuzungumzia mambo ya kuimarisha Jumuiya ya Afrika Mashariki, wanakuwa wanazungumza kwa dhati ya mioyo yao au ni kwa unafiki tu? Funika kombe mwanaharamu apite!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wanaounda Bunge la Afrika Mashariki huchaguliwa na Mabunge ya nchi zinazounda Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hata hivyo, baada ya kuchaguliwa hawarudi tena kwenye Mabunge yao kutoa taarifa ya kazi wanazozifanya. Husubiri kipindi chao kiishe na kisha warudi kwenye Mabunge ya nchi zao na kuomba kura. Nadhani huu siyo utaratibu mzuri hata kidogo! Napenda kushauri kama ifuatavyo:-

Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki wawe wananchi kwenye Mabunge ya nchi zao kutoa taarifa ya kazi zao kwa kipindi fulani. Yaweza kuwa mwaka mmoja au miaka miwili na nusu. Pili, mambo yote muhimu yanayojadiliwa na kupitishwa na Bunge hilo kama vile mambo yote yaliyoorodheshwa kwenye ukurasa wa 81 wa kitabu cha hotuba ya bajeti (au kiambatanisho Na. 8) yalipaswa yatumwe kwa Mabunge na Wabunge wa nchi zinazounda Jumuiya. Aidha, nashauri Wabunge wa Bunge la Afrika

Mashariki wawajibike kikamilifu kwa Mabunge yao kama vile Wabunge wa Mabunge ya nchi zinazounda Jumuiya, wanavyo wajibika kwa wananchi (majimbo) waliowachagua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano/Ushirikiano wetu ni mzuri na unaweza kuwa na manufaa endapo tu viongozi Wakuu wa Kisiasa watakuwa na utashi wa kisiasa na kiuchumi *(political & Economic will).* Nashauri kila hatua tunayoingia; tuiingie kwa tahadhari kubwa ili tusirudie yale ya mwaka 1977.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. DR. GERTRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tumejiandaaje kuzalisha bidhaa zenye ubora wa kuanzia nchi za Afrika Mashariki tusije tukawa dampo la *East Africa*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu gani umefanyika kulinda kutoroshwa kwa mali za Tanzania kwenda nchi jirani na wao kuuza nje na kunufaika na *forex,* kulinda ardhi ya Tanzania kwa sababu hili ndilo suala nyeti, kulinda soko la ajira na kuzuia wahalifu kutoka nchi moja kuingia nyingine?

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kumpongeza Waziri mwenye dhamana, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalamu kwa kuwa na uwezo wa hali ya juu kuiongoza Wizara pamoja na kuandaa hotuba nzuri kama Mheshimiwa Waziri alivyoiwasilisha. Ni kwa mantiki hii, naiunga mkono kwa asilimia zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono hoja, napenda kutoa mchango wangu katika vipengele vifuatavyo:-

(1) Kuwa na mazungumzo ya pamoja ili kuhakikisha kunakuwa na msimamo wa pamoja wa kupambana na uhalifu ambao umekuwa ukifanyika na kugundulika kuwa wahalifu huwa wanatoka nchi moja na kwenda nchi nyingine;

(2) Kuwa na msimamo wa pamoja kwa nia ya kudhibiti bidhaa kuhodhiwa na nchi nyingine kwa faida ya nchi moja;

(3) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa msimamo wa Jumuiya ni kuwa na ushirikiano wa kibiashara, nashauri kuwa na utaratibu wa kuwa na masoko ya aina hiyo kwa Mikoa ile inayopakana na nchi zilizoko kwenye Jumuiya; na

(4) Barabara zinazounganisha nchi na nchi na hata Mkoa kwa Mkoa zitengenezwe na Jumuiya.

**MHE. GEORGE MALIMA LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kukupongeza kwa hotuba yako nzuri yenye ufafanuzi wa kina kuhusu

Wizara yako.  Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.  Pamoja na kuunga mkono hoja hii naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

(1) Tanzania ni nchi mojawapo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki:  Je, imejidhatiti vipi kwa uwiano kuingia katika soko la ajira katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki?

(2) Kwa kuwa Kiswahili imekuwa lugha ya Afrika:  Je, kuna jitihada gani katika Jumuia ya Afrika yenyewe kuanza kutumia lugha ya Kiswahili kama lugha yao kwanza kwenye Mikutano, Makongamano, Warsha na kadhalika likiwemo Bunge la Afrika Mashariki?  Hii ilizifanya nchi nyingine kuiga na kuitumia lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. OMARI S. KWAANGW':** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna matatizo makubwa sana wanayopata wafanyabiashara wanaposafirisha bidhaa kabla na baada ya kufika kwenye vituo vya mipakani.  Wafanyabiashara walalamikia sana urasimu mkubwa wakati wa ukaguzi wa ubora na viwango vya bidhaa.  Tatizo lingine ni vizuizi vingi sana barabarani ambavyo vinaleta usumbufu mkubwa sana.  Jumuiya ya Afrika Mashariki isiporekebisha matatizo ya forodha, hakuna biashara ya maana na yenye tija kwa nchi zote kwa sababu wafanyabiashara wakubwa na makini wataacha kufanya biashara kutokana na usumbufu usio wa lazima.

Nashauri Serikali yetu ijenge masoko ya mazao mipakani hasa Namanga ili tuvute wafanyabiashara wa Kenya wanunue bidhaa hasa za mazao ya nafaka kama mahindi, mbaazi na maharage pale pale mpakani badala ya kuja Mikoani na Vijijini ambapo hununua mazao ya watu bado yakiwa shambani na kwa bei ya ulanguzi.

Pili, pia Serikali ione uwezekano wa kujenga mnada wa mifugo pale mpakani Namanga ili kuondoa watu kuvusha mifugo Kenya kwa njia za Panya.

Naipongeza Wizara kwa msimamo thabiti kuhusu masuala ya Ardhi na kwamba kila nchi waliamua kuwa masuala ya ardhi na makazi katika Hifadhi ya Soko la Pamoja yazingatie sheria za kila nchi mwanachama.

Hata hivyo, sasa kuna mbinu mpya zinazotumika kupora ardhi. Mbinu hizo hutumia baadhi ya watu kununua ardhi kwa niaba ya wageni kwa kutumia majina yao kwa kuwa ni wenyeji.  Jambo hili la ardhi kama msingi wa mtaji na haki ya msingi ya raia wa nchi hii linahitaji elimu ya kutosha.  Makusudi ya lazima yafanyike kuelimisha Watanzania kuhusu athari za kuuza ardhi kinyemela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaonekana Kanda 1,2,3 na 4 zina wafadhili na zinaendelea vizuri. Kanda ya tano, inayoanzia Iringa – Dodoma hadi Babati ambayo ni sehemu muhimu sana ya historia ya barabara kuu ya Kaskazini *The Great North Road* haipewi kipaumbele cha kutosha. Sehemu hii imekuwa kero kubwa na kwa kweli inachelewesha maendeleo ya kiuchumi, kitalii na kijamii katika nchi zetu.

Naomba ufafanuzi ni nini hasa wajibu wa Jumuiya kusaidia nchi yetu kupitia ufadhili ili sehemu hii ijengwe kwa kiwango cha lami.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nichukuwe nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa juhudi wanazochukuwa za kuhakikisha kwamba Jumuiya ya Afrika Mashariki inaimarika lakini pia kuweka mbele maslahi ya Watanzania pale panapoonekana kuna makinzano katika mambo fulani hususani suala la ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nitauelekeza katika mambo mawili:-

Kwanza, katika ukurasa wa 56 na 57 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri amegusia suala la miradi ya Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Miradi hii inaonekana ni marudio ya mwaka hadi mwaka, lakini wananchi wa Zanzibar wanaona kama ni kiini macho. Ahadi zimekuwa zinatolewa mara kwa mara, lakini utekelezaji wake unaishia kwenye mipango.

Tumeelezwa kwamba uwanja wa ndege wa Karume uliopo Pemba ni miongoni mwa miradi ya kipaumbele ambayo imeombewa ufadhili kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB).* Hatua hii ni ya kupongezwa kwa kuwa Wizara ya Fedha na Uchumi imeshawasilisha orodha ya miradi hiyo huko *ADB* tangu Januari mwaka huu. Ni vyema basi Wizara ikatueleza ni hatua gani imeshafikiwa hadi sasa na mradi huo unategemewa kufanya ukarabati wa jambo gani na unategemewa kuanza lini? Nimesema hivyo kwa kuiona Pemba kuwa ina kila raslimali za kuwezesha kujengwa Chuo Kikuu hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala zima la kusimamia soko la pamoja katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, ninaiomba Wizara kulisimamia ipasavyo soko la karafuu. Kama tunavyofahamu, zao la karafuu visiwani Zanzibar ni zao muhimu sana kwa uchumi wa visiwa hivyo. Hivi karibuni soko la karafuu limekuwa linayumba katika Soko la Dunia na hivyo kuathiri uchumi wa Zanzibar.

Mheshimwa Mwenyekiti, ili kulinusuru soko la karafuu kuporomoka, ninaiomba Wizara hii kuchukuwa nafasi madhubuti kuhakikisha soko la zao hili linaimarika kwa manufaa ya wananchi wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ningependa kulichangia ni suala la Elimu. Ni jambo lililo dhahiri kwamba kiwango cha elimu hapa nchini petu iko katika kiwango cha chini ukilinganisha na jirani zetu hususani Kenya. Ni wajibu wa nchi yetu sasa kuchukuwa hatua madhubuti ya kuhakikisha Vyuo Vikuu vinajengwa na kuimarishwa ili tuweze kuzalisha wasomi wengi ambao wataingia katika Soko la Ajira katika Jumuiya yetu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, ni lazima Wizara kwa kushirikiana na Wizara yenye dhamana ya Elimu kuona kwamba Vyuo Vikuu hapa nchini vinajengwa katika Mikoa mbalimbali. Kwa sababu hiyo basi, ninaiomba Wizara hii iangalie uwezekano wa kuandaa mradi wa ujenzi wa Chuo Kikuu Pemba kitakachosimamia taaluma za lugha, tamaduni na mambo ya Bahari.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, malumbano/mgogoro wa Kisiwa cha Migingo kati ya Kenya na Uganda unahatarisha amani na mustakabali mzima wa mashirikiano kati ya nchi wanachama wa Jumuia ya Afrika Mashariki. Je, ni nini msimamo wa Tanzania juu ya mgogoro huu mbaya?

Tanzania ni mwanachama muhimu pekee inayoweza kusuluhisha mgogoro huu lakini imekaa kimya. Msimamo wake ni upi na inafanya nini kusaidia kusuluhisha? Naomba maelezo. Mheshimiwa Museveni - Rais wa Uganda amekuwa kikwazo kwenye mgogoro huu kwa kutamka kuwa kisiwa cha Migingo ni cha Kenya, lakini maji yanayozunguka kisiwa hicho ni ya Uganda! Huu ni uungwana?

Tumekuwa tukisisitiza juu ya matumizi ya lugha ya Kiswahili eneo la Afrika Mashariki lakini jana tu tumeshuhudia kwenye dhifa ya Kitaifa, Maraisi – Mheshimiwa Mwai Kibaki na Mheshimiwa Jakaya Kikwete wakisoma hotuba zao kwa Kiingereza wakati wote wawili wanakifahamu Kiswahili vizuri. Napenda kujua kama itifaki inakataza lugha ya Kiswahili kutumika katika dhifa kama hizo.

Kulegalega kwa demokrasia eneo la Afrika Mashariki ni kikwazo kwa maendeleo ya nchi wanachama. Hali bado sio shwari Kenya na tumeshuhudia migongano ndani ya Serikali ya Umoja ya Rais Kibaki na Waziri Mkuu Odinga. Pia kuendelea kwa Museveni kutishia kuwa atakaa madarakani hadi atakapofikisha miaka 75, vyote vinaashiria hali ni tete eneo hili la Afrika Mashariki wakati nchi kama Ghana zinasonga mbele kwa kuzingatia mfumo wa kidemokrasia.

Napendekeza nchi zetu zianze kujenga *'institutions'* imara zaidi za uongozi na utawala bora na Mabunge yenye madaraka zaidi ikiwa ni pamoja na mfumo wa *'bicameral legislature'* kwa Mabunge yetu kupanua zaidi demokrasia. Vinginevyo, kutegemea viongozi kama Kibaki na Museveni hatuwezi kuungana kisiasa kuunda Serikali ya Shirikisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kutoa pongezi zangu kwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki - Mheshimiwa Dr. Kamala, Naibu Waziri - Mheshimiwa Mohammed Aboud, Katibu Mkuu - Dr. Stegomena Bamwenda, Naibu katibu Mkuu na Watendaji wengine kwa hotuba nzuri na kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la faraja kwamba mchakato wa mtengamano unaendelea vizuri kwa ujumla. Hata hivyo, hapana budi kuwa na tahadhari maalum ili nchi zote wanachama zipate manufaa stahiki bila kupunjana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vikwazo visivyo vya kiforodha *(NTBs)* ni miongoni mwa changamoto kubwa. Katika kutekeleza itifaki ya forodha na kujiandaa kuendea soko la pamoja ni muhimu tukawa na mikakati mahsusi dhidi ya *NTBs* na uongezaji wa wingi na ubora wa bidhaa tunazozalisha kwa ajili ya soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiwa ni pamoja na uwekezaji, elimu kwa wananchi, miundombinu bora, teknolojia sahihi, mitaji ya kutosha na hatua thabiti dhidi ya urasimu kwamishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la faraja kubwa kwamba kuhusu ardhi, makubaliano yamefikiwa kwamba Sheria za ardhi ya kila nchi mwanachama zitumike. Uamuzi huu ni mzuri na hatuna budi kutumia ipasavyo dhidi ya wananchi wetu kupewa fursa ya kuwekeza na kuendeleza ardhi yetu. Uhuru wa wananchi wa nchi wanachama pamoja na mitaji kuhama kutoka nchi moja hadi nyingine hapana, uwe na tahadhari maalum ili pasitokee nchi moja au chache zikafaidika zaidi kuliko nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uamuzi wa Arusha kuendelea kuwa Makao Makuu ya Jumuiya pamoja na kutoa fursa kubwa ya ajira kwa Watanzania unastahili kuanziwa na kuchukua hatua stahiki kufaidika ipasavyo na maamuzi haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ARCH. FUYA G. KIMBITA:** Ninawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji wengine wote hapo Wizarani kwa kutuletea hotuba nzuri. Hongereni sana.

Naomba nitoe ushauri kwenye maeneo yafuatayo:-

(i) Umiliki wa Ardhi: Ninaipongeza sana Serikali kwa msimamo wake kuhusu masuala ya ardhi lakini tunahitaji kuwa waangalifu zaidi kwani pamoja na mengine, wenzetu wanachokiwinda zaidi ni ardhi.

(ii) Ajira kwa Wananchi: Ninashauri kupitia Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara nyingine kuelimisha wananchi wetu kuhusu masuala ya ajira kutokana na ushindani uliopo.

(iii) Ushindani wa Kibiashara: Je, Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara nyingine inayo itelenjensia ya biashara? Kwani Biashara ni vita. *We need to be very smart!*

(iv) Biashara ya Maziwa: Ni kwanini kwa vikwazo vyenye kuudhi sana kwa maziwa kutoka Tanzania kuingia Kenya? Ninaomba suala hili liangaliwe kwa umakini mkubwa.
Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. BALOZI ABDI HASSAN MSHANGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki – Mheshimiwa Dr. Kamala, Naibu Waziri - Mheshimiwa Aboud, Katibu na Wataalamu wote wa Wizara hii na Taasisi zake kwa utendaji mzuri sana unaozingatia kwa dhati maslahi ya Tanzania. Naomba ufafanuzi katika maeneo yafuatayo:-

Mipaka kati ya Tanzania na nchi tunazopakana nazo hasa Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi iwekewe alama za kudumu, kubwa nyingi na za wazi ili kuepuka uwezekano wa migogoro ya nchi wanachama wa Jumuiya.

Pia vituo Rasmi vya Biashara na uhamiaji viongezwe na viboreshwe viweze kutoa huduma bora zaidi kwa wafanyabiashara na wasafiri kati ya nchi wanachama wa Jumuiya.

Lugha rasmi za Afrika Mashariki, iwekewe mikakati, miundombinu na *program* mahsusi kuwawezesha wananchi wengi zaidi hasa wasomi na wafanyabiashara kuwa fasaha katika lugha hizo rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Nampongeza Mheshimiwa Dr. Kamala - Waziri wa Umoja wa Afrika Mashariki kwa kuwasilisha vizuri hoja na msimamo wake katika kutetea nchi yetu katika suala zima la uhusiano wetu na wenzetu nchi za Afrika Mashariki. Nampongeza pia Naibu wake Mheshimiwa Aboud.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuendelea kuishauri nchi yetu iendelee kutunza heshima yake iliyokwishajijengea ya Tanzania kujulikana kama kisiwa cha Amani duniani kote. Heshima hii ni kinga na ngao yetu katika kuwezesha mafanikio makubwa kwa haya yafuatayo na mengine mengi:-

Katika mtandao wa Afrika Mashariki *(East Africa network)* kuna reli inayotarajiwa kujengwa kutoka Masaka – Bukoba – Rwanda – Burundi. Naishauri Serikali yetu itoe kipaumbele katika ujenzi wa matandao huu wa Reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania kama nchi na Kagera kama Mkoa, mtandao huu wa reli utainua kwa haraka uchumi wa nchi yetu na hasa wananchi wa Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashauri na kuwashawishi wananchi wa Kagera wachangamkie uwekaji wa mazingira bora katika kufanikisha hili na wafaidike na mtandao huu. Wanakagera changamkieni fursa hii.

Pamoja na kuipongeza Wizara katika jitihada iliyofanikisha uhakika wa upatikanaji wa umeme na kuusambaza katika miji midogo ya mpakani, na Namanga imeshapata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua inayoendelea ya kuupatia umeme mji mdogo wa Mutukula (Tanzania) katika Wilaya ya Misenyi ni ukombozi mkubwa kweli. Tanzania tulikuwa tunadhoofika ukilinganisha na mpaka wa Uganda. Nashauri kasi iongezeke na Tanzania pawake.

Aidha, nawashauri Watanzania hasa Halmashauri ya Wilaya ya Misenyi kupima viwanja mpakani kuwapa muda wa kuvijenga ili kuboresha mazingira ya mpakani mwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefarijika na vyanzo vingi vya umeme vilivyomo katika *Ziwa Victoria* vyenye uwezo wa kufikia Megawati 150. Hivi vitaokoa na kurejesha uchimbaji wa *Tin* kule Karagwe, kuharakisha machimbo ya Kabanga *Nikel* kuanza kuchimbwa. Vile vile, naamini umeme utakuwa wa gharama nafuu hali ambayo itaokoa pia mazingira yetu dhidi ya ukataji miti na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwetu sisi Kagera mradi wa mlongo – Chikagati unaotarajiwa kutekelezwa kupitia Umoja wa Afrika Mashariki, utasaidia Karagwe kupata umeme wa uhakika na gharama nafuu. Umeme huu utumike kuanzisha viwanda usiishie tu majumbani, majumba ya starehe na kusahau masuala makubwa ya kiuchumi na kijamii ambayo ndiyo malengo yetu makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iwatie moyo Watanzania kuanzisha Viwanda kwa wingi katika Mkoa wa kagera, bila kujali uchache wa watu wa Kagera, kwa ujumla kwa sababu soko sasa litategemea nchi jirani zikiwemo Uganda, Sudan, Kenya na kadhalika. Haya yatafanikiwa hivi punde, kwa sababu Rwanda na Burundi wanajiunga katika *Customs Union* kuanzia tarehe 1 Julai, 2009, hali itakayofungwa maeneo hayo kiuchumi.

Naishauri Serikali sasa iboreshe usafiri katika ziwa Victoria chini ya Wizara hii ya Umoja wa Afrika Mashariki na kuanzisha meli kubwa za usafiri wa abiria na mizigo yakiwemo mafuta ili kuboresha miundombinu ya usafiri vilevile kuziokoa barabara zetu dhidi ya mizigo mizito ambayo ingepitia majini, pia kuongeza ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iongeze Jeshi la Polisi Mikoa iliyo mipakani ili usalama wetu wa mali na raia usitetereke wakati wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. HEMED M. HEMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuamka nikiwa mzima pamoja na kuwepo usalama katika nchi yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nachukua nafasi hii kukupongeza wewe, Naibu Spika, pamoja na Wenyeviti wote kwa umahiri wenu katika kutuongoza pia kutuvumilia pale tunapowakosea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baada ya maelezo yangu hayo, sasa naomba uniruhusu kutoa mchango katika Wizara husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia hotuba ya Mheshimiwa Waziri na Naibu wake – Mheshimiwa Alhaji Mohamed Aboud, utafahamu Wizara hii ina wataalamu ambao wamebobea kitaaluma za katika nchi zetu za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia ya Serikali ni njema, ila kuna mambo muhimu ya kuyapima ili ikiwezekana kutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikiano wa Afrika Mashariki katika nchi yetu ni dhana potofu kwa Watanzania. Hii inatokana na kukosekana kwa taaluma kwa watu wote kuhusu jumuiya hii. Hivyo basi, muda uliopo ni vyema, Serikali inapaswa kuwaelimisha Watanzania kuhusu Ushirikiano huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachowazwa na Watanzania ni Ardhi. Wajibu wa nchi ni kulinda ardhi yake, nasi hatuna budi kulinda ardhi yetu kwani ardhi ndio umoja wetu wa Kitanzania. Pamoja na mashirikiano yetu isije ikatokea hilo katika jumuiya hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu soko, ni pamoja na uingilianaji wa watu bila ya matatizo. Hili ni eneo muhimu kuliangalia kwani kunaweza kutokea watu kuingia katika nchi na kumiliki ardhi. Jambo hili linaweza likapitia kwa mtu binafsi kumilikisha mgeni ardhi. Hivyo basi, ni vizuri kuongeza taaluma kwa watu wetu ili kunusuru tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia utamaduni, mila za kitanzania ni watu wanapendana kama ndugu. Napata wasiwasi mkubwa kupitia nchi wanachama wenzetu kuwa mara nyingi hutokezea mizozo katika nchi zao. Je, tunasoma nini kupitia mizozo hiyo ambayo hadi sasa inajitokeza. Je, kuna mkataba maalum katika jumuiya hii, ambao unaweza kumwondoa uanachama nchi ambayo ina migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usalama Watanzania tumeona mapigano ya baadhi ya wananchi wa nchi mwanachama kuvamia mifugo ya Watanzania kwa njia ya wizi. Je, Jumuiya yetu imesoma nini katika tatizo hili ambalo huhatarisha maisha ya watu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uwezo. Kwa dhana potofu iliyotawala vichwani mwetu ni kuona Watanzania tuko nyuma kielimu. Kwanza napenda kujua hii ni kweli? Kwa kuzingatia ajira ya Afrika Mashariki napata wasiwasi kwa Watanzania pale ambapo itajitokeza kuwa Watanzania tumezidiwa kielimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuia ya Afrika Mashariki inaweza kumgomboa Mtanzania katika umaskini ikipitia kuwepo soko mahsusi la Afrika Mashariki. Wizara inapaswa iwahamasishe Watanzania wetu ili waweze kutekeleza biashara zao. Baada ya maelezo yangu, sasa nimpongeze Waziri – Mheshimiwa Kamala, Naibu Waziri - Mheshimiwa Mohamed Aboud.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapa hongera Waziri na Naibu Waziri kwa kazi zao. Ahsanteni.

**MHE. KHADIJA SALUM AL-QASSMY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ni kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kufika hapa Bungeni bila ya kukamatwa mkono. Nasema *Alhamdulillah.*

Pia nachukua fursa hii kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika, Naibu wako pamoja na Wenyeviti wako wote kwa jinsi mnavyotulea katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia hotuba ya Wizara husika, utaona nia ya Serikali katika kusimamia mipaka yetu ya nchi. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake kwa hotuba yao iliojaa matumaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushirikiano wa Umoja wa Afrika Mashariki ni mzuri sana, ila tunahitaji sana kuwa macho katika ardhi yetu. Nchi ni ardhi na watu wake Serikali yapaswa kutoa elimu kwa Watanzania wote kwani kwa kuzingatia maamuzi ya kuwepo kwa soko la pamoja tujue hili litaweza kuingiliana na watu wa nchi hii na ile bila tatizo. Hii ni nzuri ila kuna raia ambao hawana nia mbaya, wakaweza kuuza ardhi yetu kwa wageni. Jambo hili linahitaji sana kuangaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuangalia mkataba uliopo wa ushirikiano wetu ni kutokuwepo kwa mzozo katika nchi mwanachama. Je, Serikali inasema nini katika hili hali hivi sasa nchi wanachama zina mizozo? Pia, kumejitokeza tatizo la baadhi ya wafugaji kutoka nchi jirani mwanachama kuingia nchini na kuvamia mifugo kwa njia ya wizi. Je, huku sio kuvunja amani? Ahsante.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia na kupata fursa hii kuchangia katika hotuba ya bajeti ya Afrika mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia fursa hii kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Dr. Deodorous Kamala - Waziri wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Mohamed Aboud - Naibu Waziri wa Afrika Mashariki, Katibu Mkuu na Watendaji wote

wa Afrika Mashariki kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa shughuli za Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika misingi ya kukua kwa uchumi wa nchi zetu ndogo na masikini hasa zinazoendelea zinalazimika kwa dhati kabisa kuwa na nguvu ya uchumi kwa ushirikiano wa masuala mbalimbali ya soko kikanda. Misingi hii ndiyo inayoimarisha uwezo wa wafanyabiashara wetu kutangaza na kuuza bidhaa zao kwa kutegemea zaidi wateja wa ndani suala ambalo linajenga uwezo wa viwanda kutokana na mauzo yanayotokana na ushirikiano nchi wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha hilo jambo muhimu la kuzingatia ni suala la kujengea uwezo wa uzalishaji viwanda vyetu. Kupitia suala hili lazima Jumuiya iandae kituo kimoja ambacho kitakuwa ni chombo cha kupima ubora wa bidhaa zinazotokana na viwanda vyetu vya ndani. Chombo hiki lazima kiwe Makao Makuu ya Jumuiya Arusha kufanya hivyo kutasaidia kuondoa hila kwa baadhi ya nchi kushusha au kukataa baadhi ya bidhaa kwa kigezo kwamba hazina ubora.

Serikali ihamasishe wafanyabiashara wa ndani kuzingatia na kutengeneza bidhaa zinazoweza kushindanishwa. Serikali ishike soko la Rwanda, Burundi, *Eastern Congo* na Uganda kwani ni soko ambalo litainua hali ya uchumi wa nchi yetu, tuimarishe Bandari, Reli, Barabara na huduma za anga. Nashauri Wizara kuanzisha Ofisi ndogo za Afrika Mashariki maeneo ya mipakani tumekubaliana na nchi wananchama wa Jumiya ya Afrika Mashariki ili kufanya kazi mbalimbali za Jumuiya ikiwemo.

**MHE. MARGARET A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri pamoja na kwamba Wizara ni mpya, lakini kazi inaonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia machache kama ifuatavyo:-

Nimefurahishwa sana kwa shughuli zilizotekelezwa na Bunge la Afrika Mashariki kuwa moja ya maazimio waliyopitisha Wabunge ni lile la kuhimiza nchi wanachama kuridhia Azimio la Haki za Watu wenye Mahitaji Maalum, naamini watu wenye ulemavu wakiwemo. Msukumo huu ulikuwa wa manufaa kwa walengwa na napongeza Serikali yetu Tanzania kwamba hima iliandaa taratibu za kuridhia Azimio la Kimataifa la Haki za Watu wenye Mahitaji Maalum mnamo Mkutano wa kumi na Tano wa Bunge letu. Tunachosubiri sasa Bunge la Afrika mashariki lisichoke lihimize nchi wanachama watunge Sheria zitakazoendana na Azimio husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono ushauri uliotolewa na Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kuhusu utaratibu wa Kisheria wa kuwalinda Watanzania na ardhi yao ili wageni wasivamie tu ilimradi.

Ushauri huu ni muhimu sana, kwani raslimali ardhi ndiyo kuu kwa Watanzania wengi wanayoitegemea na Sheria zifuatwe kama tulivyojipangia. Tusipokuwa makini katika hili, Tanzania ambayo ina ardhi nzuri ya kutosha inaweza kuporwa na watoto wetu wakakosa ardhi nzuri. Pongezi zaidi kwa maamuzi yaliyofikiwa na Wakuu wa nchi zote wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina uhakika endapo itifaki ya umoja wa forodha inaeleweka kwa kiwango sawa katika nchi wanachama. Nasema hivi kwa sababu ni hivi juzi nimeona kwenye luninga wananchi wa Burundi wakilalamika na kuhoji nini watapata wakijiunga na itifaki hii? Kwa msingi huo nashauri elimu iendelee kutolewa kwa wananchi kabla ya kusaini itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchakato huo, naunga mkono hoja.

**MHE. OMAR ALI MZEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa umeipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar juu ya ushiriki wake wa dhati katika majadiliano mbalimbali katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, lakini mashaka yangu makubwa yapo pale ambapo Zanzibar ilikuwa mwanachama mwanzilishi wa Jumuiya hiyo, lakini ikaondolewa bila hata ya ridhaa yake, kama ni katiba wakati huo ilikuwepo kabla ya kuvunjika kwa jumuiya hiyo, lakini kwa kuondoa Wizara ya Mambo ya Nje na kuanzisha Wizara ya nje na ushirikiano wa kimataifa, ndio hapo kumeiondoa Zanzibar kutokuwa mwanachama wa Jumuiya hiyo. Kama Zanzibar ingelikuwa ni mwanachama, Tanzania ingelifaidika zaidi kutokana na ushiriki wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi yenye amani na utulivu ukilinganisha na nchi wanachama kwa mfano uchaguzi wa hivi karibuni wa Kenya tumeona nini kimetokea, ugomvi wa Kenya na Uganda kwa kisiwa kidogo nini kinaashiria na hatua gani zimechukuliwa na Jumuiya kuhusu ugomvi wa Kenya na uganda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tuna ardhi ya kutosha, lakini wenzetu kila leo ni migogoro ya ardhi: Je, tutailindaje ardhi yetu kutokana na wageni wengi ambao wataingia nchini na kuvamia kila sehemu kutomiliki ardhi yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi iliyopangwa kutekelezwa kwa Zanzibar nafikiria ni kitendawili, kwani imeombewa utekelezaji. Je, ikishindikana, nini kitatokea? Kwa vile haina ushiriki wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashaka yangu makubwa ni ule mradi wa kiwanja cha ndege cha Karume ambao ni kipaumbele: Je, ni kweli mradi huo utatekelezwa? Ahsante.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hotuba ya Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki ukurasa 13 kifungu 24 ziko bidhaa ambazo zinaingizwa nchini bila ya kulipiwa ushuru. Hilo ni jambo la faraja. Lakini ninachotaka kufahamu kwa kina ni msamaha huo wa kodi kwa bidhaa. Unawasaidia wananchi kwa

kupata bidhaa hizo kulingana na msamaha huo: Je, msamaha huo si unawanufaisha zaidi wafanyabiashara wakubwa tu? Uzoefu unaonyesha wafanyabiashara wakubwa ndio wanaonufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Katiba sio msahafu, ipo haja Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ibadilishwe ili Zanzibar nayo iwe na uwanachama wa Jumuia ya Afrika ya Mashariki. Kimaslahi ya kiuchumi na nguvu za maamuzi ndani ya Jumuia ya Afrika ya Mashariki utaimarika zaidi iwapo Zanzibar itakuwa na uanachama wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa 19 kifungu 33 imeelezwa katika Jumuiya kuna ongezeko la ajira. Mfano mwaka 2005 ajira mpya ni 2,643 na mwaka 2006 ajira mpya zilikuwa 5,379: Je, katika ajira hizo kuanzia mwaka 2005 mpaka 2008 Watanzania wangapi waliajiriwa kwa miaka hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Serikali mbili, yaani Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Zanzibar, yako mambo ambayo yanapaswa yashuhulikiwe na Muungano na yako mambo yanayoshuhulikiwa na Zanzibar. Sasa iweje mambo ambayo sio ya Muungano yashuhulikiwe na Muungano katika Jumuia ya Afrika ya Mashariki? Ahsante.

**MHE. RITA L. MLAKI:** Kwanza napenda nimpongeze Waziri – Mheshimiwa Kamala, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii. Mmeweza kutuwakilisha vizuri nchi yetu katika Jumuiya hiyo.

Ninapongeza sana mpango wa ushirikiano wa kibiashara kuangalia uwezekano wa eneo huru la kibiashara *EAC – SADC – COMESA*. Hii itatusaidia sana. Ila ningependa kujua kama nchi zilizo *separately EAC or SADC or COMESA* zitaachwa uhusiano wao *as individual intergration* na kuunda *one big block* yenye nchi zote za *EAC, SADC and COMESA*? Ningependa nyie kama zitafanya biashara kwa pamoja na sio kwa kubagua nchi zilizo *say EAC and not COMESA or not SADC!* Nitaomba Waziri anipe ufafanuzi kidogo.

Pili, bado kuna matatizo ya Wafanyabiashara wadogo wadogo wanaofanya biashara Kenya. Wafanyabiashara wetu bado wananyanyasika na mabango yao yanaondolewa huko Kenya. Naomba mlitizame hilo kwa undani zaidi. Tatu, ningeomba Serikali ilegeze masharti kidogo ya watu wa Kenya kuja kufanya kazi Tanzania. Hiyo ni nguvu kazi nzuri na inaweza kutusaidia tusiogope kuwa watachukua kazi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. MOHAMED ABDUL AZIZ:** Napenda kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri Dr. Diodorus Kamala kwa hotuba nzuri, naomba nichangie katika masuala yafuatayo:-

Kwa mujibu wa makubalinao ifikapo mwaka 2010 bidhaa ambazo ni *Semi finished and finished products* zitakuwa zinazotozwa ushuru wa 0% kutokana na kuwa na viwanda vingi kati ya nchi za wenzetu hasa Kenya, upo uwezekano mkubwa wa Tanzania kuwa soko la Bidhaa za Kenya nilitaka kujua Serikali inajiandaa vipi kuona viwanda vyetu vimepata uwezo wa kuzalisha bidhaa bora ili kumiliki ushindani na pia Serikali inajiandaa vipi kuhakikisha kuwa bidhaa zinazoingizwa kutoka katika nchi wanachama wa Jumuia kuwa ni kweli zinatoka katika nchi hizo na sio kwamba zinatoka nchi za nje na kuzifanya nchi hizo kuwa daraja tu la kuingiza bidhaa bila ushuru kutoka nchi za kigeni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nashauri suala la ardhi lisiwe jambo la kuingizwa ndani ya makubaliano ya kuwa ni mali ya wananchi wa Afrika Mashariki kwa vyovyote vile Ardhi ya Tanzania iwe ni kwa ajili ya Watanzania tu. Hata kama ardhi hiyo hatumiliki sasa, lakini Watanzania tunaongezeka. Tulikuwa milioni tisa miaka ya sitini leo hii tunakaribia milioni 40. Sio lazima tugawe ardhi yetu yote hivi sasa. Lazima tujifunze matatizo yaliyotokea katika baadhi ya nchi za wenzetu ambazo matatizo au migogoro ya ardhi imepelekea nchi hizo kuingia katika machafuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi ndio taya, ndio mali na ndio urithi pekee usiohamishika. Naomba Waziri anithibitishie nini msimamo wa Serikali kuhusu suala la ardhi katika Jumuia ya Afrika Mashariki.

**MHE. SULEIMAN OMAR KUMCHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina haja ya kuzungumza mengi. Ni kusisitiza tu kwamba ardhi ibaki kwa Watanzania pekee tulipokuwa tunapata uhuru tulikuwa na watu milioni tisa, sasa tuko milioni 40, ardhi ni ileile haijaongezeka. Tusijenge mazingira ya matatizo kwa Watanzania hapo baadaye kwa kukosa ardhi. Ardhi ibaki kwa Watanzania pekee. Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri Mungu amlinde.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na Watendaji wote kwa kuwasilisha bajeti yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla hatujaingia katika Jumuiya ya ushirikiano wa Afrika Mashariki, ni vyema wananchi wakamilikishwa ardhi kwa kupatiwa hatimiliki ili ardhi hiyo iwe ni mali yao, watoto wao na hata vijukuu vyao hapa baadaye badala ya mfumo huu tulionao ambao Serikali kupitia Rais wa nchi ndio mmiliki wa ardhi yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi ni raslimali muhimu sana ambayo shughuli mbalimbali zinaweza kufanyika kupitia ardhi kama vile kilimo, ufugaji, ujenzi wa majumba, viwanda na vitega uchumi mbalimbali. Kwa hiyo, Serikali inapaswa kuona umuhimu wa ardhi yetu kwa maslahi ya wananchi wetu na Taifa kwa jumla. Ni vyema

Serikali ikajiandaa vyema ili tutakapoingia katika jumuiya, ardhi yetu isijeikawanufaisha wageni zaidi kuliko wazawa wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania tumezoea kuishi kwa amani, utulivu na mshikamano. Je, Serikali imejiandaa vipi ili kuingia katika Jumuiya ya Afrika Mashariki isije kutuletea vurugu na hivyo kuharibu mfumo mzima wa maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kenya wamejiimarisha vizuri katika suala la viwanda na biashara. Tanzania tumejiandaa vipi kukabiliana na ushindani katika suala zima la biashara?

Mheshmiwa Mwenyekiti, kuna kero mbalimbali hasa zinazohusu Muungano wetu. Je, Serikali imejiandaaje ili kumaliza matatizo yetu ya ndani?

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Watendaji wote wa Wizara. Nyote kwa pamoja hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Karagwe na Kyerwa na Watanzania wote kwa ujumla, tunaomba na kusisitiza mradi wa umeme wa Mrongo Chikagati mpakani mwa nchi yetu na Uganda Ujingwe kwa haraka. Umeme huu ninaomba ufike maeneo yote ya Wilaya ya Karagwe kuanzia Kimbo la Kyerwa na Jimbo la Karagwe na kuingizwa katika vijiji vyote vya Wilaya ya Karagwe kwa kuwa wananchi wote wanao uwezo wa kuulipia. Nashauri Jumuiya ya Afrika Mashariki ifadhili maradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti barabara ya Mrongo hadi Gakorongo imepandishwa hadhi toka barabara ya Wilaya hadi ya Taifa kwa sababu inaunganisha Tanzania na Uganda na pia inaunganisha Tanzania na Rwanda na Burundi nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ijengwe na Jumuiya kwa kiwango cha lami. Reli ijengwe toka Uganda, Tanzania kupitia Karagwe hadi Burundi na Rwanda. Itainua uchumi wa nchi zetu hizi.

Pongezi kwa kupunguza wizi wa mifugo Wilayani Karagwe uliokuwa unafanywa na wezi toka nchi jirani ya Rwanda na Uganda. Jumuiya ya Afrika Mashariki ikaze kamba kukomesha moja kwa moja wizi huu. Nchi jirani za Rwanda, Burundi, Uganda na Kenya ziache kushabikia wizi huu, zipambane na wizi huu kwa uwazi na ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kwa kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wake kwa maandalizi na uwasilishaji wa makadirio ya mapato na matumizi kwa Wizara hii Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utagusa katika maeneno machache tu ambayo ama ni ya ushauri au ufafanuzi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo la kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na Wakuu wetu wa nchi wanachama halina budi kupongezwa sana kwa vile dunia ya leo bila ya umoja, nchi (hasa zinazoendelea) uchumi wake utaendelea kuwa duni na hivyo kuwa na hali duni kwa maisha ya wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya hii hivi karibuni itaadhimisha miaka kumi tangu ianze ikiwa imejiwekea mipango kemkem. Hata hivyo, utekelezaji wa mipango iliyojipangia ufanisi wake umejikita zaidi kwenye eneo la Umoja wa Forodha pekee na masuala mengine, utekelezaji wake kuendelea kusuasua. Wasiwasi wangu ni kuwa mipango hiyo itaendelea, ilitajwa kwenye makabrasha tu bila kutekelezwa: Hivi Mheshimiwa Waziri anaweza kulieleza Bunge lako Tukufu ni muda upi kwa kila mpango utaanza na kumalizika utekelezwaji wake? Miradi hiyo watekelezaji wakuu ni nchi mwanachama au miradi hiyo inasubiri ufadhili kupitia Jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na mgogoro wa kugombania kisiwa kilichomo kwenye *Ziwa Victoria* kati ya nchi wanachama wa Jumuiya (Kenya na Uganda). Hivi ugomvi huu haudhoofishi Jumuiya ya Afrika Mashariki? Kwa nini jambo dogo kama hili lifikie hatua iliyofikiwa sasa? Nina wasiwasi kuwa Jumuiya hii ni kama mvua za rasha rasha tu. Naamini kabisa, baadhi ya viongozi wa nchi wanachama wa Jumuiya hii walitaka kuanzisha Muungano huu kwa maslahi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na wasiwasi huu, Tanzania isitishe kwa muda kuwa mwanachama wa Jumuiya hadi pale itakapoonekana viongozi wa nchi zinazogombana wamepata ufumbuzi wa kudumu, vinginevyo viongozi wa nchi tano za Jumuiya wakae na kusuluhisha ugomvi huo mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miradi ya Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, nazipongeza sana Serikali mbili za *SMT* na *SMZ* kwa mashirikiano mazuri ambayo yameiwezesha Zanzibar kuwasilishiwa miradi yake kadhaa kama ilivyoorodheshwa ukurasa wa 56 wa kitabu cha hotuba ambayo itafadhiliwa kupitia mpango wa ufadhili wa Jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukarabati wa uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Zanzibar hivi karibuni *SMZ* imesaini mkataba na mkandarasi (Kampuni ya Ufaransa) ya kukarabati uwanja huo kazi ambayo itaanza wakati wowote baada ya Mkandarasi kukamilisha upelekaji wa zana za ujenzi kwenye eneo la ujenzi *(site).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyofahamu mimi mradi wa ukarabati wa uwanja huo umefadhiliwa na Benki ya Dunia ya Maendeleo *(IDA).* Naomba ufafanuzi, mchakato unaoendelea wa kutafuta fedha za ukarabati wa uwanja huu kupitia ufadhili wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo Jumuiya ya Ulaya *(EV)* imeonyesha nia ya kufadhili mradi huo. Endapo *EU* watakubali ufadhili wa mradi huu, ni kazi zipi zitakazofanywa kwenye uwanja huo zaidi ya zile zinazofanywa hivi karibuni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana fedha zitakazopatikana kutoka kwa wahisani wa Jumuiya ya Ulaya zisije zikapelekwa kwenye miradi mingine kwa visingizio kuwa ukarabati wa kiwanja hicho kitakuwa tayari kimefanyiwa ukarabati kwani bado kuna mahitaji mengi zaidi yanayotakiwa kufanywa kwenye kiwanja hicho cha ndege kwa mfano Ujenzi wa *apron* na *passenger terminal* mpya na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wengi hawana taarifa ya kuwa kuna Wabunge wa aina hii wanaochaguliwa kupitia Mabunge ya wanachama wa Jumuiya. Naishauri Wizara itoe elimu kwa wananchi wetu kuwaelimisha juu ya jambo hili la Bunge la Afrika Mashariki na umuhimu wa Wabunge hao. Aidha, Wizara iwawekee taratibu Wabunge hao wa kuwatembelea wananchi kikanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa Waheshimiwa Wabunge hawa walichaguliwa na Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Kwa upande wa Tanzania), lakini hatupati taarifa zao wanazozifanya. Ni vyema sasa wateue mwakilishi wao ili angalau mara moja kwa kila mwaka aje Bungeni (Jimboni kwao) kuwasilisha taarifa wanazozifanya Bungeni kwao na kubadilishana fikra na wapiga kura wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikia kuna pendekezo la Wabunge wa Afrika ya Mashariki kuchaguliwa na wananchi wa nchi husika. Je, ni kweli? Kama siyo, nini mapendekezo mbadala ya upatikanaji wa Wabunge wa Afrika Mashariki na ule wa 50?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Mungu ibariki Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**MHE. FATUMA MIKIKADI:** Kwanza ninampongeza kwa kusoma vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kuhusu Viwanja vya Ndege, Kilimanjaro, Dar es Salaam, Mtwara, Lindi, Zanzibar, Pemba na Kigoma. Kwanini nimevitaja Viwanja hivi? Nimevitaja viwanja hivi kwa sababu vipo mipakani mwa Tanzania ambamo ndimo tunamokutana na jirani kwa shughuli za kibiashara, kimaisha, kijamii, kisiasa na kadhalika.

Kwa mtazamo wangu, Airport hizo zingekarabatiwa vizuri zaidi ili tuweze kuingiza uchumi na pia kuonyesha kuwa, na sisi tupo mbele katika ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika Bandari za mipakani Kando ya Ziwa Victoria - Mwanza, Musoma, Bukoba, kando ya Ziwa Tanganyika, Bandari zake zote na kando ya Bahari ya Hindi. Bandari zote hizi ni nyenzo kubwa, matumizi ya Jumuiya ya ushirikiano wa Afrika. Maana ya ushirikiano huu wa Afrika ni kukuza uchumi, kuendeleza biashara, kupata mahitaji muhimu. Kwa hiyo, sisi Tanzania inabidi tuandae mazingira mazuri ili iwe kitega uchumi chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshaona kuwa, tunauza chumvi nyingi sana nje (Tazama ukurasa 15) kwa nini tusiwasaidie Mikoa inayotengeneza chumvi ili izalishe

chumvi zaidi kama Bagamoyo, Lindi, Tanga, Dar es Salaam na kadhalika wasaidiwe pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Mtwara Corridor, Central Corridor, Tanga Corridor* hizi ni muhimu kwa mawasiliano, uchumi, biashara kwa ushirikiano huu zifufuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vituo vya Uhamiaji vya mpakani vikiwemo Mtwara, Namanga, Tunduma, Kigoma, Mwanza, Tanga na Dar es Salaam, viimarishwe. Pia njia za panya kwa maana njia ambazo watu wanapita kiwizi, sio halali zidhibitiwe kwani watafanya ushirikiano wetu usiwe na amani na utulivu.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kusema kuwa ninampongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake yote wakiwemo Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara hii kwa hotuba nzuri. Hotuba hii inatupa picha ya mambo yajayo na Watanzania wajiandae vipi kuungana na wenzao katika nchi za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi ndiyo rasilimali muhimu kwa Watanzania zaidi ya asilimia 80. Watanzania hawa ukiwanyang’anya ardhi wanakuwa maskini wa kutupwa ndani ya mwaka mmoja tu. Naomba kuelezwa na Mheshimiwa Waziri, kwa nini hotuba hii imekwepa kuelezea masuala ya ardhi katika hotuba yake? Kuna nini kinachofichwa? Nini kinachoogopwa hata hotuba hii isielezee chochote kuhusu maendeleo ya ardhi na hatima yake kadri tunavyoendeleza mchakato wa muungano wetu? Wananchi wanayo haki ya kujulishwa kinachoendelea. Naomba Mheshimiwa Waziri atueleze bayana Wizara yake kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi na TAMISEMI itawasaidiaje wananchi kupata hati za kumiliki ardhi mapema iwezekanavyo? Bila wananchi kupata hati hizo hadi mchakato wa ushirikiano ukamilike Wizara hii itakuwa imewasaliti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inashangaza sana na kusikitisha sana unaposikia kiongozi Mtanzania anaposhawishi Watanzania waachie maeneo wazi kwa Wageni wakati hajajua kuwa Watanzania wanaendelea kuzaana na mpango wa uzazi wa mpango umeshindwa. Kiongozi huyo akijua kuwa ardhi haipanuki na yeye akiwa ana miliki mashamba makubwa, huu ni usaliti pia.

Ushauri wangu ni kuwa, kwa ujumla Tanzania bado haijawa tayari kuingia katika shirikisho hilo. Hapa tulipofika inatosha. Tujipange zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyomalizia asubuhi, nilisema kwamba, tutakapoingia nitamwita Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara hii ili atumie muda wa robo saa katika kujibu hoja mbalimbali ambazo zimetolewa hapa na baada ya hapo tutampa nafasi Mheshimiwa Waziri mtoa hoja ili aweze kuhitimisha hii hoja yake.

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutuwezesha kutujalia kuwa hapa jioni hii tukiwa wazima na wenye afya. Aidha, nikushukuru wewe Mwenyekiti kwa namna unavyotuongoza katika Bunge letu hili Tukufu. Pia nitumie fursa hii kumshukuru sana Rais Jakaya Kikwete, kwa kuniteua kuwa Naibu Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Aidha, nimpongeze kwa kazi nzuri anayoifanya ya kulitumikia Taifa letu. Nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa namna ambavyo wanamsaidia Rais katika kutekeleza majukumu yake vizuri sana na kuifanya nchi yetu kuwa katika hali ya amani na utulivu mkubwa; nawashukuru sana.

Pia nichukue nafasi hii kuishukuru sana familia yangu, hasa mke wangu na watoto wangu, kwa namna wanavyoniunga mkono katika shughuli hizi za kujenga Taifa letu. Namshukuru sana Waziri wangu, kwa ushirikiano wake mkubwa na msaada wake mkubwa kwangu ni wa aina ya kipekee. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Vilevile nawashukuru sana Watendaji wa Wizara hii, wakiongozwa na Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote na Wafanyakazi wote wa Wizara hii, kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kufanya kazi zetu za kila siku. Pia nichukue fursa hii, niishukuru sana Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Masilingi, Mbunge wa Muleba, kwa kazi nzuri wanayoifanya na ushirikiano mkubwa wanaotupa na maelekezo ya busara yanayotufanya kutekeleza vyema majukumu yetu. Nitoe shukrani maalum kwa Waheshimiwa Wabunge wote, kwa namna ambavyo wanatupa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza kazi zetu za kila siku. Kwa kweli Waheshimiwa Wabunge, mnatusaidia sana na tunashukuru sana. Tunawaombea Mungu awazidishie kheri na baraka nyingi katika shughuli zenu. *Amen.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na muda, nitaomba radhi sana kwa kuwa muda wetu ni mdogo, inawezekana kabisa usitoshe kujibu hoja zote za Waheshimiwa Wabunge, lakini tutajitahidi kadiri tutakavyoweza kujibu zinazowezekana kujibiwa na zile ambazo hatukupata nafasi, basi tunaomba radhi tutahakikisha kwamba, tunazijibu hoja hizo kwa maandishi kwa Waheshimiwa Wabunge wote. Waheshimiwa Wabunge, michango yenu kwetu sisi imekuwa mafunzo makubwa sana na darasa kubwa sana la kuweza kumudu vyema kutenda kazi zetu hasa kwa kutetea maslahi ya nchi yetu; tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nieleze kwa kifupi sana umuhimu wa kuwa na mtengamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Jambo hili ni muhimu sana kwetu, kwa sababu ni mazoezi makubwa ya kujitayarisha katika ushindani mkubwa wa kibiashara huko ulimwenguni. Leo nchi ambazo zina chumi zinazolingana, tunapoanza kufanya kazi pamoja, tunajifunza vizuri kushindana, tunajiweka vizuri katika nguvu ya kutetea pale tunapokwenda kwenye mazungumzo na majadiliano na Taasisi mbalimbali na Jumuiya mbalimbali za Kimataifa. Kwa hiyo, utaratibu huu unatusaidia sana na ni mzuri sana na ule wasiwasi mkubwa ambao tulikuwa nao huko nyuma, kwa kuingia katika mtengamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, naamini Watanzania wengi sasa

umepungua na wameona maslahi au matokeo makubwa yaliyojitokeza kwenye maeneo ya biashara, uwekezaji na masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo, tumepiga hatua kwa njia moja ama nyingine. Kwa hiyo, nataka nichukue fursa hii, kuwapongeza sana wataalamu wetu wanaoshiriki katika majadiliano na taasisi zote zinazoshiriki katika majadiliano haya ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, kwa namna ambavyo wanajitahidi kujenga heshima kubwa ya nchi yetu na kujenga hoja ya dhamana zinazoweka msimamo wa nchi yetu. Kwa hiyo, nashukuru sana kwa yote haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba niende moja kwa moja kwenye hoja ambazo zimezungumzwa hapa Bungeni leo. Nikianza na hoja iliyozungumzwa na Kambi ya Upinzani na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, kuhusu ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Waheshimiwa Wabunge, utaratibu ambao tunao mpaka sasa haujatupa matatizo yoyote zaidi ya kutujengea nguvu zaidi na kutupa uwezo zaidi wa kujenga hoja pale tunapokwenda katika majadiliano yao mbalimbali. Utaratibu huu umetupa nafasi kubwa sana ya kuweza kumudu vyema majadiliano mbalimbali katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Umetupa nguvu kubwa na ni utaratibu unaotumika na nchi nyingi tu ulimwenguni hata hizi nchi kubwa kama Marekani, Canada, Uingereza na kwingineko ulimwenguni, wanatumia utaratibu kama huu hawatumii utaratibu wa kwenda kwa mmoja mmoja.

Kwa msingi huo, ningependa kuwajulisha Waheshimiwa Wabunge kwamba, utaratibu tunaokwenda nao ni mzuri na haujatupa matatizo. Najua hivyo ni utaratibu ambao umejengwa Kikatiba. Ukiangalia mtengamano huu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, unaotufanya twende hatua kwa hatua kuanzia hatua ya Umoja wa Forodha, Soko la Pamoja, Sarafu moja na hatimaye Shirikisho la Kisiasa hapo tutakapokubaliana, utaona ni mambo ambayo yanagusa sehemu mbili za Muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiingia kama sehemu moja ya Muungano kwenda kwenye mazungumzo ya namna hii, inawezekana kabisa katika majadiliano hayo unapoingia peke yako ukaathiri upande mwingine wa Muungano. Kwa hiyo; ni vizuri sana tunapoingia katika majadiliano, tuingie mahali kwa pamoja kwa maana kabla ya kwenda kwenye mazungumzo na wenzetu, kwanza tunajenga msimamo wa nchi kwa pamoja na tunapokwenda pale tunakuwa ni jambo moja, vinginevyo unaweza kuleta taathira kubwa hata kudhoofisha Muungano wetu, kitu ambacho hatungependelea sote humu ndani. Kwa hiyo, utaratibu wa sasa ni mzuri, ikiwa hoja ni suala la kuwa na Wabunge wengi, hoja hiyo tunaweza kuizungumza tu ndani ya Jumuiya tukasema kwamba, uwakilishi wa Wabunge tisa ni kidogo, tuongeze idadi ya Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoongeza idadi ya Wabunge, tujue pia tunaongeza idadi ya gharama; cha msingi ni Wabunge ambao leo wanatuwakilisha, je wanatuwakilisha kwa kiasi ambacho mnakihitaji. Hilo ndilo jambo la msingi na naamini Wabunge wetu ni makini, mahiri, wanatetea sana hoja ya nchi yetu na wana uwezo mkubwa. Tena Wabunge wa pande zote mbili ni makini sana na wana uzoefu mkubwa sana na wanafanya kazi nzuri sana, inafaa tuwapongeze kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, utaratibu tunaokwenda nao naona ni mzuri; unaimarisha umoja wetu, unaimarisha Muungano wetu na unatujengea nguvu za majadiliano. Kwa hiyo, bado utaratibu huu ingekuwa ni vyema tukaendelea nao. Kuna mambo yanayohusu miradi ya Zanzibar, hili pia lilisemwa sana hasa na Kambi ya Upinzani na Mheshimiwa Hamad Rashid na Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mheshimiwa Mwadini Jecha na Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa*;* alisema aja aja kianga aja aja huyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, niseme wazi kabisa kwamba, utaratibu wa miradi ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, una mchakato wake wa kufuata, lazima ule utaratibu ufuatwe. Tunapopeleka ile miradi, haikubaliwi siku hiyo hiyo tu; kwanza, inatakiwa ifanyiwe uchambuzi kama miradi hiyo inakidhi viwango vya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Baada ya kufanyiwa uchambuzi huo, inabidi Sekretarieti ikae na sekta husika, kuzungumzia kwa makini zaidi ile miradi ili kuiona kama imekamilika na kama ina upungufu wowote, inahitaji kuongezewa maandiko mengine hasa kufanya *study* ambayo inaweza kuwavutia wahisani na wafadhili wetu wa maendeleo, inabidi pia wakae pamoja waitafakari, waiwekee utaratibu mzuri ili iweze kufanyika na iweze kuwavutia hawa wahisani wetu na wenzetu katika maendeleo.

Kwa hiyo, msingi wake mkubwa kuchelewa si kwamba, inacheleweshwa makusudi, lakini *process* na miradi hii haikuja muda mrefu sana. Kwa hiyo, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, kwa sasa tumefikia hatua kubwa ya *process* ya kumalizia miradi hii ianze, basi namna ya kutafuta fedha kwa upande wa wafadhili na hatua hizo zimefikia hatua nzuri sana. Kwa upande wa mradi mmoja ambao hauko katika hatua ya mwisho kabisa ni Mradi wa *Airport* ya Karume Pemba. Mradi huu tayari upo kwenye ADB 11 na hatua zake ziko katika hatua ya mwisho ili kuanza kwa mradi huo. Lazima tuwe na ustahimilivu, kutafuta fedha si jambo rahisi; ni jambo gumu hasa wakati kama huu ambapo ulimwengu una mtikisiko mkubwa sana wa uchumi. Kwa hiyo, tuendelee kuvuta subira na nikuhakikishieni Waheshimiwa Wabunge kwamba, hali hii tutafikia mahali pazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kengele ya mwanzo imeshanililia, nitajitahidi kwenda haraka zaidi. Kuhusu suala la elimu kwa umma; hoja hii imechangiwa sana na Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed – Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ulinzi na Usalama. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, Wizara yetu imejipanga vizuri katika kuhakikisha kwamba, inatoa elimu kwa umma kuanzia ngazi mbalimbali. Ushauri wenu kwanza, tunauzingatia; ni ushauri muhimu sana wa Watanzania kuelewa mchakato mzima huu wa mtengamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, lakini hatua inaanza. Tumeanza upande wa Zanzibar tayari Unguja na Pemba tumepitia Wilaya zote kutoa elimu hii.

Tumeanza kwa Mikoa ya Kusini tu, imekwenda Mtwara, Lindi na hivi karibuni nitaendelea na mikoa mingine kwa upande wa Tanzania Bara ili kuendeleza kutoa elimu kwa umma. Hata hivyo, kupitia runinga, magazeti, vipindi mbalimbali vya kwenye

runinga na kuwasiliana na Taasisi mbalimbali zisizo za Kiserikali kwenye Vyuo Vikuu na maeneo mengine muhimu yote, hatua zinachukuliwa kwa kwenda kutoa elimu ila hili jambo lieleweke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano hai sana ni huu wa leo hapa, umeanza kuchangiwa na zaidi ya Wabunge 37. Kwa hiyo, hii inaonekana kwamba, Wizara yetu inaanza kujulikana ukilinganisha na huko nyuma ilikuwa na idadi ndogo tu ya Wabunge. Tulikuwa tunazungumza na Waziri wangu hapa, kumwambia kwamba, inaonekana Wizara yetu inaanza kujulikana, hata maswali tunaanza kuulizwa hapa Bungeni. Kwa hiyo, tunashukuru sana na tunataka kuwahakikishia kwamba, jitihada hizi zitaendelea hasa kwa mwaka huu wa fedha. Jambo la msingi hapa ni kutupitishia hii bajeti tuliyonayo mbele yetu na tuweze kufanya kazi hii kwa uzuri zaidi. Naamini Waheshimiwa Wabunge mtaifanya kazi hiyo vizuri, kwa sababu tunayo mahusiano mazuri ya kuona jitihada tunayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la wizi wa mifugo hasa huko mpakani; ni kweli hili jambo linahuzunisha sana. Kwanza, nitoe pole sana kwa ndugu zetu wale wa Rorya na Tarime, kwa wizi ambao unaendelea. Sisi kwa upande wetu kama Wizara, kwanza, tutawasiliana na wenzetu wa Wizara nyingine husika, zenye kusimamia mambo haya ya ulinzi na usalama hasa upande wa Jeshi la Polisi ili kuhakikisha kwamba, ulinzi katika maeneo yale unazidi kuimarishwa na kupambana vilivyo na uhalifu unaotokea pale. Pia yale mashauri ambayo yaliyotolewa na Mheshimiwa Mwera na Mheshimiwa Sarungi; Mheshimiwa Sarungi ametoa mapendekezo mengi mazuri ambayo tutayafanyia kazi. Alitaka jambo hili lipelekwe katika Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki, kazi hiyo tutaipeleka na itakuwa moja katika ajenda ya mazungumzo ya ule wizi unaotokea pale mpakani, maana ni jambo la kawaida kutokea katika mipaka yetu. Kwa hiyo, nataka kuliondoa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mkakati ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, unaosimamia suala la amani na usalama na mkakati huu unaendelea vizuri. Vikosi vyetu vya ulinzi na usalama vinapashana habari kwa kufuatilia nyendo mbalimbali ili kupunguza wizi unaojitokeza katika maeneo mbalimbali ya mipakani. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Sarungi, hatua zitachukuliwa kuhakikisha kwamba, yale yanayotokea yaondoke kabisa yasiweze kutokea, kwani yaliwaadhibu wananchi wetu, jambo ambalo ni la kusikitisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, vile vile walilizungumzia suala la malumbano ya Kisiwa cha Migingo. Nataka niwahakikishie kwamba, suala hili sasa lina mtazamo mzuri sana ndani ya Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki. Nchi hizi mbili zimekubaliana kwamba, ziendelee kulizungumza jambo hili kwa majadiliano ya amani na utulivu ya kindugu kwa sababu ni nchi mbili ndugu. Kwa msingi huu, mazungumzo yataendelea ili kutafuta njia muafaka ya kuondosha mgogoro huo. Msimamo wa nchi yetu ya Tanzania ni kutaka majadiliano haya yaende kwa utaratibu huu, ambao wenzetu wameukubali wa kufanya majadiliano haya kwa njia nzuri ya muafaka ili upatikane bila ya kutokea matatizo kati ya nchi zetu mbili. Ndani ya mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki, ibara ya 6 inaeleza wazi kwamba,

yanapotokea matatizo kati ya nchi wanachama, basi utaratibu mzuri wa kufanya ni mazungumzo kati ya nchi na nchi zilizohusika ili kuondoa tatizo hilo. Naamini ndugu zetu wa Kenya na Uganda, watalipatia ufumbuzi tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile liko moja la haraka haraka kuhusiana na suala la ajira kwa upande wa Zanzibar ndani ya Wizara yetu ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Zipo hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Wizara kwa nia ya kuhakikisha kwamba, Wazanzibari wanapata fursa ya kufanya kazi katika Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Hatua zimeanza; kuna baadhi ambao tayari wameajiriwa na tayari tumeandika barua Zanzibar, kuwasiliana na Idara inayohusika na Afrika Mashariki kuhusu utaratibu mzuri ambao utasaidia kuwa na wafanyakazi kutoka upande wa Zanzibar. Licha ya hayo, Kamati ile inayoshughulikia kero za Muungano ya SMT na SMZ, tayari imeweka utaratibu mzuri sana wa kuonesha ushiriki wa Zanzibar katika Taasisi na vyombo vya Muungano. Hilo jambo litakuwepo kisheria na linatolewa mapendekezo mazuri na kabla ya Desemba, 2010, utekelezaji utakuwa umeanza na hatua zitachukuliwa. Kwa hiyo, jambo hili la manung'uniko kwa upande mmoja kuhusu habari ya ajira, nafikiri litakuwa ni historia baada ya kutekelezwa hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu siko tayari kugongewa kengele mara ya pili, naomba nimalizie kwa kuwashukuru sana kwa kutusikiliza na kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, muipitishe bajeti yetu hii kwa moyo mkunjufu ili mtupe fursa ya kwenda kufanya kazi. Mwisho kabisa, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed. Sasa naomba nimwite mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki ili naye aweze kutumia nusu saa hapa, kuhitimisha hoja aliyowasilisha asubuhi.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nitoe shukrani zangu za dhati kwako, kwa jinsi ulivyoendesha shughuli hii toka tuanze asubuhi. Vile vile nichukue nafasi hii, kutoa shukrani zangu za dhati na za Wizara kwa Waheshimiwa Wabunge, kwa michango yao mizuri itakayotusaidia kuboresha utendaji wa shughuli zetu za kila siku pale Wizarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niahidi kwamba, kwa kuzingatia muda, hatutaweza kujibu hoja zote lakini tutafanya haraka kadiri itakavyowezekana, kuhakikisha hoja zote za Waheshimiwa Wabunge tunazijibu kwa maandishi. Nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Killimbah, ambaye alimwakilisha Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, lakini labda kabla ya kufanya hivyo, niwashukuru na niwatambue kwamba, jumla ya wachangiaji 38 waliojitokeza nawashukuru sana, lakini niwatambue kwa kuwasoma majina yao; kwanza ni Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah, Mheshimiwa Salim Yussuf Mohamed, Mheshimiwa Joseph James Mungai, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Prof. Philemon Sarungi na Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile tulipata wachangiaji 31 kwa kuandika, nao tunawashukuru sana na ni hawa wafuatao; Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Prof. Philemon Sarungi, Mheshimwia Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Charles Nangoro Mwera, Mheshimiwa Eng. Christopher Chiza, Mheshimwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Balozi Dkt. Getrude Mongella, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro, Mheshimiwa Arch. Fuya Kimbita, Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Khadija Salum Al-Qassmy, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Margreth Mkanga, Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Rita Mlaki, Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mheshimiwa Suleiman Omar Kumchaya, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa Bujiku Philip Sakila na Mheshimiwa Mama Anne Malecela. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizitazama hoja mbalimbali zilitolewa, zinagusa maeneo mbalimbali; ziko hoja zinazogusa masuala ya ardhi, ziko hoja zinazogusa masuala ya utumiaji wa fursa, ziko hoja zinagusa masuala ya Umoja wa Forodha, kuna hoja zinagusa masuala ya ushiriki wa Zanzibar, kuna hoja za Soko la Pamoja na hoja za utoaji wa elimu na hoja za mtengamano. Nikianza na Kamati, tunashukuru kwa hoja zote walizozitoa na ushauri walioutoa na maelekezo waliyoyatoa. Kama nilivyosema kabla ni kwamba, tutazingatia maelekezo hayo. Mojawapo ambalo Kamati imesisitiza na kushauri ni kwamba, tuwe na jitihada za makusudi kuhakikisha tunashughulikia vizuri vikwazo visivyo vya kodi kama ambavyo imekuwa ikijitokeza kwa mfano Kiwanda cha Maziwa, wakati fulani kilitaka kupeleka maziwa nchi mojawapo mwanachama kule wakaambiwa walipe asilimia 60 ya kodi.

Tulikumbusha wahusika wakaelewa, kwa hiyo, wakawa wameacha kufanya hivyo lakini kipo Kiwanda kimoja cha Safi kilijaribu kuuza nyama Kenya kule wakasema zile nyama hazikuwa na viwango. Tumewasiliana na wenzetu wa Kenya na wenzetu wa Safi, kwa hiyo, hilo linafanyiwa kazi na yako mambo mengi**;** kuna nchi moja ambayo yenyewe taratibu zake haziendani na nchi nyingine za Afrika Mashariki; wao wanatumia taratibu za COMESA za kuruhusu wakati sisi tunatumia taratibu za SADC. Kwa hiyo, yote haya tumeyazungumza kwenye vikao na tumekubaliana kwamba, tutayafanyia kazi. Labda jambo kubwa tunaloweza kulisisitiza kama nilivyosema ni kutoa wito tena kwa nchi wanachama, kuepuka kabisa kuweka vikwazo vipya, tukishaondoa vikwazo basi tusiweke vikwazo vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ilikuwepo hoja, Kamati imeagiza kwamba ni vizuri mchakato wa kujenga Makao Makuu ya Jumuiya ukaenda kwa kasi. Tunakubaliana na ushauri wa Kamati na tutalisimamia hilo, kwa sababu kama mnavyofahamu, hivi sasa Ujerumani imetupa *Euro* milioni 14 na kadiri tutakavyochelewa, gharama zitabadilika. Kwa hiyo, tusingependa turudi tena Serikali ya Ujerumani kuwaomba watuongezee. Kwa hiyo, tunatarajia na kadiri mipango ilivyo, haraka itakavyowezekana ujenzi wa Makao Makuu utaanza mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kulikuwa kuna suala la kuhamasisha Watanzania; Kamati imeshauri na Watanzania wamesikia kwamba ni vizuri kutumia bidhaa za ndani. Ukweli ni kwamba, katika uchumi, unapotumia bidhaa zilizozalishwa nchi nyingine maana yake unajenga ajira za ile nchi. Unapotumia bidhaa za nchi nyingine, maana yake unajenga uchumi wa ile nchi. Kwa hiyo, ushauri huu uliotolewa na Kamati ni wa msingi na tutaendelea kuusisitiza. Tutaendelea kutoa elimu kwa Watanzania ili tutangulize bidhaa zetu katika utumiaji. Kamati ilizungumzia suala la Umoja wa Forodha kwamba ni vizuri tusiwe na haraka tukafika sehemu tukajikuta kwamba, hatufanikishi katika ushiriki huo. Napenda niseme tu kwamba, kama tulivyowasilisha katika kitabu chetu ni kwamba, mauzo ya Tanzania yanaongezeka kila siku toka Umoja wa Forodha ulipoanza na ushahidi umeonesha hata viwanda vidogo ambavyo hapo kabla vilikuwa vinauza kwa shida katika Afrika Mashariki navyo mauzo yake yameongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatumia mfano wa Kiwanda cha TANICA, hiki ni Kiwanda kidogo sana kule Bukoba. Kiwanda hiki mwaka 2004 kilikuwa kinauza kahawa yenye thamani ya dola 115,307, lakini mara tu baada ya kuwa tumeanza kutekeleza Umoja wa Forodha, sasa mauzo yameongezeka mpaka dola 243,470. Vile vile siku za nyuma zilizopita, kulikuwa na matatizo kwamba, Tanzania machungwa yetu yalikuwa yanakwenda kama machungwa tu kuuzwa kule Kenya. Hivi sasa kuna Kiwanda kimoja cha UNNAT, ambacho kimeanza kuzalisha *juice* na sasa kinauza *juice* Kenya na kinauza *concentrate* Kenya. Kwa hiyo, tunafikiri kama tukiweza kufanya vizuri na kuwezesha viwanda vilivyo vingi zaidi kufanya hivi, basi tutaweza kufanya vizuri zaidi katika Umoja wa Forodha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani tunakushukuru sana kwa mchango wako mzuri na kwa hoja nzuri, umesisitiza umuhimu wa NTBs kwamba, tuziangalie. Hoja hii inafanana na hoja ya Kamati yetu ya Bunge. Vile vile umezungumzia kuhusu ardhi tusiache kiholela. Tunashukuru sana kwa kusisitiza hilo, tutaendelea kulisimamia. Umesisitiza pia juu ya umuhimu wa kwamba, ule mpango tutakaoandaa wa utekelezaji wa Soko la Pamoja ni vizuri mpango huo ukawashirikisha wadau wote. Tunakubaliana na ushauri huu uliotolewa na Kambi ya Upinzani na naomba niwahakikishie kwamba, tutauzingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa Upinzani vile vile wameshauri kwamba, ni vizuri kuheshimu uhuru wa kila nchi na sisi tunakubaliana na ushauri huo, kwa sababu hivi sasa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, kila nchi bado imebaki na uhuru wake. Tanzania imebaki kama Tanzania, Kenya inabaki kama Kenya, Rwanda inabaki kama Rwanda na Burundi inabaki kama Burundi. Kwa hiyo, katika ushirikiano huu na mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, unasisitiza suala la nchi kuheshimiana, unasisitiza kutotumia ubabe, unasisitiza umuhimu wa kugawana mapato sawa. Ushauri huo wa Upinzani unaendana na mkataba unavyoeleza na tunashukuru kwa ushauri huo tutaendelea kuuzingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la ardhi ambalo wachangiaji wote waliochangia wapatao 38, kwa njia moja ama nyingine wamelizungumzia. Kama nilivyosema katika hotuba, Wakuu wa Nchi tayari wameshaagiza kwamba, suala la ardhi zitumike sheria za nchi wanachama. Labda tu nielezee kwa kusisitiza kama nilivyosema ni nani wamelizungumzia suala la ardhi. Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah amelizungumzia, Mheshimiwa Killimbah, Mheshimiwa Salum Yussuf Mohamed**,** Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Sarungi, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Dkt. Mongella, Mheshimiwa Mkanga, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Omar Mzee, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Kimbita, Mheshimiwa Khadija Al-Qassmy, wote wamesisitiza suala la ardhi.

Sasa niseme kidogo tu kwamba, Wakuu wa Nchi wameshatoa maelekezo na tutayazingatia. Suala la ardhi kutumika, sheria za nchi husika si Tanzania tu tunafanya hivyo na wala si nchi za Afrika Mashariki tu tunafanya hivyo. Tunayo mifano mingi sana duniani, maana watu wengine wasije wakashangaa wakasema mbona sasa hawa wanaingia kwenye Soko la Pamoja, lakini wanasema suala la ardhi zitumike sheria za kila nchi. Kwanza ile Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyovunjika, suala la ardhi halikuwemo kwenye masuala ya Soko la Pamoja. Kwa hiyo, tunaendelea kutekeleza kile tu ambacho tulishaanza kukitekeleza. Waheshimiwa Wabunge, ukiangalia Mataifa mbalimbali duniani, kwa mfano, Saudi Arabia; kule Saudi Arabia ni marufuku kabisa kwa mgeni kumiliki ardhi, liko wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano ukienda kule Philippines, inaelezwa kabisa kwamba mgeni haruhusiwi kumiliki ardhi Ufilipino. Lakini vilevile ukienda nchi kama Thailand, wao wanasema ikitokea bahati mbaya ukarithi ardhi kwenye hiyo nchi na wewe si raia basi wanakupa mwaka mmoja tu uhakikishe ardhi hiyo umeirejesha kwa mtu ambaye ni Mthailand. Ikitokea Mtanzania umeenda kule, umekutana na rafiki, amekurithisha ardhi basi utanufaika na ardhi hiyo kwa mwaka mmoja baada ya hapo, inabidi uirejeshe kwa wahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiangalia hata nchi kama Mexico, wao wanasema, ni marufuku kwa mgeni kukaa ndani ya Km 100 kutoka kwenye mpaka kwamba popote unaweza ukakaa lakini ndani ya km 100, kama wewe ni mgeni, ni marufuku. Kwa hiyo, lazima ukae ndani ili wakuangalie vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si hiyo tu, ukiangalia *State of Missouri* ya kule Marekani, yenyewe inapiga marufuku wageni kumiliki ardhi lakini vilevile inapiga marufuku wageni kutumia Mawakala kupata ardhi. Kama alivyosema Mheshimiwa Kwaangw', kwamba tunaweza tukasema wageni wasimiliki ardhi lakini wajanja wakatumia Watanzania wakapata ardhi. Mtu anakuja kwako anasema nitafute ardhi anamiliki. Sasa kule Missouri wanazuia mgeni kumiliki ardhi lakini wanazuia na ma-*gent* na watu wengine ambao wanaweza wakatumika kuwawezesha watu wengine kumilikisha ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa mifano hii ili watu waelewe kwamba tunalolifanya Afrika Mashariki, si jambo geni lakini hata kule Marekani mwaka 1976 walikuwa wana Sheria, *US Agricultural Foreign Investment Disclosure Act. Sheria* ile ilikuwa inakutaka mgeni ukiwa na *interest* kwenye masuala ya ardhi, kwa zaidi ya heka kumi na ndani ya siku 90 lazima utoe taarifa kwamba mimi sio Mmarekani, niko hapa, nina ardhi ili waweze kukujua uko wapi na unafanya nini. Kwa nchi kama USA ambayo na yenyewe inadhibiti masuala ya ardhi, ni dhahiri kwamba nchi za Afrika Mashariki, Waheshimiwa Marais hawajakosea kusema kwamba kwa masuala ya ardhi, zitumike Sheria za nchi wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko hoja nyingine zilizotolewa kwa mfano Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro na Mheshimiwa Fuya Kimbita. Kama nilivyosema, ni vuzuri tuwe makini katika masuala ya Umoja wa Forodha lakini vilevile na Kambi ya Upinzani imelisisitiza hili na nimeeleza kwamba tutakuwa makini. Lakini niseme bahati nzuri ukisoma Itifaki inayoanzisha Umoja wa Forodha, ina mambo ya msingi inayaweka. *Article* ya 19, inasema kwamba, kama nchi yoyote itaona jambo fulani limeleta madhara kwenye hiyo nchi kwa sababu ya kutekeleza Umoja wa Forodha, ina wajibu wa kuchukua hatua za kurekebisha hali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo tulishaliona na tumeshachukua hatua za kurekebisha na liko ndani ya Itifaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiangalia *Article* ya 18, yenyewe inazungumzia masuala ya biashara, unafikiri kuna jambo umefanyiwa na unafikiri kwamba linaleta madhara kwa nchi, kwa hiyo tunaruhusiwa kuchukua hatua za kurekebisha hali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile kuna hiki kitu kinaitwa *anti dumping;* kwamba ikitokea watu wanataka kuleta bidhaa zao huku kwenye soko la Afrika Mashariki kwa gharama ya chini kuliko walivyozizalisha, hatuwezi kukaa tu kimya, tunaruhusiwa kupitia Umoja wa Forodha kurekebisha hali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna kifungu cha 35 ambacho kinasema kama kwenye kutekeleza Umoja wa Forodha itaonekana kwamba kuna nchi inaonekana kuumia zaidi kuliko nchi nyingine basi nchi hiyo inayo fursa kuchukua hatua kurekebisha hali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukiangalia yote haya, ni kwamba kinachotakiwa ni kujipanga vizuri na kuhakikisha kwamba Umoja wa Forodha unakuwa wa neema na ukiangalia mwenendo unavyokwenda, kwa kweli ni wa neema. Ukiangalia tulivyoanza, tulikuwa tunauza bidhaa za mashambani lakini kadri siku zinavyokwenda, mambo yanabadilika na tunazidi kuuza bidhaa zilizobora zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia nchi zote wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ukiangalia Tanzania ukubwa wake, ukiangalia idadi ya watu walio Tanzania, ukiangalia rasilimali zilizo Tanzania na ukichukua ile *logic* ya uchumi kwamba kwenye uchumi wowote ule unaweza ukakuta uchumi unakua lakini unafikia hatua unaacha

kuendelea kukua, tunasema ni *optimum level* lakini unaweza ukakuta uchumi mwingine unaendelea kukua lakini unakua kwa hasara. Kwa hiyo, ndani ya nchi za Afrika Mashariki, ziko nchi ambazo uchumi wake umeshakua umefikia *optimum level* ili uendelee kukua inabidi wafanye mambo makubwa ambayo ni vigumu sana kuyafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiangalia uchumi wa Tanzania, ni uchumi ambao bado unakua na haujafikia *optimum position*. Kwa sababu hiyo, nina uhakika kwa siku chache zijazo, uchumi wa Tanzania, sipendi kutumia neno la kumeza, nitumie neno kwamba uchumi wa Tanzania ndiyo utakuwa uchumi bora na imara kuliko uchumi wowote ule ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ruth Msafiri na Mheshimiwa Blandes, wameelezea umuhimu wa kutumia Mto Kagera kuzalisha umeme mwingi zaidi. Ni kweli hivi sasa kuna mradi ambao tunashirikiana na Uganda, watazalisha *megawatt 10* lakini Mto Kagera kuna uwezekano wa kuzalisha mpaka zaidi ya *megawatt 150*. Changamoto tuliyonayo, ni kutafuta wawekezaji ili kuweza kuzalisha umeme huu na ikiwezekana kuweza kuziuzia hata nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile kuna uwezekano wa kuzalisha hata umeme kwa gesi katika maeneo mengine. Ukienda kule Pangani, ziko njia ambazo zilishawekwa zamani za kuwezesha kufikisha umeme huo Kenya. Nafikiri tukiweza kuwekeza kwenye eneo hili peke yake, tutaweza kutamba katika Afrika Mashariki kwa kuweza kuuza nishati na hivyo kuboresha zaidi biashara yetu katika Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mungai tunamshukuru kwa mchango wake mzuri alioutoa. Labda niseme kwamba Jumuiya ya Afrika Mashariki ya sasa ilivyoundwa, imeundwa kuhakikisha kwamba yale matatizo yaliyopelekea Jumuiya iliyovunjika yasitokee tana. Kwa mfano, sababu mojawapo iliyosababisha Jumuiya ya Afrika Mashariki ivunjike ni kwamba kulikuwa na manung'uniko ya watu kufikiri fulani ana watu wengi wameajiriwa kwenye reli, fulani ana watu wengi wameajiriwa kwenye mashirika ya ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa mfumo wa sasa ni kwamba hatutaraji kwa sasa kuwa na Mashirika hayo makubwa kama ya Afrika Mashariki badala yake tunaweka miundombinu na mazingira mazuri ya mashirika kama hayo kuweza kuendelea kwa kila nchi kushughulikia jambo lake, kwa sababu tusingependa kurudi kule tulikokuwa. Lakini kadri siku zinavyokwenda, kama ikitokea siku moja tukifika kwenye Shirikisho la Kisiasa, huenda tukafikiria kurudi kwenye utaratibu wa zamani. Lakini kwa sasa nadhani tutaendelea na muundo wa sasa uliopo kwa sababu unatusaidia sana kuepusha matatizo ya kuweza kugombana na mambo mengine lakini taasisi hizi zinaweza zikaendelea kushirikiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja ambayo imetolewa na Mheshimiwa Mungai kwamba ni vizuri kama una ardhi kubwa huitumii kama inawezekana achia wengine watumie. Kwa hiyo, tumemsikia Mheshimiwa Mungai; lakini niseme tu Tanzania kama Tanzania wenzetu wengi wakija wakiwa wanapita wanafikiri kwamba tuna ardhi kubwa

lakini ukweli ni kwamba kila ardhi iliyo Tanzania ina kazi yake. Kwa sababu hata kuhifadhi ardhi kwa ajili ya vizazi vijavyo na yenyewe ni kazi kwamba katika mpango wako, unahakikisha una ardhi kwa ajili vizazi vijavyo na hiyo ni matumizi ya ardhi. Tunazo Mbuga nyingi sana za wanyama lakini sote tunafahamu kwamba hadi hivi sasa tunavyozungumza maeneo mbalimbali ya Tanzania kunatokea matatizo ya ardhi ya hapa na pale. Kwa hiyo, nadhani Watanzania tusifikirie kwamba tuna ardhi kubwa na tunaweza kumwita mtu yeyote aje atumie bila utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachosema ndani ya Afrika Mashariki, kama unataka kuja Tanzania wewe ni mgeni, unataka kuja kuwekeza na nini, tutatumia Sheria zetu zilizopo, ni Sheria nzuri tu, tutakupa ardhi, utawekeza, utafanya na mambo mengine lakini kinyume cha hapo inaweza kutuletea matatizo siku zijazo. Tusisahau kwamba nchi nyingi sana duniani watu wanauana, watu wanapigana vita kwa sababu ya migawanyo ya ardhi isiyo mizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja ambalo ni zuri. Nchi zote za Afrika Mashariki hata zile ambazo siku za nyuma zilikuwa zinashangaa Sera ya Ardhi ya Tanzania, hivi sasa zimeanza kuchukua maamuzi kwenda kwenye muelekeo wa kuwa na Sheria inayofanana na ya Tanzania. Kwa hiyo, tuko sahihi, tuendelee kusimamia sera zetu lakini wageni, tunawakaribisha waje wawekeze lakini kwa kutumia Sheria ambazo tumejiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mohamed Rished, tunamshukuru sana kwa mchango wake mzuri, amezungumza masuala ya kuwa na ada zinazofanana. Ni jambo ambalo tutaendelea kulifanyia kazi na kulisimamia. Lakini amesema jambo moja ambalo nakubaliana naye kwa asilimia 100 kwamba, ni vizuri tukaendelea kutoa fursa za upatikanaji wa mikopo kwa sababu kama watu wetu hawataweza kupata mikopo kwa gharama nafuu, basi itakuwa ngumu sana kuweza kutamba ndani ya soko la Afrika Mashariki na ndiyo maana Bunge hili kama mnavyofahamu mlifanya mabadiliko kwenye Sheria ya Ardhi lakini vilevile mmeshafanya mabadiliko kwenye Sheria ambayo inawezesha hata sehemu ya nyumba kuweza kupata hati lakini vilevile kuna utaratibu wa kutumia zile Hati za Kimila. Mabadiliko yote haya yanalenga kuwezesha Watanzania wengi zaidi kupata mikopo mingi zaidi. Ni matarajio yetu na hatua nyingine zitaendelea kuchukuliwa ili kuwawezesha Watanzania kupata fedha na hivyo kuweza kuwekeza zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Prof. Sarungi, tunakushukuru sana, nakupa pole kwa matatizo ya wenzetu hawa 40 waliofariki. Lakini kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri, suala lako tumelipokea na tutalifuatilia kwa karibu kwa kushirikiana na wenzetu ili tuweze kuona tunaweza tukafanya nini kumaliza tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya mgogoro wa Migingo ilitolewa na Mheshimiwa Zambi, Mheshimiwa Omar Ali Mzee na Mheshimiwa Paul Lwanji. Nashukuru Naibu Waziri kwa jinsi alivyojibu labda nisisitize tu. Msimamo wa Tanzania katika hili ni kwamba ni vizuri tukapata ufumbuzi wa tatizo hilo kwa kutumia majadiliano. Ni matarajio yetu, wenzetu wataweza kulimaliza suala hili kwa kutumia

majadiliano. Hata Bunge la Afrika Mashariki, tayari limeshatoa Azimio la kuwataka hawa wenzetu kupata ufumbuzi kwa majadiliano.

Mheshimiwa Juma Said, tunamshukuru sana kwa mchango wake, uliuliza tumejiandaa vipi kuhusu viwanda. Ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki hivi sasa tunaandaa Sera ya Viwanda pamoja na Uwekezaji na Sera ile italenga kuzifanya nchi za Afrika Mashariki zisishindane zenyewe kwa wenyewe. Tunaratarajia Sera hii itatusaidia na Sera hii si mpya, ilishakuwepo kwenye miaka 1960 ingawa utekelezaji wake haukwenda vizuri kama ulivyokuwa umetarajiwa. Lakini vilevile kupitia Wizara ya Viwanda, wameshaeleza mipango mbalimbali tunayoendelea nayo ya kuimarisha viwanda vyetu. Hivi karibuni, mlisikia kwenye ule mpango wa kupambana na kuyumba kwa uchumi duniani, tumeongeza fedha kwa ajili ya *Export Processing* na nyinginezo na ziko *opportunities* mbalimbali ambazo zote zinalenga kwenye kuimarisha viwanda vyetu, tuna masuala ya *Export Processing Zone* na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lubeleje, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa Dr. Mongella na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, wamezungumzia suala la ajira kwamba tuwe makini tunapoenda kwenye soko la Afrika Mashariki tusije tukakuta tunatengeneza tatizo. Mimi nakubaliana nao kwa asilimia 100 na hata ukisoma ile *Wako Report*, ilieleza kwamba suala la ajira ni vizuri kuwa makini kwa sababu si vizuri kusema soko la Afrika Mashariki la ajira ni soko la nchi moja.

Mheshiiwa Mwenyekiti, hilo halitapendeza na ndiyo maana katika mazungumzo yanayoendelea, soko la pamoja tumeshakubaliana kwamba masuala ya ajira yatakuwa *progressive*. Kwa maneno mengine, yataenda hatua kwa hatua. Lakini tumeshakubaliana kwamba kila nchi itaeleza inataka kutoa ajira zipi na kila nchi lazima ieleze inafungua milango kwenye eneo lipi, sio unaenda tu kutafuta ajira. Lakini vilevile tumeshakubaliana kwamba tutafanya *manpower survey* ili kuweza kujua ndani ya Afrika Mashariki nani yupo wapi na anafanya nini. Yote haya yanalenga kutufanya tusilete matatizo kwenye soko la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile kuna suala la kwamba Tanzania hivi sasa tunawekeza sana kwenye elimu, kwenye sekondari na vyuo vikuu, wote mnafahamu kasi tunayoenda nayo. Tukiendelea hivyo, tunauhakika kwamba tutaweza vilevile kufanya vizuri katika soko la ajira. Hivyo, tunauhakika kwamba tutaweza kufanya vizuri katika soko la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru sana Mheshimiwa Anne Kilango kwa mchango wake wa maandishi, ametoa tahadhari kwa kusema kwamba jamani haya mambo ya ushirikiano ni vizuri tukaenda hatua kwa hatua, tusikimbilie kwenye Shirikisho la Kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alichokisema yupo sahihi hata ukisoma Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, kifungu cha 5 (2) kinaeleza kabisa kwamba tutaanza na Umoja wa Forodha, tutaenda kwenye Soko la Pamoja, tutaenda kwenye Sarafu Moja na

baadaye tutaweza kwenda kwenye Shirikisho la Kisiasa. Kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Anne Malecela kwa ushauri wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba Mheshimiwa Mungai alipokuwa anachangia, alielezea umuhimu wa kuwa na Baraza la Mitihani la Afrika Mashariki. Ni wazo zuri na ndiyo maana kupitia *East Africa Universities Council* tayari tumeweka Sheria ambayo inalenga kuangalia mitaala ya elimu na mambo mengine. Kwa hiyo, tunaenda kwenye mwelekeo huo huo kama alivyoshauri Mheshimiwa Mungai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja alilolisema kwamba ni vizuri Sarafu Moja ikaja haraka, tumeunda Kamati ya kuanza kuangalia na tunatarajia Sarafu Moja mwaka 2012. Lakini niseme na hili lieleweke kwamba kwenye miaka 1965, Tanzania ilitoa mapendekezo kwamba badala ya kuvunja ile *East Africa Currency Board* iundwe *Central Bank* ya Afrika Mashariki. Huo ndio ulikuwa msimamo wa Tanzania na Tanzania wakati ule ilikuwa na wazo kwamba tukishakuwa na *Central Bank* tuwe na Shirikisho la Kisiasa kwa wakati ule lakini kwa bahati mbaya msimamo huo uliendelea kubaki kuwa wa Tanzania na wenzetu waliona kwamba ni vizuri kuwa na subira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haya mambo huwa yanabadilika, saa nyingine, mwingine anakuwa na haraka, wakati mwingine anakuwa taratibu na ikibadilika inaonekana huyu ana haraka na huyu anaenda taratibu. Kwa hiyo, haya mambo yanategemea mambo mengi. Matarajio yetu mwaka 2012, tutaweza kuwa na sarafu moja. Lakini yote haya yatategemea jinsi gani hatua moja inavyofanikiwa na kwenda kwenye hatua nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nirudie tena kukushukuru wewe na Waheshimiwa Wabunge. Nikuombe sasa Bunge lako lituidhinishie fedha tulizoziomba ili tuweze kuendelea kutekeleza yale yote ambayo tumeahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**Fungu 97 - Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki**

**Matumizi ya Kawaida**

Kif. 1001- *Administration and General* … …. … ... ... ... ... ..Shs. 1,832,418,600/=

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *vote 97, subvote 1001, item 210100*. Naomba nipate ufafanuzi juu ya bajeti hii kwa sababu kwa kweli naona haitoshelezi. Mimi nadhani wao mambo yao ni mengi lakini pesa iliyopo hapa ni kidogo mno. Wana mipango mingi ambayo wangeweza kupanga, kwa mfano bandari,

*airport* wangeweza kuweka mazingira mazuri ambayo wangeweza kuyapanga lakini sasa pesa hii haitaweza kutosheleza kuweka mazingira mazuri ya bandari, *airport* na mambo mengine ambayo nchi zingine wangeweza kuwakuta kusudi waweze kuyakuta kwa ajili ya...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mikidadi, uliza swali ili Mheshimiwa Waziri aweze kukusaidia.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawasawa. Naomba ufafanuzi juu ya bajeti hii pamoja na swali langu ambalo nimeliuza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fatma Mikidadi, nadhani swali lako ni kwamba kwa nini wameomba fedha kidogo?

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Kwa nini wameomba fedha kidogo?

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kuona umuhimu wa kutenga fedha nyingi. Lakini kama mnavyofahamu, ni kwamba katika muundo wa sasa wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, masuala karibu asilimia 99, yanatekelezwa na nchi wanachama. Kwa hiyo, fedha ambazo tunaomba sisi ni kwa ajili ya kufanya masuala ya uratibu, sasa mambo mengine yanakuwa yanatekelezwa kwenye Wizara mbalimbali. Kwa hiyo, fedha hizi niseme kwamba zinatosha na zitatuwezesha kufanya kazi nzuri zaidi na ukizingatia ukweli kwamba wakati tunaanza Wizara hii tulianza na shilingi bilioni nane lakini sasa tumepanda mpaka shilingi bilioni 14. Ni matarajio yetu kwamba bajeti hii itakuwa inaongezeka kadri siku zinavyokwenda na kadri ya shughuli za Wizara zinavyoongezeka.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani nimekuja nakimbia nilikuwa na shughuli za Kamati. Ninaomba ufafanuzi kwa Mheshimiwa Waziri. Katika mchango wangu wa maandishi, nilizungumzia hoja ya nchi wanachama wa *East Africa*, kuwa na *protocol* ya kubadilishana wahalifu kwa tafsiri kwamba katika maeneo kama vile kule Kigoma au Kusulu, tunapata shida ya wahalifu wanaotoka nchi wanachama wa *East Africa* kutoka Burundi, Rwanda wanakuja kufanya uhalifu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilivyofanya utafiti wangu, nimebaini kwamba hatuna *protocol* ya kubadilishana wahalifu katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kama ameshalitolea ufafanuzi, nitaomba radhi sana kwako lakini ninaomba ufafanuzi Mheshimiwa Waziri anasemaje katika jambo hili. Je, haoni kwamba ni wakati muafaka, nchi wanachama wafikirie kuwa na *protocol* ya kubadilishana wahalifu ili wahalifu hawa katika nchi za Afrika Mashariki, akifanya uhalifu katika nchi moja aweze kurejeshwa katika nchi nyingine. Ninaomba ufafanuzi na sina haja hata kidogo ya kushika mshahara wa Waziri.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Mawaziri la Afrika Mashariki huwa lina sekta ndogo ndogo za Baraza la Mawaziri na kwa kujua umuhimu wa masuala ya ulinzi na usalama na mambo mengine, tayari Jumuiya ya Afrika Mashariki tumeanzisha *Sector Council* zinazohusiana na masuala ya *defence and security* na kupitia eneo hilo wataalam mbalimbali, Wakuu wa Majeshi, Wakuu wa Usalama na Polisi wanakutana mara kwa mara kuangalia eneo hili. Lakini ushauri wake ni mzuri na kwa kuwa sasa hizi *council* tumeshazianzisha za masuala hayo, tunaichukua hoja hiyo ili tuweze kuwa na utaratibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niongeze jambo jingine ambapo kati ya Tanzania na baadhi ya nchi wanachama kuna haya makubaliano ya nchi na nchi. Kwa hiyo hili tutalipeleka kwa sura mbili. Sura ya kwanza tutalipeleka kwa sura ya Afrika Mashariki lakini na sura ya pili kuna vikao vya nchi na nchi, tutalisisitiza vilevile kuweza kuzingatia suala hili.

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kuuliza swali moja dogo kwamba kwa kuwa mnafanya kazi ya uratibu wa kuuza bidhaa zetu nchini Kenya, je, machungwa yaliyozagaa kule kwetu Kilwa Kipatimo yamo?

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru sana Mheshimiwa Dr. Mpanda kwa kutueleza kwamba na yeye kwenye eneo lake kuna uzalishaji mkubwa wa machungwa na napenda niseme kwamba hatua ya kwanza ni kuhimiza kuhakikisha kwamba badala ya kuuza machungwa tuweze kuuza juice na mambo mengine. Lakini hata kama ni kuuza machungwa ambalo na lenyewe si jambo baya, basi machungwa hayo yaweze kuuzwa kwa taratibu nzuri. Niseme tu, katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Kenya ni mojawapo la soko la uhakika ambalo tukijipanga vizuri, tutaweza kunufaika nalo. Kwa hiyo, tutawasiliana na Wawekezaji mbalimbali, tutahamasisha na watu wengine ili tuone ni kwa jinsi gani tunaweza tukatekeleza ombi la Mheshimiwa Dr. Mpanda kuhakikisha kwamba na machungwa ya kule yanapata soko katika Afrika Mashariki.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, kwa kazi nzuri kwa kweli wanayoifanya kutetea maslahi ya nchi yetu kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ninahitaji ufafanuzi kwenye ukurasa wa 37 na 38 ya hotuba yake. Mheshimiwa Waziri amezungumzia habari ya mtandao wa barabara ambazo zinatambuliwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika mtandao wa Kanda ya Tano, amezungumzia barabara ya Tunduma, Iringa, Dodoma Arusha, Namanga na Moyale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, tunapongeza jitihada za Wakuu wa nchi wanachama, kuzindua rasmi ujenzi wa barabara ya Arusha – Namanga - Usa River lakini nilitaka nifamhamu sasa kwamba hapa katikati tulimbana Waziri wa Miundombinu kuhusu kipande cha barabara kutoka Iringa, Dodoma mpaka Babati ambacho hakina lami na bado hakijapata wafadhili, kipande cha Dodoma Babati, kwa kuwa zimetajwa hapa na Mheshimiwa Waziri, nilitaka kujua kwanza, sina hakika, yeye anapokwenda Arusha

akiwa hapa anapitia wapi? Anapitia Chalinze kwenda Arusha au anapitia Babati kwenda Arusha? Sasa ufafanuzi ninaohitaji ni huu, je, wajibu sasa wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa Kanda hii ya tano ni nini katika kuisaidia Serikali ya Tanzania kuhakikisha kwamba Wafadhili wanapatikana kujenga kipande hiki ambacho hakina lami?

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Namshukuru Mheshimiwa Kwaangw' kwa hoja yake. Labda nimwambie tu, ninapokuwa nakwenda Arusha huwa napita Babati kwa sababu njia hii ni karibu kuliko kuzunguka Chalinze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya ya Afrika Mashariki kitu ambacho tunakifanya hivi sasa ni kuwasiliana na Mashirika mengi ya Fedha duniani. Unapokwenda kutafuta fedha za kujenga barabara, kama barabara hiyo inaishia kwenye nchi, itakuwia vigumu kupata fedha, kama ukienda kuitangaza barabara ambayo inaonekana ni ya kikanda kama ilivyo barabara hii. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutafanya kila linalowezekana kuhakikisha kwamba fedha za barabara hii zinazohitajika, zinapatikana. Tunaitangaza katika mashirika mbalimbali ili tuweze kupata fedha za kuijenga lakini si hii tu na barabara zingine ambazo tunasema ni barabara za Afrika Mashariki na tayari Wakuu wa Wanchi wametuagiza Mawaziri wa Afrika Mashariki, tuongeze kasi ya kutafuta fedha za kuhakikisha miundombinu ya barabara za Afrika Mashariki zote zinaweza kutengenezwa kwa kiwango cha lami.

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo ambayo Mheshimiwa Waziri ameyatolea ufafanuzi juu ya Kanda ya Tano ambayo yanafanana na lile ambalo nilikuwa nataka kupata ufafanuzi kwenye kanda ya pili. Pamoja na kwamba barabara ya kutoka Tanga - Pangani -Bagamoyo badala ya Saadani - Bagamoyo; imeshafanyiwa *feasibility study* na tunafahamu kwamba hii barabara iko katika mpango wa Afrika Mashariki, ni hatua gani sasa ambazo zinachukuliwa ili kuweza kuona barabara hii imeingia katika mchakato wa kutengenezwa kwa kiwango cha lami na unafikiri inaweza ikachukua muda gani pamoja na kwamba si rahisi lakini kutafuta wafadhili na mwelekeo unavyokwenda, matumaini katika barabara hii yakoje?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Rished, ni kwamba barabara hii, hivyo unavyoitamka wewe ndivyo ilivyo hasa, Tanga – Pangani – Saadani – Bagamoyo. Barabara kutoka Horohoro – Tanga, tayari upembuzi yakinifu umekamilika na ujenzi unatarajia kuanza si muda mrefu chini ya ufadhili wa *MCC*. Hivi sasa, Serikali ya Tanzania, kwa kushirikiana na Jumuiya ya Afrika Mashariki, inafanya upembuzi yakinifu kwa lile eneo la Tanga – Pangani – Saadani – Bagamoyo. Mara baada ya kumaliza upembuzi yakinifu huu, basi hapo tutaanza kuchukua hatua za kutafuta wafahili kwa ajili ya kujenga barabara hiyo. Kwa sasa, siwezi kukwambia muda gani itachukua, lakini tutajitahidi iwe mapema iwezekanavyo kwa sababu ni barabara muhimu, tunajua umuhimu wake kwa kusaidia maendeleo ya Bandari zote mbili ya Tanga na Dar es Salaam.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya*

*Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 – *Finance and Accounts* ... ... ... ..Tsh.261,249,800/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif.1003 – *Policy and Planning*.. . ... ... ... Tsh.8,975,532,700/=

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 97, kifungu kidogo 1003, kifungu kidogo zaidi 220800, *Training Domestic*. Mwaka 2007/2008, hawakupata pesa, mwaka 2008/2009 pia hawakupata pesa lakini katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri inaonyesha kwamba mafunzo ya ndani yalifanyika. Ninapenda tu kufahamu mafunzo haya yalifanyika kwa kutumia fedha ipi? Kwa fedha hii ambayo wanapewa sasa kwa ajili ya kufanya mafunzo ya ndani, ni mafunzo ya aina gani wanayotegemea kuyafanya? Ukitazama katika kifungu kile cha 122, ukurasa wa 65 wa kitabu cha hotuba, utaweza kuona kwamba kuna watumishi kama 40 ambao watapata mafunzo ndani na nje lakini pia katika kifungu hiki kidogo cha 220900…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nyami, tunaomba uulize unachotaka kukifahamu, uliza swali!

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kufahamu ni mafunzo gani ya ndani ambayo wanataka kuyatoa na fedha gani ilitumika kutoa mafunzo ya ndani wakati hapakuwa na kifungu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nyami, swali ni moja tu. Mheshimiwa Waziri atajibu swali moja hilo la mwanzo.

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako, naomba kumjibu Mheshimiwa Nyami kama ifuatavyo:-

Mafunzo ni ya aina mbalimbali kwa ajili ya watalaam wetu. Lakini hapa unapoona fungu hilo la 22800, Mheshimiwa anaona kwamba ni dogo; katika kila fungu akitizama, hii ni sehemu ya *Policy* na *Planning* lakini akienda kwingine...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, hizi shilingi milioni 18 zinataka kufanya kazi ya kufundisha kitu gani? Ndiyo swali lenyewe lilivyokuwa.

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Ni mafunzo ya ndani ya nchi ya watalaam wetu.

**MWENYEKITI:** Basi imetosha hiyo!

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Niko katika *subvote* 1003, *sub item 221000 – Travel in Country*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia fungu hilo, utaona kwamba kuna ongzeko la zaidi ya shilingi milioni 220, ukilinganisha na mwaka jana. Ninaomba kupata ufafanuzi, hizi safari za ndani kwa mwaka jana zilikuwaje na kwa nini mwaka huu wameongezewa fedha kiasi hicho?

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyofahamu, kila mwaka kila Wizara inakuwa na shughuli mbalimbali ambazo inapanga kwamba ziweze kufanyika. Kwa hiyo, mwaka mwingine mnapanga, fedha inakuwa haitoshi, kwa hiyo, mnapata kidogo, mwaka mwingine mnapanga shughuli zile zile na fedha ikipatikana, basi zinaweza kupatikana. Kwa hiyo, shughuli za kufanya ndani ya nchi ziko nyingi ukizingatia kwamba kazi ya Wizara hii ni kuratibu na vikao vingi vinafanyika kule Arusha ambayo ni *travel in country* ambayo inabidi twende, maana ukikosekana kwenye kikao kwa sababu yoyote ile, mkutano huo unakuwa umeahirishwa na saa nyingine maslahi ya nchi yako yanaweza yakapotea kwa kushindwa kuhudhuria vikao.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1004 – *Trade, Finance and Investment...* ... ... ... ... ... TShs.1,039,077,600/=
Kif. 1005 – *Economic and Social Infrastructure...* ... ... ... ... ..TShs.670,162,400/=
Kif. 1006 – *Political, Defense and Security...* ... ... ... ... ... ... ...TShs.318,240,100/=
Kif. 1007 – *Procurement Unit...* ... ... ... ... ... ... ... ... TShs.186,407,300/=
Kif. 1008 – *Information, Education and Communication...* ... ... .TShs.113,869,000/=
Kif. 1009 – *Management Information System...* ... ... ... ... ... ... ... TShs.201,172,000/=
Kif. 1010 – *Internal Audit Unit...* ... ... ... ... ... ... ... ... ... Tsh.117,776,700/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1011 – *Legal Services Unit...* ... ... ... TShs.167,787,700/=

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kidogo 210100 – *Basic Salary*. Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia utaona kwamba watu hawa wa Kitengo cha Sheria, hawana mshahara. Ninaomba ufafanuzi ni kwa nini hawana mshahara?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwenye 210100 mwanzo kabisa hapo, sehemu ya pili inaonekana kwamba pana sifuri kwa mwaka 2009/2010 kwa maana ya kwamba hawa watu watakuwa hawana mshahara. Lakini mwaka 2008/2009 pana shilingi 8,342,100/=. Sasa swali lake hasa liko hapo, kwa nini hapa pana sifuri?

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa yao imetengwa kwenye fungu la *Administration and General*.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**FUNGU 97 – WIZARA YA AFRIKA MASHARIKI**

Kif. 1001 – *Administration and General*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...TShs.0/=
Kif. 1003 – *Policy and Planning*... ... ... ... TShs. 146,789,000/=
Kif. 1004 – *Trade, Finance and Investment*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... TShs.0/=

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, Bunge limekaa kama Kamati ya Matumizi, limeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kwa Mwaka 2009/2010, kifungu hadi kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo basi, naliomba Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio hayo. Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja!

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki!

(*Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka 2009/2010 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijakamilisha shughuli yetu jioni hii ya leo, kwanza nichukue nafasi kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na watendaji kwa kutuwasilishia vizuri sana hii bajeti na namna alivyoweza kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, nampongeza sana na namtakia jioni njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla sijamaliza, basi nichukue nafasi hii, nitoe matangazo mawili niliyonayo hapa kwenye meza yangu. Kwanza, kuna wageni wa Mheshimiwa Idd Azzan, Mbunge wa Kinondoni kutoka Kundi la Taarab, Jahazi *Modern* Taarab, likiongozwa na Mzee Yussuf Mfalme, wakiwa na mwimbaji wao mpya, Bi. Mwanahawa Ally. Kama wamo humu ndani, naomba wasimame! Waheshimiwa Wabunge, wanaomba kumuona huyo Mzee Yussuf Mfalme.

*(Hapa Mzee Yussuf (Mfalme) alisimama)*

**MWENYEKITI:** Ahsanteni sana! Bi. Mwanahawa naye sasa tunaomba kumuona!

*(Hapa Bi. Mwanahawa alisimama)*

**MWENYEKITI:** Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kesho tarehe 18 Julai, 2009 kutakuwa na Burudani ya Waheshimiwa Wabunge kwa hisani ya NMB kama ifuatavyo:-

Kuanzia saa 9.00, mpira wa miguu na mpira wa pete na kuanzia saa 2.00 usiku kutakuwa na tafrija kwenye viwanja vya Bunge, jengo la utawala. Bendi itakayotumbuiza ni Sakistar na Mgeni rasmi atakuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mpaka hapo ndio tumefikia mwisho wa shuguli za leo kwa sababu kwenye *Order Paper*, shughuli zote ambazo zimepangwa kufanyika leo zimeshakamilika. Kwa maana hiyo, nachukua fursa hii sasa kuliahirisha Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 12.12 Jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumamosi Tarehe 18 Julai, 2009 Saa Tatu Asubuhi)*